**29 JANUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

### Kikao cha Pili – Tarehe 29 Januari, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (Na. 3) Bill, 2024)*; na

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024)*.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA: -**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu: -

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024)*; na

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024)*.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 21

### Fedha za Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Misughaa, Issuna na Mang'onyi – Singida

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za kujenga Vituo vya Afya Kata za Misughaa, Issuna na Mang'onyi?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa kata ambazo hazina vituo vya afya kote nchini ikiwemo Kata za Issuna, Misughaa na Mang'onyi katika Jimbo la Singida Mashariki. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipeleka shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Ntuntu na Iglanson katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ikungi itatenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Issuna. Kata za Misughaa na Mang'onyi zitajengewa vituo vya afya kwa awamu kwa kuzingatia mahitaji na vigezo vilivyoainishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nichukue nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni kwamba Jimbo la Singida Mashariki lina kata 13, lakini vituo vya afya vipo kwenye kata mbili tu ambazo ni Ntuntu pamoja na Unyahati, kata 11 hazina vituo. Ninaomba nipate majibu ya Serikali kwamba, kata za kimkakati nilipeleka Misughaa ambayo tulitarajia kupelekewa fedha mpaka leo hatujapata, lakini Kata ya Issuna, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Emmanuel Nchimbi alishasema kituo hicho kijengwe mapema kabla ya uchaguzi. Sasa ninaomba nipate jibu la Serikali, ni lini sasa fedha hizo zitapelekwa kwa ajili ya kujenga vituo hivyo? Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kituo hiki cha Afya cha Ntuntu ni miaka mitatu kama alivyosema kimepelekewa fedha, hakijakamilika mpaka sasa kwa kutoa huduma, ni *OPD* pekee yake inafanya kazi, jengo la mama na mtoto ambalo ilikuwa ni

lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto havijakamilika. Ninaomba kujua *commitment* ya Serikali, imeshanijibu hapa itapeleka baada ya miaka miezi miwili, miezi miwili imeshapita. Ninaomba kujua ni lini sasa ...

**SPIKA:** Mheshimiwa, umeshauliza swali.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa kituo hicho kitajengwa ili wananchi wale waweze kupata huduma hiyo ya afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maswali yake mawili; kuhusiana na swali la kwanza, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya kuhakikisha inaimarisha huduma za afya msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali katika huu mwaka wa fedha italeta fedha shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha mkakati katika majimbo yote ya Tanzania Bara, ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa shughuli za Serikali. Nimhakikishie kwamba ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Issuna kitatekelezwa na Serikali inatafuta fedha ili ihakikishe ahadi iliyotolewa na kiongozi wetu, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nichukue nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kutumiza wajibu wake wa msingi, kwa

sababu fedha zilishaletwa kwa ajili ya kuhakikisha Kituo hiki cha Afya cha Ntuntu kinajengwa, asimamie na kama kuna fedha zimepungua aongeze kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ili majengo haya muhimu hasa ya mama na mtoto yaweze kukamilika na huduma ya afya iweze kutolewa kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndakidemi, niliokuona.

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena, uliza swali moja kwa moja kwa sababu dakika zilizohesabiwa kwa kila swali ni nne, kwa hiyo na yale ya nyongeza na kila kitu, dakika ni hizo hizo ili tuweze kwenda na muda, lakini pia kutoa nafasi kwenu kuwakilisha zile hoja za wananchi. Uliza swali moja kwa moja, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ni kama alishajibu, nilitaka kuuliza je, ni lini Serikali itajenga kituo cha kimkakati katika Kata ya *Old Moshi Mashariki*? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwamba Serikali katika huu mwaka wa fedha italeta fedha shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo yote Tanzania Bara ikiwemo Kituo hiki cha Afya alichokitaja cha *Old Moshi Mashariki.*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa.

Na. 22

**Sekondari ya Rubanga – Geita Kuwa ya Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Rubanga iliyopo Geita kuwa ya kidato cha tano na sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, shule za kidato cha tano na sita za bweni ni za Kitaifa na huchukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini. Jimbo la Geita kwa sasa lina shule moja ya kidato cha tano na sita ambayo ni Bugando.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Rubanga bado haijakidhi vigezo vya kuipandisha hadhi kuwa ya kidato cha tano na sita ikiwa ni pamoja na kutokuwa na mabweni, bwalo na madarasa ya kutosha. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kuendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili Shule ya Rubanga iwekwe kwenye mpango wa kupandishwa hadhi kuwa ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya shule za sekondari ikiwemo Shule ya Sekondari ya Rubanga kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Katika halmashauri hii, je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Evarist iliyopo

Nyarugusu kutoka Wilaya ya Geita kuwa kidato cha tano na cha sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpa majibu Mheshimiwa Tumaini Magessa kuhusiana na swali lake hilo kwamba Serikali itaendelea kufanya tathmini na kupita kufanya *verification* katika shule mbalimbali Tanzania nzima ikiwemo katika jimbo lake. Shule hii ya Evarist na yenyewe itapitiwa ili kufanya uhakiki na kufanya tathmini na kuleta fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ambayo inahitajika kwa ajili ya shule kuwa na vigezo vya kupandishwa kuwa kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kazi hiyo itafanywa na Serikali ili shule hizi zipandishwe hadhi na ziweze kuwanufaisha wanafunzi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Watumishi wa Afya Kujaza Ripoti za Utendaji Kila Mwezi**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, kwa nini watumishi wa afya wasijaze ripoti za utendaji kazi kila mwezi badala ya kila wiki ili wapate muda zaidi kuhudumia wagonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, lengo la utoaji taarifa za utekelezaji wa mipango ya Utendaji Kazi ya Watumishi wa Umma katika vipindi tofauti ni kuwezesha kubaini mwelekeo wa utekelezaji katika kufikia malengo ya taasisi kwa ujumla. Aidha, taarifa za utekelezaji wa mipango ya utendaji kazi ya watumishi zinajadiliwa katika vikao vya taasisi vinavyofanyika kila wiki kwa lengo la kubaini hali ya utendaji kazi wa taasisi husika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa afya na watumishi wengine wa umma wanapaswa kuendelea kutoa taarifa za utekelezaji wa mipango yao ya utendaji kazi katika kipindi cha siku, wiki na kadri itakavyohitajika. Lengo ni kubaini changamoto zinazojitokeza kipindi cha utekelezaji na kuweka mikakati ya kuzitatua kwa wakati. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kukagua au kutoa ripoti ni suala muhimu sana katika kuwasimamia wafanyakazi, lakini kada ya afya ni kada muhimu sana ambayo inaokoa maisha ya watu. Hamwoni kuna namna kwa kada hii pekee ikapewa nafasi ya kutoa kwa mwezi badala ya kila siku, kwa sababu saa 24 ni saa za kuangalia wagonjwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa upimaji watumishi kupitia *PEPMIS* tumeweka kwa muda kwa wiki kwa makusudi maalum kwamba tuweze kutambua tatizo kwa muda mfupi na kulitatua. Kuweka muda wa mwezi mmoja haitaweza kutusaidia kwa sababu tutakosa kupata *consistency* ya majukumu aliyoyafanya

mtumishi kwa sababu itakuwa ni muda mrefu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na tangu tumeanza zoezi hili hatujapata malalamiko ya hawa watumishi moja kwa moja, kwamba jambo hili linawasumbua, wameendelea kujaza hiyo *PEPMIS* kwa wakati na mpaka sasa zoezi hili linaendelea vizuri. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Watumishi Walioathirika na Mwongozo wa Upandaji Madaraja wa Miaka Minne**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kukwamua watumishi walioathiriwa na Mwongozo wa Upandaji Madaraja wa Miaka Minne?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukuwa jitihada mbalimbali za kuoanisha na kuwianisha upandishaji wa vyeo vya watumishi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imewapandisha vyeo watumishi 180,000 wakiwemo watumishi walioathirika na zoezi hilo. Aidha, katika utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya mwaka 2023/2024, Serikali imewapandisha vyeo watumishi zaidi ya 232,530 wakiwemo walioathirika na zoezi hilo, uhakiki wa vyeti *fake* na watumishi hewa. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini hawa watumishi waliokumbwa na miaka minne na watumishi wa miaka mitatu sasa

wamewapandisha kwa pamoja, wote wamekuwa kwenye *position* moja. Swali la kwanza; ninaomba Serikali inielezee ni utaratibu gani watachukua kuleta *seniority* kati ya wale waliokumbwa miaka minne na hawa wa miaka mitatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; walimu waliajiriwa mwaka 2012 walisahaulika, sasa walivyokuja kupandisha vyeo wamepandisha wa mwaka 2013, 2014 na kuendelea. Sasa ni utaratibu gani watachukua ili hawa sasa waonekane kuwa ni ma-*senior* kwa hawa waliongia miaka iliyofuata? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Janejelly kwa namna anavyofuatilia mambo ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa walioathirika na miaka minne, Serikali tumechukua hatua ambako mpaka sasa tumebaki na kiasi kidogo cha watumishi hao ambapo jitihada ambayo inafanyika sasa, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 tutahakikisha watumishi wote walioathirika na kupanda vyeo miaka minne wanapandishwa kwa mserereko ili waweze kuwa sawa na wengine wale waliowatangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu walioajiriwa mwaka 2012 na watumishi wengine ambao walitakiwa kupanda vyeo mwaka 2016 na *promotion* zilisitishwa kwa sababu ya uhakiki. Ninaomba nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, hawa mpaka sasa tuna idadi ya watumishi 6,559 ambayo kwa mwaka huu wa fedha tumepanga bajeti na kama kuna wachache watakaosalia tutawakamilisha katika mwaka wa fedha utakaofuata kwa maana ya 2025/2026. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna watumishi wamestaafu toka mwaka 2020 mpaka sasa bado

hawajapata mafao yao na kwa kuwa waajiri hawakupeleka fedha kwenye mifuko. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha watumishi hao wanapata mafao yao? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya watumishi wanaostaafu wanacheleweshewa kulipwa mafao kwa sababu moja tu baadhi ya waajiri wamekuwa wazembe wa kufikisha taarifa zao katika Ofisi ya Rais, Utumishi ili tuweze kuwa-*process* kwa wakati na Mheshimiwa Zodo ni moja ya mtu aliyeniletea kero hiyo ofisini na tunaishughulikia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie Bunge lako kuwataka waajiri wote kwamba wastaafu wanapomaliza muda wao hili jambo sio la dharura, ni jambo ambalo linafahamika, watimize wajibu wao wa kuleta taarifa kwa wakati ili Ofisi ya Rais, Utumishi tuweze kushughulikia suala hilo kwa wakati. Kama kuna wengine watabainika na tulipitisha sheria hapa ndani ya Bunge tutawachukulia hatua kwa sababu kama Serikali hatutaki kuona wastaafu wa nchi hii wananyanyasika wakati wamefanya kazi yao kwa uadilifu kwenda kutumikia Taifa lao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali inazungumza nini kuhusu watumishi wanaojitolea katika kada mbalimbali hususani kada ya elimu ambapo kuna watumishi wapo huko wamejitolea kwa zaidi ya miaka sita na kumi sasa hivi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mara kadhaa ndani ya Bunge hili mjadala huu umeibuka juu ya vijana wetu wanaojitolea katika sehemu mbalimbali siyo tu kada ya ualimu, lakini tulitoa *commitment* kama Serikali ndani ya Bunge kwamba tutaenda kufanyia mchakato jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilihakikishie tena Bunge lako, mchakato huu umefika katika hatua ya mwisho na tutaomba ruhusa yako (kibali) pia tukishirikishana na Kamati ili tuweze kuliboresha vizuri na baadaye tutatoa sasa mwongozo katika mwaka huu wa fedha namna ambavyo tuta-*accommodate* vijana wetu wanaojitolea. Kama Serikali tunatambua kujitolea kwao na tunathamini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Kupeleka Umeme Vitongoji Visivyo na Umeme – Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme vitongoji visivyokuwa na umeme Wilaya ya Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, kwa kuwa jana limefanyika tukio la kihistoria la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Wakuu wa Afrika, ninaomba kwa ridhaa yako nimpongeze kwa uongozi wake wa mfano uliopelekea Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu jana wakati akimkaribisha Mheshimiwa Rais kuzungumza, alisema Tanzania tumepata heshima hii kwa sababu mbili. Moja, kwa umadhubuti wa Mheshimiwa Rais wa kuendeleza sekta ya nishati Tanzania na Afrika; na la pili, kwa Mheshimiwa Rais kutambulika kimataifa kama *champion* wa nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, ninaomba kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mkutano huu uliowaleta Wakuu wa Nchi na kuweka msimamo wa *Mission* 300 kuelekea 2030. Heko Afrika! Heko Tanzania! Heko Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2024, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imefanikiwa kupeleka umeme katika vitongoji 146 kati ya 355 sawa na 41.1% vilivyopo katika Wilaya ya Kakonko, Mkoani Kigoma. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, vitongoji 15 vya Wilaya ya Kakonko vinatarajiwa kupelekewa umeme kupitia mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Vitongoji vilivyosalia vitaendelea kupelekewa umeme kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Aidha, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; wakati utekelezaji huo ukifanyika wa 41%, upelekaji huo haukuzingatia kupeleka umeme kwenye taasisi za Serikali na binafsi hasa misikiti, makanisa na shule za msingi za Serikali. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba taasisi hizo zinapata umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati utekelezaji huu ukifanyika, ulikwenda sambamba na ufyekaji wa mashamba ya miti, migomba, mahindi na kadhalika katika mashamba ya wananchi. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi ambao mashamba yao yaliharibiwa wanapewa fidia? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu kupeleka umeme kwenye taasisi za Serikali na taasisi binafsi hususan makanisa pamoja na misikiti, Serikali ilikuwa na mradi ambao tulikuwa tunauita UVIKO-19 ambao umepeleka umeme katika taasisi zaidi ya 400. Kwa hiyo, kwa eneo hili la Kakonko, kama bado kuna maeneo ya taasisi ambayo hayajafikiwa na umeme, ninamwelekeza Meneja wa Wilaya kwa bajeti waliyonayo kwa maeneo ambayo yanafikika waendelee kufikisha umeme kwenye taasisi hizo. Sisi kupitia miradi ambayo tunayo ambayo inaendelea na miradi ambayo itaanza kwa mwaka huu wa fedha, tutaangalia maeneo hayo kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fidia kwenye Miradi ya *REA*, Miradi ya *REA* ni miradi ambayo imejikita kupeleka huduma kwa jamii na miradi ambayo imetekelezeka kwenye vijiji vyote kwa misingi hiyo, ni miradi ambayo haina fidia. Tunawashukuru wananchi wote kwa utayari wao wa kupisha maeneo ili kupitisha miradi hii ambayo leo imepelekea kufikisha umeme kwenye vijiji 12,318 na tunawaomba waendelee na moyo huo huo kwa Miradi ya *REA* inayofuatia kwenye vitongoji, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ninarejea tena, usitoe historia, nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji vya Mkoa wa Simiyu ambavyo havina umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tunayo miradi ambayo inaendelea ikiwemo miradi ya vitongoji 15, lakini kwa mwaka huu wa fedha tunategemea kuanza mradi mkubwa kupeleka umeme kwenye vitongoji 4,000 na Mkoa wa Simiyu na wenyewe utanufaika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kitongoji cha Mwanghalaja na Jineli ambavyo havina umeme kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, vitongoji ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge, nitaenda kuviangalia kama vipo katika miradi inayoendelea na kama havipo basi tutavipa kipaumbele katika miradi inayofuatia ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji vilivyopo katika Wilaya ya Newala, Mtwara Vijijini na Masasi ambavyo mpaka sasa havijaunganishwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, vijiji hivi vya Newala, Mtwara pamoja na Masasi, kote wakandarasi wako *site* na walikuwa kwenye hatua za mwisho za utekelezaji. Tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawasimamia ili kwa muda ambao wamesema ambao ni muda mfupi uliobakia, waweze kukamilisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, kwenye vitongoji 15 ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, mnapelekea umeme kwa kila jimbo, inasemekana ni vile ambavyo viko karibu na *line* kubwa, vile ambavyo viko mbali na *line* kubwa…

**SPIKA:** Swali, swali, swali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, kwa nini hizo fedha zisibaki kwenye hivyo vitongoji hata kama viko nje na *line* kubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, namna ambavyo miradi hii imekuwa *designed*, ni kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo ya vitongoji ambavyo tayari vimepitiwa na *line* kubwa. Ninampa faraja Mheshimiwa Mbunge, kwa mradi ambao tunaenda kuanza sasa, vile ambavyo viko mbali na *line* kubwa na vyenyewe vimewekwa kwenye mpango na vitaanza kupatiwa umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapelekea umeme kwenye vitongoji zaidi ya 58 katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambavyo kwa sasa hakuna umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tumeanza na vitongoji 15 na katika mradi ambao tutaanza hivi karibuni na vyenyewe tutaongeza idadi ya vitongoji ili wananchi wa eneo la Mheshimiwa Mbunge waendelee kupata umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, ni lini Vitongoji vya Kwemashai, Muheza, Nkaloi na maeneo mengine yatapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba nitaenda kuangalia kama vitongoji hivi tayari tumeshaviweka kwenye mipango yetu na kama havipo basi tutavichukua kwa ajili ya miradi inayofuata ya kupelekea umeme kwenye vitongoji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, Vitongoji vya Wilaya ya Kyerwa zaidi ya 300 havina umeme. Nini mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme katika vitongoji hivyo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo yana vitongoji vingi zaidi ambavyo havina umeme, miradi inayofuata vilevile tutakuwa tuna *consideration* ya maeneo ambayo vitongoji vingi havijafikiwa. Kwa hiyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa Jimbo hili la Kyerwa pia tutaliangalia kwa jicho la kipekee. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Kupunguza Bei ya Gesi ya Matumizi ya Nyumbani**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza bei ya gesi ya matumizi ya nyumbani kwani wananchi wengi wamepata mwamko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 ambapo pamoja na masuala mengine, Serikali imejikita katika kuhakikisha inapunguza bei ya gesi ya mitungi ya kupikia *(LPG)*. Vilevile, Serikali inaendelea na utoaji wa ruzuku ya 20% – 50% ya bei ya mitungu ya gesi ya *LPG* kwa watumiaji wa mwisho. Aidha, Serikali itaendelea kuja na mikakati mingine ili kuhakikisha bei ya gesi inapungua. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza mawakala wa gesi vijijini ili kuwasaidia wananchi kupata huduma kwa urahisi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vya kujazia gesi kwenye magari maeneo yote nchini ikiwemo Zanzibar? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, moja, kwenye upande wa kuongeza mawakala, tayari tumeanza mazungumzo

na kampuni za *LPG* ili kuhakikisha tuna-*map* maeneo yote ili wananchi wakitaka kujaza gesi, basi wajaze gesi hiyo kwenye mitungi kwa urahisi. Tunaendelea na mikakati hii, mpaka sasa tumefikia tu miezi sita ya utekelezaji wa mkakati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunalifanyia kazi kwa ufanisi mkubwa sana ili wananchi waweze kujaza gesi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vituo vya kujaza gesi kwenye magari, kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo mbalimbali, kwa Dar es Salaam tuna ujenzi wa vituo vitatu ambavyo tunajenga kwa ajili ya kupunguza foleni ambayo ipo katika vituo vya *CNG*. Vilevile, kwa kushirikiana na sekta binafsi tunavyo vituo vingine ambavyo tunavijenga lakini kupitia Shirika letu la Maendeleo ya Petroli, tunanunua vilevile magari ya kuhamishika kwa ajili ya kuhakikisha barabara nzima kuanzia Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma kuna vituo hivi kwa ajili ya kuwarahisishia wananchi wanaotaka kujaza gesi kwenye magari.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea kulifanyia kazi jambo hili kwa ufanisi mkubwa sana ili wananchi waendelee kuwa na moyo wa kuweka mifumo ya gesi kwenye magari yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pamoja na kupunguza bei ya gesi, kuna maeneo ambayo bado haitakuwa nafuu zikiwemo nyumba za malezi za masista kama Huruma. Serikali ina mpango gani wa kuwapa ruzuku maeneo hayo ili waweze kuwa na ile mitungi mikubwa ya mapipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli maeneo hayo ni maeneo muhimu sana kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Kwa sababu tunaendelea na utekelezaji wa mkakati huu tunaomba watupe muda, tutakuja na mikakati

ambayo kwa kweli itakuwa jumuishi kwa aina zote za makundi katika jamii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaelekea Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Kuanza Kazi kwa Mnada wa Mifugo Kileo – Mwanga**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini mnada wa mifugo uliojengwa Kata ya Kileo - Mwanga utafunguliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mnada wa Mpakani Kileo bado haujafunguliwa kwa kuwa mnada ulihitaji ukarabati wa miundombinu muhimu ya vyoo na sehemu ya kupakilia mifugo ambavyo ni muhimu katika shughuli za mnada. Hata hivyo, ukarabati wa miundombinu hiyo ulikamilika mwezi Oktoba, 2024.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji kuhusu matumizi na kuanza kutumika kwa mnada ulifanyika katika Vijiji vya Kifaru, Kileo na Kivulini ambapo waliweza kupendekeza siku ya Jumatano kuwa iwe siku ya mnada. Aidha, Tarehe 4 Desemba, 2024 ilipangwa mnada uanze rasmi, lakini kulitokea changamoto ya kuharibika kwa miundombinu ya barabara kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. Hadi kufikia sasa, jitihada za halmashauri zinaendelea na tayari wamewasiliana na *TARURA* kwa ajili ya kuona namna ya

kurekebisha barabara hiyo. Pindi changamoto hiyo itakapotatuliwa mnada wa Kileo utafunguliwa na kuanza kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Serikali, ninashukuru, sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 28

**Bajeti ya Elimu kwa Umma kuhusu Utekelezaji wa Masuala Mbalimbali Nchini**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti kubwa ya elimu kwa umma kwa masuala mbalimbali yanayotarajiwa kutekelezwa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ya jamii. Katika kuhakikisha kuwa jamii inapata uelewa wa kazi mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali. Wizara zote na taasisi zake zinasisitizwa kutenga fedha kwenye mafungu yao kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji na mafanikio ya shughuli na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa muundo na mgawanyo wa majukumu ya Serikali, jukumu hili linatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Wizara ya Habari, Michezo, Utamaduni na Sanaa pamoja na vitengo vya mawasiliano Serikalini katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Massaburi, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali imejipangaje kufanya kampeni kabambe ya elimu kwa umma kwa maeneo ambayo yataleta tija kwa wananchi na hata kwa Taifa? Maeneo kama kilimo cha kisasa, mtu ni afya, usalama barabarani, upandaji wa miti na utunzaji wake, elimu ya makuzi ya vijana na elimu ya mlipakodi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Massaburi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga katika mikakati mbalimbali kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vyetu vyote,vya habari *TV*, magazeti na mabango mbalimbali. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, hata yeye asaidie katika kueleza na kutoa elimu kwa umma kwa mafanikio makubwa sana ambayo yamepatikana hasa Awamu hii ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, sasa aulize swali lake.

Na. 29

**Kumaliza Ujenzi wa Barabara ya Katumba – Mbambo – Tukuyu**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Barabara ya Katumba Mbambo hadi Tukuyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza ujenzi wa Barabara ya Katumba – Mbambo – Tukuyu yenye urefu wa kilometa 83 kwa awamu. Sehemu ya kutoka Lupaso – Mbambo kilometa 20 na kutoka Kabanja hadi Tukuyu kilometa saba ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika. Sehemu iliyobaki ya kutoka Katumba – Lupaso kilometa 35.3 na Mbaka – Kibanja kilometa 20.7 mikataba ya ujenzi imesainiwa na kwa sasa mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi baada ya kulipwa malipo ya awali. Kazi zimepangwa kukamilika mwezi Mei, 2027 kwa sehemu zote mbili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Kati ya ninyi mnaosimama kwa ajili ya maswali ya nyongeza, wale mliouliza jana mtaketi ili wasimame wale ambao hawakupata nafasi jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Albert Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Serikali kwa sababu kulikuwa na changamoto kubwa sana kwenye hii barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, barabara kutoka Kyimo – Ikuti – Ibungu - Ileje lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya Idweli – Ngumburu – Lugombo ni lini itaanza kujengwa kwa sababu tayari imeshakabidhiwa *TANROADS*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kimo – Ikuti – Luswisi – Katengele – Kalembo hadi Ibungu ni barabara ambayo ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na tulielekezwa iwe imefanyiwa usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea barabara hii inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Rungwe na Wilaya ya Ileje. Upande wa Mkoa wa Mbeya, kwa maana ya Kimo hadi Kafwafwa usanifu uko hatua za mwisho na upande wa Ileje, kwa maana ya Kafwafwa – Katengele – Kalembo – Ibungu, usanifu umeshaanza, kwa ajili ya maandalizi kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara iliyotajwa ambayo sisi tunaitambua kwamba, inaanza pale Nambawano – Ngumburu – Lugombo ni barabara ambayo imepandishwa hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*. Mkandarasi yupo ameshapatikana. Changamoto kubwa ni eneo ambalo mvua kubwa sana inanyesha. Kwa hiyo, anachofanya Mkandarasi sasa hivi ni pale anapopata nafasi kuhakikisha kwamba, hii barabara inapitika, lakini ni kutengeneza barabara yote na kuiweka katika *standard* ya *TANROADS,* hasa pale ambapo hali ya hewa itakuwa imekaa sawa. Imeanzwa kutekelezwa mwaka huu wa fedha kwa maana ya *TANROADS*. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ninyi ndio hamkuuliza maswali jana?

Haya tuanze na Mheshimiwa Gwajima. Sasa kwa sababu, Mheshimiwa Gwajima wapo wawili humu ndani, Mheshimiwa

Askofu Josephat Gwajima. Maswali yawe mafupi, ili wote mpate nafasi; Mheshimiwa Mbunge, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Ni lini, Serikali itapanua Barabara inayotoka Kiwanda cha *Wazo Hill* kuteremka kwa Ndevu inayosababisha ajali nyingi kwa sababu, imekuwa nyembamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, swali hili nadhani siyo la kwanza kwa Mheshimiwa Askofu kuuliza. Tulichokifanya ni kuwaelekeza wenzetu wa *TANROADS,* Mkoa wa Dar es Salaam, ili waweze kuleta taarifa iweze kusanifiwa na kupanuliwa, kwa maana ya kutoka kuwa nyembamba na kuwa pana. Barabara hii ilijengwa muda mrefu na wakati huo watu walikuwa ni wachache, sasa magari yameongezeka hivyo, iweze kukidhi mahitaji ya sasa na kupunguza ajali ambazo zinatokana na wembamba wa barabara ile. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikabwe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Mogabiri – Nyamongo ni mbovu sana. Mitambo imetoka *site* na hata *service road*…

**SPIKA:** Swali. Swali, swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kupunguza adha kwa watu wangu wa Tarime Vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ina Mkandarasi yuko *site.* Ninaomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkandarasi pamoja na Meneja wa Mkoa wa Mara kuwa,

hawatakiwi kutoka *site*. Aweze kuhakikisha kwamba, anatengeneza zile barabara za *diversion,* ili barabara iendelee kupitika.

Mheshimiwa Spika, tunachoongea sasa hivi ni tunaandaa fedha kwa ajili ya kumlipa huyo Mkandarasi kwa *certificate* ambazo amesha-*raise* kuja kwetu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, nini hatima ya ujenzi wa Barabara ya Ibanda – *Itungi Port* na Iponjola – *Kiwira Port*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara zote hizo mbili zilipata mkandarasi, lakini alisitishiwa mkataba. Tunavyoongea sasahivi, barabara hiyo iko kwenye hatua za mwisho za manunuzi, kwa maana ya kumsainisha mkandarasi mpya, baada ya taratibu za kutangaza upya na kumpata mkandarasi mpya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali. Ni lini Serikali itakarabati Babaraba inayotoka Ngongo – Ngapa – Rutamba – Milola – Mandawa – Ruangwa kwa sababu, barabara hii imeathiriwa na mvua kubwa ambazo zimenyesha mwaka jana? Ahsante sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara zote ambazo ziliathiriwa na mvua mwaka jana zimetafutiwa fedha, ili kuanza kutengenezwa. Nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Lindi kuhakikisha kwamba, maeneo yote ambayo ni kikwazo ahakikishe anampeleka mkandarasi ambaye

amepangwa kufanya kazi, ili aweze kutengeneza yale maeneo ambayo ni korofi na magari yaweze kupita. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, nini mpango wa Serikali wa kuanza ujenzi wa Barabara ya Haydom – Mogitu ambayo usanifu na upembuzi yakinifu umeshakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja usanifu umeshafanyika na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Wanaliwale wanataka kusikia Barabara ya Nangurukuru – Liwale ni lini ujenzi wa kiwango cha lami utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza hii ni kati ya barabara ambazo ziliathirika sana kwenye kipindi cha mvua cha mwaka jana na madaraja mengi sasa hivi wakandarasi wako *site.* Kwenye maeneo ambayo tulitangaza kujenga tuko kwenye hatua za manunuzi ili kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni lini barabara ya kilometa 10 kutoka *Airport* kwenda Nyanguge itaanza kujengwa, baada ya mkandarasi kukabidhiwa *site* toka Mwezi wa Sita mwaka jana, mpaka leo hajaingia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ambayo tunaanza kuijenga kwa kilometa 10 tunachotafuta sasa hivi ni fedha ya kumlipa *advance* huyo mkandarasi ili aanze kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ni lini utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa kutoka Kolandoto kwenda Kishapu, kilometa 20 ambazo zimetengwa katika mwaka huu wa fedha utaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii ambayo tunaitekeleza, tulipanga kuanza kuijenga barabara hiyo mwaka huu. Tunachosubiri sasa ni kibali cha kuitangaza, ili iweze kuanza kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom na Lalago itajengwa kwa kiwango cha lami, pamoja na kuwa mkandarasi amesaini miaka miwili iliyopita? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni moja ya barabara ambazo zimetengenezewa utaratibu maalum ambao utatumika kuzijenga. Ni kati ya zile barabara saba ambazo tulikuwa tunazieleza na sasa imeundwa kamati ya kutafuta utaratibu wa namna ya kuzijenga kwa hatua, ikiwemo barabara hiyo ambayo amesema Mheshimiwa Awack. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Barabara ya Mbuguni, kuanzia Tengeru, hadi Mererani itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami baada ya usanifu na upembuzi yakinifu kumalizika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo baada ya kukamilisha usanifu, kipindi hiki cha bajeti, naamini itapangiwa bajeti ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza kuhusu ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Mlimba – Njombe. Ni lini Serikali itawalipa Wakandarasi wote wawili waliopewa kazi ya kujenga kilometa 100 kutoka Ifakara kwenda Chita, ili waanze kazi, yapata mwaka mmoja sasa tangu wasaini mikataba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ina *lot* mbili na hivi ninavyoongea *lot* ya kwanza mkandarasi ameshalipwa *advance,* kwa maana ya malipo ya awali. Kipande cha pili tunatafuta fedha, muda si mrefu tutamlipa, ili kazi ianze kwa *lot* zote mbili, kwa maana ya vipande vyote viwili, lakini kipande cha kwanza ameshalipwa *advance*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Bukombe Hadi Katoro kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ROSE V. BUSIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Bukombe hadi Katoro kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Bukombe – Katoro yenye urefu wa kilometa 58.20 kwa kiwango cha lami, unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Bukombe (Ushirombo) hadi Bwenda (kilometa 5.3). Zabuni za kumpata mkandarasi zimefunguliwa tarehe 20 Januari, 2025 na kazi ya tathmini ya zabuni hizo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya pili ya kutoka Kashelo hadi Nyikonga (kilometa 10.4) pamoja na Daraja la Nyikonga iko katika hatua ya majadiliano. Mkataba wa kazi unatarajiwa kuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Februari, 2025. Kwa sehemu zilizobaki za Bwenda – Kashelo (kilometa 16.3) na Nyikonga – Katoro (kilometa 26.2), Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninataka kujua ni lini itajenga Barabara ya Geita – Nyarugusu mpaka Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Geita – Nyarugusu hadi Kahama imegawanywa katika vipande viwili. Kipande cha Kahama hadi Ilogi tayari mkandarasi yuko *site* anaijenga kwa kiwango cha lami. Kutoka Ilogi – Nyarugusu hadi Geita tupo katika hatua za mwisho wa manunuzi, ili kuweza kusaini mkataba kwa kilometa zote 61.2, ili kuunganisha Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Itoni – Lusitu kwa kiwango cha zege utaanza baada ya kusimama kwa muda wa mwaka mmoja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mwanyika ni ambayo mkandarasi alishapatikana, yuko *site* na muda si mrefu tutamlipa fedha za awali, ili aweze kuendelea na kazi. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, katika barabara zile 27 za kipaumbele fedha ni nyingi sana; tumeshalipa barabara 17, tatu zimelipwa nusu na chache hizi ambazo hazijalipwa malipo ya awali fedha inatafutwa iweze kulipwa haraka, ili wakandarasi waendelee na kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbulu – Garbabi, kilometa 25. ujenzi wake umesimama. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kweli ilikuwa imesimama, lakini tunavyoongea sasa hivi mkandarasi yuko *site* na ameshapata fedha za awali. Kwa hiyo, tunaamini kazi zitaanza haraka iwezekanavyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Uvinza mpaka Kasulu kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Genzabuke. Kipande cha barabara hiyo kilichobaki kinatoka Mpanda hadi Kasulu. Tunategemea itakuwa ni sehemu ya barabara ambayo tutaijenga kwa kiwango cha lami kwa fedha ambayo ilibaki kwenye barabara zilizojengwa katika Mkoa wa Katavi. Kwa hiyo, ipo kwenye mpango iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ili tuunganishe Katavi na Kigoma, kwa maana ya Uvinza hadi Kasulu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni lini Barabara ya Mingoi – Kiembeni ambayo imerudishwa chini ya umiliki wa *TANROADS* itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, kwanza ni lazima ijengwe katika *standard* za *TANROADS,* halafu iweze kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kadri fedha itakavyopatikana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Masanja, swali la nyongeza.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya kutoka Nhungumalwa - Ngudu hadi Magu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja, ambayo tutaanza kujenga kilometa 10, tayari ilishatangazwa na sasa hivi tuko kwenye hatua za manunuzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Mkandarasi wa Barabara ya Nansio – Rugezi atarudi *site* na kukamilisha ujenzi wa barabara ile? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni Mkandarasi mzawa ambaye anajenga hiyo barabara na tayari tumeshapokea maombi yake ya *advance* pamoja na kazi ambayo ameifanya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi tunaandaa malipo yake, ili aweze kuendelea na kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyouliza Mheshimiwa Mbunge, ndio zile barabara saba ambazo nimesema utaratibu mpya umeandaliwa na hizo barabara tutazielezea namna zitakavyotekelezwa tofauti na ule mpango uliokuwepo awali. Kamati imeundwa rasmi, maalum, kwa ajili ya kuzipitia barabara hizo na kutafuta namna sahihi ya kuzijenga kwa utaratibu ambao tumeuzoea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa Barabara ya Katumba – Suma – Ruangwa, ni lini atapeleka mitambo *site* ikizingatiwa kwamba, ameshalipwa *advance*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkandarasi huyo amelipwa *advance* kama wiki moja au mbili zilizopita, anachofanya sasa hivi ni kukusanya wafanyakazi na kuainisha maeneo ambayo atajenga kambi zake; atajenga kambi mbili kwa maana ziko barabara mbili na mkandarasi ni mmoja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunaamini utakapofika mwezi Februari katikati kazi zote zitakuwa zimeanza, lakini tumemhimiza kabla mitambo haijafika aanze kufanya zile kazi, kwa maana ya magari yaanze kupita mle ambamo yanakwama kwa sababu, hatukupanga fedha za *maintenance,* yeye ndio anatakiwa afanye hiyo kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake...

Na. 31

**Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami, Korogwe**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Maramba hadi Mabokweni utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya *Old Korogwe* – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Maramba hadi Mabokweni (kilometa 127.69) iko katika hatua za mwisho, ambapo kwa sasa Mhandisi Mshauri anafanya kazi ya kuigawa katika sehemu nne, kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji. Kazi hii inatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Mwezi Machi, 2025. Baada ya kukamilika kwa

usanifu, Serikali itaanza ujenzi kwa kadri ya fedha zinavyopatikana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Alfred Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina ombi. Barabara hii ni ndefu, ili kuleta matumaini hasa kwa wananchi, ninaomba ujenzi wake uanze pande zote mbili; upande wa kwa Mufti Mkuu wa Tanzania huku Kwamndolwa na upande wa Mabokweni kote kuende kwa wakati mmoja. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umepokea ushauri huo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea ushauri. Ndiyo maana ile barabara tumeigawa katika vipande vinne kurahisisha utekelezaji, ikiwa ni pamoja na ombi la Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali angalau itajenga kwa awamu barabara kutoka Njiapanda mpaka Mang'ola hadi Matala kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hii barabara aliyoitaja tunaitambua ni barabara muhimu sana, mpango wetu pia ni kuijenga kwa awamu na hasa kuanzia Karatu hadi Mang'ola ndiyo eneo ambalo tunategemea tuanze kulijenga kwa kiwango cha lami ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 32

**Kero za Wafungwa na Mahabusu**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, kwa nini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haiibui kero za wafungwa na kuzitafutia ufumbuzi hadi ziibuliwe na Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2020 – 2025, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imetembelea Magereza 52, Vituo vya Polisi 59, Mahabusu za Watoto (3) na Vyuo vya Mafunzo (11). Wakati wa kutembelea maeneo hayo, Tume ilipokea kero mbalimbali za wafungwa, wanafunzi na mahabusu. Kero hizo pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Tume kuhusu hatua za kuchukua yaliwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kupitia mapendekezo ya Tume, yamefanyika maboresho katika Mhimili wa Mahakama na Taasisi za Haki Jinai ambayo yamepunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa nakala za hukumu na kuongezeka kwa kasi ya usikilizwaji wa kesi na rufaa za watu walio vizuizini, kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambayo yamesaidia kupunguza msongamano wa mahabusu gerezani na kuondolewa kwa mitondoo magerezani. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; bado mpaka sasa katika selo za polisi, lakini na katika mahabusu

zetu za magereza bado zina mifumo ile ile ya kikoloni na zimekuwa zinatumia mfumo ule wa kizamani. Sasa Serikali inasimama wapi hapo katika suala la haki za binadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Waziri mpaka sasa mna mpango gani katika kuboresha mitondoo (vyoo) maana yake wengine wanatumia mitondoo lakini wengine inawezekana wasijue mitondoo ni nini? Ni vyoo ambavyo mfumo ule wa kizamani wa kikoloni ambao watuhumiwa wa mahabusu na magereza walikuwa wanatumia kufanya haja zao zote katika chumba kile kile ambacho wanalala. Je, mpaka sasa mna mpango gani sasa tufanye selo za kisasa na mahabusu ziwe za kisasa ziendane na wakati na muda huu ambao tuko nao kwa sasa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwenye mahabusu zetu hasa zile za kizamani ambazo hazijafanyiwa maboresho ipo mifumo ambayo haikidhi viwango vya ubora kama alivyofafanua, ndiyo maana nimesema katika utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita hususan baada ya Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya Hakijinai udhaifu wote wa aina hiyo alioubainisha umeonekana na uboreshaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mahabusu zetu zinazojengwa ama ziwe za Polisi au Magereza yenyewe mifumo aliyoisema kama hiyo mitondoo huwezi kuikuta tena na Serikali katika taasisi zake zote zinazosimamia Hakijinai ikiwa ni pamoja na Mahakama, Polisi, Magereza na maeneo mengine yanaboresha mifumo hii kadri ujenzi unavyoendelea nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Tarafa nzima ya Makambako ambayo ina Kata tano kwa maana ya Kata ya Ninga – Igongoro – Ikuu – Nakichiwa na

Mtwango hawana Mahakama ya Mwanzo. Je, ni lini Serikali watajenga Mahakama ya Mwanzo pale Mtwango? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali la msingi lilikuwa halihusu Mahakama. Unaweza kulileta kama swali la msingi labda kama Waziri unayo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri lipo swali la ujenzi wa Mahakama ninaweza nikalijibu wakati huo.

**SPIKA:** Unaweza? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, *okay*. Ni kweli Mhimili wa Mahakama unao mpango wa ujenzi wa Mahakama katika ngazi mbalimbali Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Jumuishi Ngazi ya Mkoa ambazo zitachukua ngazi zote kuanzia Mahakama za Mwanzo za Wilaya, Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kulingana na mpango huu wa miaka mitano Wilaya mbalimbali zimeguswa na Mahakama za Mwanzo karibu 72 zimejengwa. Tutaangalia kwenye awamu ijayo ya kuanzia 2026/2027 uwezekano wa Makambako na ukuaji wake wa Mji ule wanahitaji kuwa na Mahakama na hivyo itazingatiwa ipasavyo. Ninashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 33

**Sheria ya Kuhasi Wabakaji**

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, lini Serikali italeta sheria ya kuwahasi wabakaji wanaofanya uzalilishaji wa kijinsia kwa watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 131(1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, imeainisha adhabu ya makosa ya kubaka kuwa ni kifungo kisichopungua miaka 30, viboko na Mahakama inaweza kutoa amri ya kumlipa fidia muathirika wa tukio hilo. Aidha, Kifungu 131(3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kimeainisha kuwa ikiwa muathirika wa tukio hilo ni mtoto mwenye umri chini ya miaka 10 adhabu pekee ni kifungo cha maisha jela.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalichukuwa swali la Mheshimiwa Mbunge, kama sehemu ya maeneo ya kufanyiwa kazi na kuona kama ipo haja ya kuongeza adhabu kwa wanaobaka watoto chini ya miaka 10 au tuendelee na adhabu iliyopo ya kifungo cha maisha jela. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani kwa wazazi, walezi wanaomaliza kesi hizi mitaani badala ya kupeleka kwenye vyombo vya sheria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, makosa yote ya jinai kwa kweli yakiwemo hayo makosa mabaya, udhalilishaji na ubakaji yanapaswa yaripotiwe kwenye vyombo vya dola na hivyo kufikishwa Mahakamani. Sasa kama wapo wazazi wanaoyamaliza mashauri kama hayo mtaani, ninaomba kupitia jukwaa lako hili tuwasihi wazazi na wananchi kwa ujumla tusifumbie macho makosa makubwa kama haya ya ubakaji na udhalilishaji, inapotokea turipoti Polisi ili wafikishwe Mahakamani na hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria zilizopo. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Ujenzi wa Majengo Mapya ya Mahakama Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga majengo mapya ya Mahakama za Mwanzo Nanyamba kwani yaliyopo ni ya zamani na yamechakaa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama, majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama na kadri ya fedha zinavyopatikana. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea vizuri kuna mpango wa miaka mitano wa ujenzi na ukarabati. Je, ni lini sasa Mahakama ya Mwanzo Nanyamba itakarabatiwa kwa sababu kwenye miaka mitano pale ninaomba nieleze kwamba ni mwaka gani Nanyamba itakarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari sasa kufanya ziara Nanyamba ili ukaangalie hali halisi ya majengo yanayotumiwa na Mahakama ya Mwanzo ya Nanyamba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nimejibu maswali kwa ujumla, lakini kwa maana ya Nanyamba mpango huu wa awali wa miaka mitano haikuwemo, lakini kwa mujibu wa taarifa za Mahakama, Nanyamba itaingia kwenye mpango wa mwaka 2026/2027 kwa ajili ya kujengwa upya kwa sababu kwa kweli Mahakama hiyo ni chakavu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utayari wangu kwenda Nanyamba ili kushuhudia hali ilivyo sina shaka nipo tayari baada hata ya Bunge hili kadri ratiba itakavyoruhusu nitatembelea Nanyamba kushuhudia jambo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, jengo la Mahakama ya Mwanzo katika Wilaya ya Urambo lina hali mbaya sana na mpaka sasa lina *asbestosis.* Je, ni lini Serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, mpango wa awali wa miaka mitano haukuweza ku-*cover* mahakama zote, tumeweza kujenga Mahakama za Mwanzo 72 pekee na kukarabati nyingine chache. Sasa, ninamwahidi kadri Mahakama ilivyojipanga katika awamu ya pili eneo la Urambo ambalo wote tumethibitisha Mahakama ile imechakaa sana itakuwa sehemu ya ukarabati wa Mahakama hiyo, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 35

**Uwepo wa Viwanja vya Michezo kwa Wenye Ulemavu**

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Viwanja vya Michezo kwa Watu wenye Ulemavu vinaendelea kuwepo na vinaimarishwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha viwanja vinavyojengwa na vinavyokarabatiwa kwa sasa vinazingatia miundombinu ya watu wenye mahitaji maalum na kuweza kutumika na makundi yote ikiwemo watu wenye ulemavu. Uzingativu huu tunautoa pia kwa wadau na taasisi zote zinazomiliki na kuendesha miundombinu ya michezo kuhakikisha wanaweka maeneo maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu kuweza kushiriki wakati wa matukio ya kimichezo kama ambavyo tumeweka katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam na uwanja tunaoujenga Jijini Arusha, Samia Suluhu *Stadium*.

Mheshimiwa Spika, aidha, tumeendelea kutoa vifaa vya michezo kwa watu wenye mahitaji maalum hasa katika ngazi ya timu za Taifa ndani ya kundi hili maalum ili kuwawezesha kutumia viwanja vilivyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantatu Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ukiondoa Viwanja vya Benjamini Mkapa ni viwanja vipi vingine vya michezo

vyenye miundombinu inayowezesha watu wenye ulemavu kushiriki michezo ipasavyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha vifaa vya michezo vinawafikia vijana wanamichezo waliomo mashuleni wenye ulemavu ili waweze kufikia malengo ya kuinua vipaji vyao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata fursa mbalimbali zikiwemo fursa za michezo.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa uwanja wa Benjamini Mkapa kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, viwanja vyote ambavyo tunakwenda kuvijenga ama kuvikarabati sasa hivi vitakuwa na miundombinu itakayowawezesha watu wenye ulemavu kuvitumia. Hali kadhalika tumetoa rai kwa wadau wote ambao wanatengeneza miundombinu ya michezo kuhakikisha miundombinu yao inawawezesha watu wenye mahitaji maalum wakiwemo watu wenye ulemavu kuweza kuitumia kwa shughuli za michezo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, tunatumia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa sasa kuhakikisha kwamba tunagawa vifaa kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya michezo kwa watu wenye ulemavu, jambo hili limekua likifanyika kwa muda sasa pamoja na kusajili vyama vya michezo vya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, nimtie moyo Mheshimiwa Mbunge ya kwamba jambo hili tunalifahamu na tunalifanyia kazi na kwa kadri fedha zinavyopatikana tutahakikisha vifaa hivi vinaendelea kugawiwa mashuleni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ulinzi na

Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Kuongeza Pensheni Askari Wastaafu wa JWTZ**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio kubaini Askari wa JWTZ waliostaafu muda mrefu na kuwaongezea pensheni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa Pensheni kwa Askari waliostaafu. Aidha, Pensheni ni suala la kisheria ambapo malipo ya pensheni kwa Askari wa Jeshi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania hufanyika kwa kuzingatia Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Kanuni za Pensheni ambayo ni *"The National Defence Act (Services Pension and Gratuity) (Amendment) 2015*".

Mheshimiwa Spika, viwango vya pensheni hutofautiana kulingana na mishahara ya wakati wa kustaafu. Kwa kutambua changamoto ya viwango tofauti vya pensheni, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefanya tathmini ya kina na kuwasilisha mapendekezo kwa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mapendekezo yaliyowasilishwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majadiliano yanaendelea kati ya Wizara na Wizara ya Fedha na kikao cha mwisho tulichokifanya katika ngazi ya Mawaziri na Makatibu Wakuu kilifanyika tarehe 7 Januari mwaka huu, lakini hapo imesomeka 2024, samahani Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya tathmini na majadiliano kukamilika, mapendekezo yatawasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kwa kuzingatia taratibu zilizopo. Kwa hiyo, tunalitambua na tunalifanyia kazi Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa vile wastaafu hawa wa miaka 1970 na 1980 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanalipwa kiwango cha shilingi laki moja tu. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kiwango hiki hakikidhi haja hata ndogo ya kuwasaidia Wanajeshi hawa waliostaafu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; kwamba, wastaafu hawa kwa kweli ni wachache sana kwa sasa na afya zao sasa hivi zinazorota siku hadi siku. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuchukua dharura ya makusudi kwa kuwapatia Bima ya Afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Ali Omar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwango kidogo cha bima ambacho umetoa mfano kwamba sasa hivi ni kama laki moja, ni kweli tunafahamu kwamba kiwango ni kidogo na kama nilivyosema viwango vya pensheni hutofautiana hata hao ninaowasema wanatofautiana kulingana na amestaafu lini, tunakushukuru kwa kuendelea kuwapigania na Waheshimiwa wengi pia wameendelea kuwaombea na kwa kutambua hali hii ndiyo maana tunafanya tathmini na tumekwishafika mbali kama nilivyokwishasema, tumeshapeleka mapendekezo hata viwango tunavyovipendekeza, naweza kwenda ndani zaidi kwamba kuna *options* tatu ambazo zimepatikana ambazo zinafanyiwa

mchakato kuona ni *option* gani tunaiweza kulingana pia na uwezo bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la bima, ni kweli kwamba kwa sasa hivi upo utaratibu wa Bima ya Afya kwa Maaskari na Maafisa wa Jeshi ambao wakati unaanza wanapata bima. Lakini wale ambao walikuwa nje wakati utaratibu huu haujaanza hawapati bima. Kama nilivyokwishajibu huko nyuma wanapatiwa matibabu, lakini kwa kutambua kwamba hawawezi kupatiwa matibabu yote, hili nalo linaangaliwa katika mchakato unaoendelea. Tumetoa kipaumbele kwa Wanajeshi ambao walipigana Vita ya Kagera ili waanze, halafu na hao wengine tutaona namna gani tunawaingiza katika utaratibu wa bima, lakini tukitambua kwamba kuna mchakato wa Bima kwa Wote ambao pia unaendelea kufanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 37

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Namasakata – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Tarafa ya Namasakata – Tunduru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kujenga Kituo cha Polisi Daraja “C” kwenye Kata ya Namasakata Tarafa ya Namasakata Wilaya ya Tunduru. Halmashauri ya Wilaya imeshatoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 4,046 kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Polisi. Ujenzi wa kituo hicho unatarajia kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025, kupitia Mpango wa Ushirikiano na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na utagharimu kiasi cha fedha shilingi 115,000,000. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Tarafa ya Namasakata ina Kata tano, lakini haina Kituo cha Polisi hata kimoja. Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuharakisha ujenzi wa kituo hicho?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Tarafa ya Nalasi kuna Kituo cha Nalasi ambacho kimetengewa milioni 115 kujenga Kituo cha Polisi Daraja “C” katika huu Mwaka wa Fedha wa 2024/2025. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa ajili ya kujenga kituo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwenye mwaka wa fedha 2024/2025 tumetenga fedha shilingi milioni 115 kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi kwenye Kata ya Namasakata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli kwenye mwaka huu wa fedha, pia Kituo cha Polisi cha Nalasi pia kimetengewa fedha shilingi milioni 114. Kwa hiyo, nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka wa fedha bado unaendelea, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivi vya polisi vya Nalasi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein nimekuona na Mheshimiwa Ndulane pia nimekuona, lakini jana mliuliza maswali. Kwa hiyo, nipeni muda ili niwapatie nafasi watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Ujenzi wa Ofisi ya Polisi Mlimba**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi ya Polisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Polisi Daraja "B" katika Halmashauri ya Mlimba. Halmashauri imeshatoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 12,183 kwa ajili ya kujenga kituo pamoja na nyumba za makazi ya askari polisi. Kituo kitajengwa eneo la Itongoa ambayo ni Makao Makuu ya Halmashauri. Fedha kiasi cha shilingi 802,926,788 zinatarajiwa kutengwa toka kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali machache. Swali la kwanza; eneo la Mlimba ni eneo ambalo lipo mbali sana na halmashauri, lakini mwaka jana niliuliza pia hilo swali na mwaka juzi, kila siku wananijibu kwamba wana mpango.

Je, ni lini sasa huo mpango utakamilika maana inaonekana kwamba ipo kwenye bajeti, lakini mpango ni lini hasa wataanza kujenga hicho kituo badala ya kuendelea kuwa na mpango?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; katika eneo hili lililopo sasa ni finyu ambalo ni eneo la *TAZARA* ambalo limejaa makorokoro na vyuma, usalama wa pale ni mdogo sana hata wananchi wakienda pale hawana sehemu ya ku-*park* magari yao wakati wanahitaji msaada kwenye kituo hicho, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ni lini mpango unaanza. Nimesema kwenye jibu la msingi tunatarajia kutenga fedha kwenye Mwaka wa Fedha 2025/2026 ndipo ujenzi wa Kituo hicho utakapoanza.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili la nyongeza, amesema eneo limejaa vifaa vya *TAZARA,* lakini nimhakikishie tunapoanza ujenzi maana yake eneo hili litafanyiwa usafi na kuhakikisha kwamba linakuwa tayari kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri hii ya Mlimba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Kata ya Ilongelo ambayo ndio Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunajenga Vituo vya Afya vya Kata awamu kwa awamu,

kwa awamu ya kwanza na pili. Kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge pia tutaweka kwenye mpango kituo alichokitaja cha polisi, ili tukitengee fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi katika eneo hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza. Mheshimiwa nani upo pale au ni Dorothy Kilave? Mheshimiwa Janeth Mahawanga? Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo hayana vituo vya polisi ni hatua gani zinachukuliwa ili kuhakikisha askari wanafika kwa wakati hasa wakati wa dharura na je, Serikali haioni haja ya kuimarisha ulinzi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth unauliza swali moja tu kwa sababu ni la nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janeth Mahawanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo hayana vituo vya polisi, askari kwenye kituo cha jirani hutumika kwenda kutoa msaada au huduma ya kiaskari katika maeneo ambayo hayana kituo cha polisi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Ujenzi wa Chuo Cha *VETA* Wilaya ya Missenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga na kukamilisha Chuo Cha *VETA,* Wilayani Missenyi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi cha Wilaya ya Missenyi ni miongoni mwa vyuo 64 vinavyojengwa na Serikali katika wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya pamoja na Mkoa wa Songwe ambao ulikuwa hauna Chuo cha *VETA* Mkoa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Misenyi, Serikali imeshapeleka jumla ya shilingi 377,893,361.01 pamoja na vifaa vilivyonunuliwa kutoka viwandani ikiwemo nondo, *cement,* mbao pamoja na mabati kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki ambapo utekelezaji umefikia 35%. Ujenzi wa chuo hiki unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa majengo yaliyopangwa kujengwa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa chuo hiki unatarajia kukamilika mwezi Mei, 2025. Aidha, Serikali itaendelea kupeleka fedha pamoja na vifaa vingine vya ujenzi vitakavyonunuliwa kutoka viwandani ili ujenzi wa chuo hiki uweze kukamilika na kuanza kutoa mafunzo kama ilivyopangwa. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ya kujenga chuo ndani ya

Wilaya ya Missenyi, pia niiopongeze Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa usimamizi ujenzi wa vyuo hivyo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika eneo la ujenzi ukienda kwa kweli sasa hivi mkandarasi takribani miezi mitatu au minne hayupo *site*. Sasa tungeomba kupata *commitment* ya Serikali kutuhakikishia kwamba huo muda ambao Mheshimiwa Waziri amesema wa mwezi Mei kwamba chuo hicho kitakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ukienda pale kuna majengo takribani sita, lakini mawili tu ndio yamewekewa kenchi za kuezeka na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mabati na vifaa vingine vimenunuliwa. Je, tutapata uhakika gani kama hivyo vifaa vinaenda kutumika ili mwezi Mei ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ametuhalikishia, chuo hicho kiwe kimekamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Missenyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye maswali ya jibu la msingi, kwanza, vyuo hivi vyote 64 pamoja na kile kimoja cha Mkoa tunajenga kwa utaratibu wakutumia *force account*. Katika mfumo huu Serikali inanunua vifaa na baadaye wakandarasi au wale mafundi tunaita *local fundi* ndio wanaotumika kwa ajili ya ujenzi kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote 64 ambao maeneo yao yanajengwa, tulipata changamoto kidogo ya vifaa vya viwandani kwa maana ya mabati na hivi sasa tayari vifaa vyote ikiwemo mabati yameshanunuliwa yapo njiani yanaelekea.

Mheshimiwa Spika, mwezi Disemba tulikuwa tumepeleka fedha karibu shilingi milioni 100 katika kila *site* ili kuhakikisha kwamba zile *local materials* pamoja na malipo ya mafundi

yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge huo mwezi Mei tuliotaja kama *target* yetu tunaweza kuufikia kwa sababu vifaa vyote tayari tumeshanunua na vipo njiani vinaenda *site* kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, je, lini Chuo cha *VETA* Mpwapwa kitakamilika ili kusudi wanafunzi waweze kudahiliwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi, Mpwapwa nayo ni miongoni mwa vile vyuo 64 na utaratibu wake ni ule ule kwamba vifaa vya umaliziaji tayari vipo njiani kwa maana ya kupaua, kuezeka pamoja na *finishing*. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba itakapofika mwezi Mei Chuo cha Mpwapwa nacho kitakuwa kimekamilika ili kiweze kutoa mafunzo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi. Mkoa wa Njombe una shule moja ya msingi ya elimu maalum ambayo watoto wakimaliza darasa la saba hawana uwezo wa kuendelea na sekondari. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu palepale na kuongeza uwezo wa shule ile kuanzisha masomo ya sekondari? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu swali dogo la Mheshimiwa Kamonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge na yeye anatoa kama ushauri kwa Serikali kwamba tunaonaje kuhusiana na suala la kuongeza miundombinu.

Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza tuna wajibu wa kufika katika hilo eneo na kuweza kuona miundombinu gani ipo na ipi inapungua. Kwa vile ni ushauri tunaomba baada ya Bunge hili tuweze kuonana tuweze kuangalia namna bora ya kufanya katika eneo hili alilolitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Wananchi Kurejeshewa Mashamba Yao**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, lini mashamba ya wananchi zaidi ya 1,000 wa Vijiji vya Kata ya Mrijo na Jangalo yatarejeshwa kwa wananchi ili kazi za kilimo ziendelee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi 1,000 wa Kata ya Mrijo na Jangalo yalishafanyiwa kazi na Serikali kupitia Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Chemba na Kiteto mwaka 2015/2016 na 2023 ambapo eneo wanalodai wananchi kuwa ni ardhi yao kwa ajili ya kilimo lilibainishwa kuwa lipo Wilaya ya Kiteto, Mkoa wa Manyara ambapo mwaka 2009 lilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali (*GN* Na. 385/2009) kuwa ni Hifadhi ya Makame *(Wildlife Management Area - WMA)*. Hivyo wananchi wa kata husika wanashauriwa kuendesha shughuli zao katika maeneo yaliyo ndani ya mpaka wa Wilaya ya Chemba na Mkoa wa Dodoma na

iwapo wanauhitaji wa ardhi nyingine nje ya mipaka ya Wilaya na Mkoa wao, wafuate taratibu za kuomba na kupatiwa ardhi na Mamlaka husika za Vijiji, Wilaya na Mkoa wanaotarajia kuomba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nina uhakika kabisa Mheshimiwa Waziri ni mwanasheria na anafahamu wananchi wa Tanzania yote wanaruhusiwa kufanya shughuli zozote nje ya mipaka ya kiutawala, maana yake wananchi wa Chemba wanaweza kufanya kilimo kwenye Wilaya ya Kiteto. Sasa ninataka niulize ni kwa nini amesisitiza kwenye majibu kwamba tuendelee kulima kwenye mashamba ya Chemba wakati mashamba yetu yapo Kiteto na yeye anajua ni mashamba yetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ninaomba unipatie fursa nielezee kwa ufupi tu. Mwaka 2003 walifanya *review* ya mipaka kati ya Kiteto na Chemba, mashamba ya Chemba tukabaki na vijiji, mashamba yakabaki Kiteto. Sasa baada ya kuona wanakijiji wamebaki Chemba yale mashamba wakayakabidhi kwa Hifadhi ya Makame bila kulipa fidia yoyote. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kama ataweza tuongozane naye, ili aone hali halisi ya wananchi ambao wamebaki Chemba hawana mashamba wakati hali halisi mashamba yao yamebaki Kiteto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza linauliza kuhusu uhalali wao wa kumiliki maeneo yale ambayo walikuwa wanayatumia mwanzo kabla ya mgawanyo mpya wa wilaya na katika mazingira ya kawaida anataka kujua ni kwa nini wasiendelee kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa ni uainisho wa ile mipaka na katika mazingira ya kawaida, mimi mwenyewe nimezungumza naye na siku ya Jumamosi wananchi walikuja ofisi, Jumapili tumekubaliana niende huko Kiteto ili nikasikilize huko uwandani tatizo lipoje.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo jibu la msingi lilivyo, mwaka 2015/2016, Kamati za pande mbili zilikaa na kukubaliana kwamba sasa wananchi wa Kiteto wajue eneo lao la Kiteto na wananchi wa Chemba wajue eneo lao la Chemba, hatuna tatizo na matumizi ya mtu kwenda kulima upande wa pili. Maeneo yote mawili yana Wabunge na niliwahi kuomba nafasi niwakutanishe waweze kuzungumza na mimi, lakini hawakuwa wamekaa sawa. Kwa hiyo, bado ninaendelea na juhudi za kuwaweka pamoja ili tuone, lakini uhalali uliopo ni kwamba ardhi ya Chemba ipo Chemba na ardhi ya Kiteto ipo Kiteto. Ni suala la watawala wawili wale labda kama watakuwa wamekubaliana waweze kukaa sawa, lakini Mbunge wa Chemba hawezi kuilazimisha Serikali itoe kauli ya kusema wananchi wale waende kule na ndio maana tumeamua sisi kama Wizara kwenda kukutana na wao tuangalie uhalisia ili tuweze kuyaweka vizuri masuala haya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ninaona Mbunge wa Kiteto amesimama, lakini ngoja nielewe kwanza hoja ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Wakati mipaka ikiwekwa maana yake ni kwamba wananchi wa Chemba wamepoteza eneo lao kwa wananchi wa Kiteto? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, lakini wakati wanagawanyika ilikuwa ni wajibu wa Mkuu wa Mkoa na Wilaya hizi za Chemba kukutana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara. Kitu ambacho kilifanyika mwaka 2015/2026 na 2023 wakaridhiana juu ya uendeshaji wa maisha ya wale wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa linapokuja, kama Wizara haiwezi kutoa maagizo ambayo yanaenda kuvunja maamuzi yale ya kimipaka na ndio maana mwisho pale nimesema hapa iwapo kuna uhitaji wa ardhi nyingine nje ya mipaka ya Wilaya na Mkoa

wao, wafuate taratibu za kuomba na kupatiwa ardhi na mamlaka za upande wa pili wanapodhamiria kwenda kupatumia ili kuondoa ile sintofahamu ya mamlaka kwa sababu…*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninyi Wabunge hapa mna mashamba Mbarali hamtoki Mbeya, mna mashamba huko. Kuna shida gani ya Mwanachemba kuwa na shamba Kiteto? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hatuna tatizo lolote, lakini kila mwananchi ambaye analima popote hakwenda kwa nguvu kuchukua lile eneo wameenda kwa makubaliano na makubaliano yale hayaleti athari ya pande yoyote katika shughuli za kiutawala.

**SPIKA:** Ngoja, Mheshimiwa jibu lako linasema hivyo wananchi wa kata husika wanashauriwa kuendesha shughuli zao katika maeneo yaliyopo ndani ya mpaka wa Wilaya ya Chemba na Mkoa wa Dodoma. Maana yake ni kwamba yale yapo nje ya mipaka yao kwa hiyo hawawezi kwenda kule? Ndio Hoja ya Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, suala lao ni tofauti na mkulima mmoja mmoja anayekwenda kutumia eneo la pili kwenye kulima kama ambavyo wewe una shamba Dodoma, kufika kwako kwenye eneo la shamba la Dodoma hakukuwa kunakwenda kwenye mfumo wa kisheria kwa maana ya kuhalalishwa kwa namna yoyote ile wewe kulima pale. Umekubaliana na ukanunua, labda kama ulinunua au ulipewa na mamlaka zinazohusika kwa makubaliano na ndiyo maana hapa mwisho nimeliweka vizuri kwamba mamlaka hizi mbili, kwa mfano hapa tuna Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hajawahi na hatuna taarifa zozote za kiofisi zinazoonesha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ameomba ardhi Mkoa wa Manyara kwa utaratibu wa wale waliohamishwa kuja huku. Kwa hiyo, inavyoonekana menejimenti ya Mkoa inaweza ika…

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Mbunge, subiri kidogo. Mimi ninataka kuelewa kwa sababu mipaka imekuja baadaye kama ulivyoeleza mwaka 2013 au 2003?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mwaka 2013.

**SPIKA:** Mwaka 2013, maana yake hawa hilo eneo kabla halijaenda Manyara lilikuwa la Chemba. Wanachemba walikuwa wanalima hapo. Sasa kama mimi ni mmiliki, lakini mpaka umepita na ninaendelea na shamba langu umiliki wangu, yaani kuhama mpaka kunaniondolea uhalali wa umiliki? Nitakupatia nafasi Mheshimiwa Mbunge, subiri nielewe hoja kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani? Kwa mfano, tunapokupa ardhi wewe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Dodoma, mipango ya matumizi bora ya ardhi ya eneo lako yanasimamiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Dodoma. Upo uwezekano…

**SPIKA:** Mimi mmiliki ninakuwa na haki gani wakati Serikali inapochukua ile ardhi kumkabidhi mwingine ambayo ni ya kwangu mimi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kawaida, ndiyo maana nimeona niende Kiteto nikakutane na makundi haya mawili ...

**SPIKA:** Aah uende! Aah, sawa, basi imeeleweka.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, tuliangalie katika muktadha wa kisheria, tuangalie katika muktadha wa umiliki wa maeneo haya katika muundo wa makubaliano ya pande zote mbili za Serikali za Mikoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Maadamu unakwenda, sawa. *(Makofi)*

Hebu tumsikilize Mbunge wa Kiteto alikuwa amesimama.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba nichangie badala ya kuuliza swali, kwa sababu imeleta mjadala.

**SPIKA:** Ngoja, sasa Mheshimiwa haitakuwa sawa. Anayeruhusiwa kuchangia ni mimi, nilikuwa naongea hapa. Kama unataka, usimame uulize swali. Ndiyo maana yule wa Taarifa naye nimemkatalia, kwa sababu ni kipindi cha Maswali na Majibu.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, basi ninaomba niulize swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa ardhi wanayodai wananchi hawa wa Chemba ipo Kiteto, na Kijiji ambacho hii ardhi inasemekana ipo kipo Kiteto na haijawahi kuondoka, ni nini kauli ya Serikai leo ili wananchi wa Chemba na Mbunge wao wafahamu, kama wanataka kupata ardhi waje waombe Kiteto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, keti tu. Hilo swali lako maadamu Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba Serikali itakuja huko Kiteto, itaenda Chemba, maswali hayo mtaulizana kule, lakini uhalisia ni kwamba, kwa Katiba ya nchi yetu na sheria za nchi yetu, hakuna mtu anatakiwa ardhi yake ichukuliwe bila yeye kulipwa, halafu ikabidhiwe tu Serikalini, halafu yeye awe anashangaa.

Kwa hiyo, watakapokuja kule, haya uliyoyauliza mtajibizana vizuri kule, lakini kwa maana ya muktadha wa swali lililopo hapa mbele, yeye hawezi kutoa hilo tamko.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ahaa! Au niulize lingine kwa njia nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Keti Mheshimiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, maadamu unao huo utayari wa kwenda huko Chemba na upande wa Kiteto, ni dhahiri mtaweza kulimaliza hili suala. Mheshimiwa Mbunge, kwa ahadi hii ya Serikali, nadhani utakuwa sehemu ya wananchi kujua kwamba ni jambo gani linaweza kurekebishwa hapo ili mambo yakae sawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawatakia kila la heri katika jambo hilo. Kama Bunge litahitajika kuingia mahali, basi baada ya huo mchakato utakapokamilika, basi litarejeshwa kwetu ili tuweze kulifanyia kazi kwa ngazi yetu. Ila kwa sasa tuiache Serikali ikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha Maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa, ninaleta matangazo niliyonayo hapa mbele, kisha tuendelee na ratiba yetu.

Tutaanza na tangazo la Wageni; tutaanza na wageni wangu. Sasa, kuna wengine wamekaa Jukwaa la Spika, wengine wamekaa majukwaa mengine ya wageni.

Tunao wageni watatu kutoka Kampuni ya Sigara Tanzania *(TCC);* Ndugu Roy Manalili, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, karibu sana; yupo Ndugu Patricia Mhondo, ambaye ni Mkurugenzi wa Mahusiano na Mawasiliano, karibu sana; yupo Ndugu Jacob Luoga, ambaye ni Meneja Mahusiano na Udhibiti, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia ninao wageni 40 kutoka Chuo cha Teofilo Kisanji, kilichopo Mkoa wa Mbeya, ambao ni Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi, karibuni sana, karibuni sana! *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hawa ni Ndugu Saganda Matondo, ambaye ni Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, karibu sana. Bwana Saganda, hebu simama tena. Jamani, nimesoma naye. Ahsante sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Hamza Ismail Shabani ambaye ni Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, karibu sana; pia, yupo Novaita Mrosso, Kamishna wa Huduma za Sheria, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Juliette Sagamiko, Naibu Kamishna wa Uhamiaji, Ufuatiliaji na Tathmini, karibu sana; pia, yupo Joseph Mtenga, Naibu Kamishna Mipango, karibu sana; yupo Andrew Malyeta, Mrakibu Mwandamizi wa Utawala, karibu sana. *(Makofi)*

Hawa wameambatana na Watendaji na Maafisa wengine kutoka Wizara na Idara ya Uhamiaji. Wanaweza kusimama wote kwa Pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye Jukwaa la Spika, pia kuna wageni saba wa Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, ambao ni Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kyela, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wa Wilaya, Ndugu Elias Ulisaja Mwanjala. Karibuni sana. *(Makofi)*

Ninaona wengine hawajasimama. Simameni wote kwa pamoja, mnaongozwa na Mwenyekiti. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; yupo mgeni wa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, ambaye ni mtoto

wake kutoka Jijini Dar es Salaam, anaitwa Arafat, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ambaye ni Askofu Dkt. Christopher Madulu kutoka Wilaya ya Hai, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Mwinjilisti Nicolas Fungameza kutoka Kanisa la *EAGT* Jijini Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo viongozi 58 wa Chama Cha Mapinduzi, wakiongozwa na Ndugu Yohana S. Msita, ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu kutoka Wilaya ya Manyoni Mkoa wa Singida, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hili ndilo tangazo nililokuwa nalo. Sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024]*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Katibu kutusomea, sasa nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari ili aje awasilishe maelezo ya Serikali kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Muswada huu wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3, wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill 2024]*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninachukua nafasi hii kuwatakia wote heri ya mwaka mpya 2025.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri na mafanikio makubwa katika nyanja zote, ikiwemo kuboresha Sekta ya Sheria nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamefanyika chini ya uongozi wake, nasi sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza nchi yetu Kimataifa, kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu; na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao

wa Kikatiba wa kutunga sheria, pamoja na kusimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo; Mheshimiwa Jerry William Silaa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, kuwa Waziri wa Ujenzi; na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ninawatakia heri katika kutekeleza majukumu yao mapya, na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wetu wa Bunge Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Ninapenda kukuahidi kwamba, mimi na ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana Samwel Marco Maneno, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninampongeza Ndugu Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria, pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi.

Tutaendelea kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi, na kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba, na Sheria, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini, sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa, na umeisaidia Serikali katika kuandaa Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Na. 3 wa Mwaka 2024 kama ulivyowasilishwa, unapendekeza marekebisho katika sheria sita zifuatazo: -

(a) Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423;
(b) Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211;
(c) Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201;
(d) Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386;
(e) Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435; na
(f) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi, ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa, na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka

2006 ili kuweka masharti kuhusu udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, na ufadhili wa silaha za maangamizi. Tangu kutungwa kwake sheria hii imerekebishwa mara sita ili kuhakikisha kuwa Tanzania inazingatia viwango vinavyotambulika Kimataifa katika udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19A, ili kumwezesha mdhibiti kutekeleza mamlaka ya kuweka vikwazo vya kiutawala katika mazingira ambapo sheria inayomwongoza mdhibiti haijaainisha mamlaka hayo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba wadhibiti wanatekeleza udhibiti mzuri wa vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211. Sheria hii ilitungwa mwaka 2013 kwa madhumuni ya kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika Tanzania, uundaji, usajili na utendaji wa vyama vya ushirika, pamoja na ukuzaji wa maendeleo ya vyama vya ushirika. Tangu kutungwa kwake, sheria hii imerekebishwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha Wasajili Wasaidizi kutekeleza pia majukumu ya uenezi. Kifungu hiki kilivyo kwa sasa kinawezesha Wasajili Wasadizi kukasimishwa majukumu ya udhibiti pekee. Lengo la marekebisho hayo ni kuwawezesha Wasajili Wasaidizi kutekeleza majukumu ya kila siku ya uenezi kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha muundo wa ngazi ya vyama vya ushirika. Lengo la marekebisho hayo ni kutoa nafasi ya usajili wa wanachama katika ngazi tofauti za vyama vya ushirika ili kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wanachama wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa juu wa idadi ya wanachama katika vyama vya ushirika kwa lengo la kuongeza wigo wa ushiriki wa watu katika shughuli za vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kuongeza Kifungu cha 24A ili kuweka malengo ya msingi ya uundaji wa ushirika ngazi ya juu, kwa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo. Lengo la marekebisho hayo ni kuwa na miongozo itakayowezesha utekelezaji wa shughuli za vyama vya ushirika vya ngazi ya juu vyenye tija kwa maendeleo endelevu kwa vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza muda wa kushughulikia maombi ya usajili. Lengo la marekebisho hayo ni kuharakisha mchakato wa usajili na kukuza ushiriki wa wananchi katika ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuhakikisha benki za ushirika zinatumia wakaguzi waliosajiliwa kama inavyoelekezwa na Benki Kuu kwa lengo la kufanya ukaguzi. Vilevile kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Msajili mamlaka ya kuchukua hatua zozote iwapo vyama vya ushirika vitakuwa na hati chafu baada ya ukaguzi. Hatua hii itatekelezwa kabla ya hatua za kisheria kuchukuliwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa ya kutatua hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 72 na 73 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuviondolea vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 zuio la kukopesha na kupokea amana kutoka kwa wadau wasio wanachama. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki kutekeleza shughuli zake za kibiashara kama benki.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 74 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu benki za ushirika kuwekeza kama benki za kawaida, na pia kuzingatia sera zake za ndani na miongozo ya

Benki Kuu ya Tanzania kuhusu uwekezaji. Vilevile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuweka udhibiti wa uwekezaji wa vyama vya ushirika kupitia kanuni zitakazotengenezwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha mfuko kushughulikia masuala yote ya kazi za udhibiti, isipokuwa gharama za ukaguzi. Marekebisho haya yanakusudia kupanua wigo wa shughuli za kifedha za mfuko.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 81 cha Sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa zuio la uwekaji dhamana wa mali zote kwa vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki. Lengo la marekebisho haya ni kulinda amana ili kuwezesha uendeshaji wenye tija na ufanisi wa biashara ya kibenki.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 141 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni za kusimamia shughuli za uwekezaji na vyama vya ushirika. Lengo la marekebisho hayo ni kumwezesha Waziri kuweka utaratibu utakaosimamia masuala ya uwekezaji katika vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201. Sheria hii ilitungwa mwaka 2001 kwa madhumuni ya kuanzisha Bodi ya Pamba Tanzania ili kuweka masharti bora ya udhibiti, uboreshaji na uendelezaji wa tasnia ya pamba. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara moja. Kwa ujumla, marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga kuimarisha shughuli zinazohusu maendeleo ya tasnia ya pamba, hususan katika ukaguzi wa mbegu za pamba, nyuzi za pamba na viwanda vya kuchakata pamba.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, Serikali inapendekeza kuondoa marekebisho ya jumla yanayopendekezwa katika Sheria hiyo ambayo yalilenga kufuta matumizi ya cheo cha '*Cotton Inspector*', na badala yake kutumia cheo cha '*Agricultural Officer*'. Lengo la marekebisho hayo ilikuwa ni kuwianisha masharti ya sheria na muundo wa

utumishi wa Bodi ulioidhinishwa ambao unatambua cheo cha '*Agricultural Officer*'. Hata hivyo baada ya majadiliano baina ya Serikali na Kamati, kifungu hiki kilionekana ni vyema kibaki kama kilivyo bila kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa mchakataji wa pamba wajibu wa kuweka akiba ya mbegu za pamba pamoja na kuweka adhabu kwa mchakataji ambaye atakiuka wajibu huo. Lengo la mapendekezo hayo ni kukuza akiba ya mbegu za pamba inayotakiwa kuwasilishwa kwa bodi kwa ajili ya kuuzwa kwa wakulima wa pamba katika misimu mingine.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha maafisa kilimo kufanya ukaguzi kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Usimamizi wa Pembejeo zinazopaswa kutumika katika kilimo cha pamba. Aidha, kifungu kipya cha 29A kinapendekezwa kuongezwa ili kuwapa wanunuzi wa pamba wajibu wa kuweka wazi kwa bodi, taarifa kuhusu pamba yote iliyonunuliwa na uwasilishaji wa mbegu za pamba na marobota ya pamba. Lengo la marekebisho haya yanayopendekezwa ni kuwezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi za miamala mbalimbali katika tasnia ya pamba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha na kupanua wigo wa majukumu ya Afisa Kilimo. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha usimamizi madhubuti wa shughuli zilizoahinishwa katika sheria ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya pamba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 38A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayoainisha utaratibu wa usafirishaji na uhifadhi wa mabalo ya pamba na kuahinisha adhabu ya ukiukwaji wa mashariti yaliyowekwa. Aidha, Kifungu kipya cha 38B kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka kwa mchakataji wa pamba wajibu wa kuwasilisha kwa bodi sampuli ya pamba kwa ajili ya upangaji wa madaraja kwa kuzingatia ubora wa pamba. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni

kuongeza uwajibikaji na kupunguza migogoro inayojitokeza kuhusiana na madaraja ya pamba.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386. Sheria hii ilitungwa mwaka 2005 kwa lengo la kuanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa ajili ya kukuza na kuwezesha umiliki wa shughuli za kuzalisha mapato na mali kwa Watanzania, kuweka mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa baraza, kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Kiuchumi na kuweka utaratibu wa udhibiti wa masuala ya fedha ya halmashauri na mfuko.

Mheshimiwa Spika, tangu ilipotungwa sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho, hivyo haya ni marekebisho yake ya kwanza ambayo pamoja na masuala mengine, yanalenga kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha tafsiri za misamiati mbalimbali iliyotumika na kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo haijatafsiriwa katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo ili kuhakikisha kuwa mashariti ya sheria yanaeleweka kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza miongoni mwa majukumu ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, jukumu la kusimamia, kuratibu, kuwezesha na kufanya ufuatiliaji wa taasisi na mashirika yanayofanya shughuli za uwezeshaji kiuchumi na hatua za ushirikiswaji wa wazawa zinazochukuliwa katika sekta mbalimbali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha usimamizi na utaratibu wa pamoja wa shughuli za uwekezaji kiuchumi nchini na kuimarisha nafasi ya baraza katika kusimamia shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Katibu Mtendaji mamlaka ya kukataa maombi ya usajili endapo mwombaji hajakidhi matakwa ya usajili.

Vilevile Kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri, kurekebisha majedwali ya sheria. Marekebisho haya yanalenga kuboresha masharti kuhusu maombi ya usajili na utoaji wa cheti cha usajili na kurahisisha utaratibu wa marekebisho ya majedwali.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 38 na 39 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka adhabu kwa makosa ambayo kwayo adhabu haijaainishwa kwenye sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha makosa yanayotendwa yanawekewa adhabu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435. Sheria hii ilitungwa mwaka 2013 ili kuweka masharti ya uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kuweka utaratibu wa kuendeleza uwendeshaji na matengenezo ya mifumo ya umwagiliaji na mifereji ya maji ili kutoa utekelezaji mzuri wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, mkakati wa maendeleo ya Taifa ya umwagiliaji. Tangu ilipotungwa sheria hii, haijawahi kufanyiwa marekebisho, hivyo haya ni marekebisho yake ya kwanza ambayo pamoja na masuala mengine yanalenga kuboresha masharti ya sheria kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wake bora.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali. Lengo la marekebisho haya ni kuweka tafsiri ya misamiati ambayo ilikuwa imetumika katika sheria, lakini haikuwa imetafsiriwa ili kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tatu na Nne pamoja na Jedwali, vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa matumizi ya neno "*Commission*" na badala yake kutumia neno "*Board*". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurekebisha makosa ya kiuandishi yaliyojitokeza wakati wa utungaji wa sheria na kuhakikisha masharti husika yanatumika kwa bodi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayoelekeza tume kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa umwagiliaji. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko kwa kuwa ushirikiano kati ya tume na mashirika ya ndani au nje ya nchi ni katika uwendelezaji wa umwagiliaji na siyo katika usimamizi wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza masharti yanayovipa vyama vya umwagiliaji vilivyoanzishwa chini ya sheria ya umwagiliaji utu wa kisheria. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza tija kwa vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa kwa kuvipa nguvu kisheria, kufanya masuala mbalimbali kama vile kuingia mkataba, kumiliki mali na kuviwezesha kupata huduma mbalimbali kama vile kukopa katika taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hicho kinarekebishwa ili kuweka masharti yatakayowezesha maelekezo kutoka kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, kutolewa kwa vyama vya umwagiliaji baada ya mashauriano na tume. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa hakuna mgongano wa maelekezo yanayotolewa kwa vyama kutoka kwa tume na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuviongezea vyama vya umwagiliaji jukumu la kuandaa hesabu, bajeti na kumbukumbu nyingine za vyama kila mwaka. Lengo la marekebisho haya yanayopendekezwa ni kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za vyama vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Sheria hii ilitungwa mwaka 2008 ili kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uwezo wa kufanya ukaguzi wa hesabu za umma kwa madhumuni ya kukuza uwajibikaji katika taasisi kwa kuzuia ubadhirifu wa fedha, rushwa

na utoaji wa taarifa kwa walipa kodi kuhusu utekelezaji wa sera na programu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza Kifungu kipya cha 4A ili kuweka masharti kuhusu namna ambavyo malipo na stahili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitaamuliwa na kufanyiwa mabadiliko. Madhumuni ya marekebisho haya ni kubainisha mamlaka ya Mheshimiwa Rais, kuhusu maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali katika sheria ili kukidhi upangaji wa maslahi hayo kwa kuzingatia uhalisia wa ofisi hiyo na zuio la Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kutoshika nafasi yoyote ya madaraka baada ya kustaafu utumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2023, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2024)* ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA SAID JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 3 WA MWAKA 2024 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 03) BILL, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 03) Bill, 2024)*. Vilevile, nichukue nafasi hii kuwatakia wote heri ya mwaka mpya 2025.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa** kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Urais mwaka 2025. Pia, nampongeza Balozi Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuteuliwa kugombea nafasi ya Urais Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika** kwa nafasi ya pekee napenda kumpongeza Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Jerry William Silaa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Dkt Damas Daniel Ndumbaro kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Mhandisi Hamadi Yusuf Masauni kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mh. Abdallah Hamisi Ulega kuwa Waziri wa Ujenzi na Mhe. Innocent Lugha Bashungwa kuwa

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ninawatakia heri katika kutekeleza majukumu yenu mapya na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.
Aidha, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bw. Baraka Ildiphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Samwel Marco Maneno kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, ninampongeza Ndg. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi. Tutaendelea kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Ushauri uliotolewa na kamati umezingatiwa na pia umesaidia Serikali katika kuandaa Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 03) Bill, 2024) kama

ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria Kuu Sita (6) zifuatazo:

1. Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 (The Anti-Money Laundering Act, Cap. 423);
2. Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211, (The Co-operative Societies Act, Cap. 211);
3. Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201, (The Cotton Industry Act, Cap. 201);
4. Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386, (The National Economic Empowerment Act, Cap. 386);
5. Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435 (The National Irrigation Act, Cap. 435); na
6. Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 (The Public Audit Act, Cap. 418).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Saba. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo Sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka 2006 ili kuweka masharti kuhusu udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara sita ili kuhakikisha kuwa Tanzania inazingatia viwango vinavyotambulika kimataifa katika udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kurekebisha kifungu cha 19A ili kumwezesha mdhibiti kutekeleza mamlaka ya kuweka vikwazo vya kiutawala katika mazingira ambapo sheria inayomwongoza mdhibiti haijaainisha mamlaka hayo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba wadhibiti wanatekeleza udhibiti mzuri wa vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211. Sheria hii ilitungwa mwaka 2013 kwa madhumuni ya kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika Tanzania, uundaji, usajili na utendaji wa vyama vya ushirika pamoja na ukuzaji wa maendeleo ya vyama vya ushirika. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara moja.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha Wasajili Wasaidizi kutekeleza pia majukumu ya uenezi. Kifungu kilivyo kwa sasa kinawezesha Wasajili Wasadizi kukasimishwa majukumu ya udhibiti pekee. Lengo la marekebisho hayo ni kuwawezesha wasajili wasaidizi kutekeleza majukumu ya kila siku ya uenezi kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume. Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha muundo wa ngazi ya vyama vya ushirika. Lengo la marekebisho hayo ni kutoa nafasi ya usajili wa wanachama katika ngazi tofauti za vyama vya ushirika ili kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wanachama wa vyama vya ushirika. Kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa juu wa idadi ya wanachama katika vyama vya ushirika kwa lengo la kuongeza wigo wa ushiriki wa watu katika shughuli za vyama vya ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza kuongeza kifungu cha 24A ili kuweka malengo ya msingi wa uundaji wa ushirika ngazi ya juu kwa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo. Lengo la marekebisho haya ni kuwa na miongozo itakayowezesha utekelezaji wa shughuli za vyama vya ushirika vya ngazi ya juu vyenye tija kwa maendeleo endelevu kwa vyama hivyo. Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza muda wa kushughulikia maombi ya usajili. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha mchakato wa usajili na kukuza ushiriki wa wananchi katika ushirika. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuhakikisha benki za ushirika zinatumia wakaguzi waliosajiliwa kama inavyoelekezwa na Benki Kuu kwa lengo la kufanya ukaguzi. Vilevile, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Msajili mamlaka ya kuchukua hatua zozote iwapo vyama vya ushirika vitakuwa na hati chafu baada ya ukaguzi. Hatua hii

itatekelezwa kabla ya hatua za kisheria kuchukuliwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa ya kutatua hoja za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 72 na 73 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuviondolea vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342, zuio la kukopesha na kupokea amana kutoka kwa watu wasio wanachama. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki kutekeleza shughuli zake za kibiashara kama benki. Kifungu cha 74 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu benki za ushirika kuwekeza kama benki za kawaida na pia kuzingatia sera zake za ndani na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu uwekezaji. Vilevile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuweka udhibiti wa uwekezaji wa vyama vya ushirika kupitia kanuni zitakazotengenezwa na Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha mfuko kushughulikia masuala yote ya kazi za udhibiti isipokuwa gharama za ukaguzi. Marekebisho haya yanakusudia kupanua wigo wa shughuli za kifedha za mfuko. Kifungu cha 81 cha Sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa zuio la uwekaji dhamana wa mali zote kwa vyama vya ushirika vinavyofanya kazi za kibenki. Lengo la marekebisho haya ni kulinda amana ili kuwezesha uendeshaji wenye tija na ufanisi wa biashara ya kibenki. Kifungu cha 141 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni za kusimamia shughuli za uwekezaji na vyama vya ushirika. Lengo la marekebisho hayo ni kumuwezesha Waziri kuweka utaratibu utakaosimamia masuala ya uwekezaji katika vyama vya ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201. Sheria hii ilitungwa mwaka 2001 kwa madhumuni ya kuanzisha Bodi ya Pamba Tanzania ili kuweka masharti bora ya udhibiti, uboreshaji na uendelezaji wa tasnia ya pamba. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara moja. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga kuimarisha shughuli zinazohusu maendeleo ya tasnia

ya pamba hususani katika ukaguzi wa mbegu za pamba, nyuzi za pamba na viwanda vya kuchakata pamba.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Jedwali la Marekebisho Serikali inapendekeza kuondoa marekebisho ya jumla yanayopendekezwa katika Sheria hiyo ambayo yalilenga kufuta matumizi ya cheo cha "*cotton inspector*" na badala yake kutumia cheo cha "*agicultural officer*". Lengo la marekebisho hayo lilikuwa ni kuwianisha masharti ya Sheria na muundo wa utumishi wa Bodi ulioidhinishwa ambao unatambua cheo cha "*agricultural officer*". Hata hivyo, baada ya majadiliano baina ya Serikali na Kamati, kifungu hiki kilionekana ni vyema kibaki kama kilivyo bila kurekebishwa. Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa mchakataji wa pamba wajibu wa kuweka akiba ya mbegu za pamba pamoja na kuweka adhabu kwa mchakataji ambaye atakiuka wajibu huo. Lengo la mapendekezo hayo ni kukuza akiba ya mbegu za pamba inayotakiwa kuwasilishwa kwa Bodi kwa ajili ya kuuzwa kwa wakulima wa pamba katika misimu mingine.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha maafisa kilimo kufanya ukaguzi kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya usimamizi wa pembejeo zinazopaswa kutumika katika kilimo cha pamba. Aidha, kifungu kipya cha 29A kinapendekezwa kuongezwa ili kuwapa wanunuzi wa pamba wajibu wa kuweka wazi kwa Bodi taarifa kuhusu pamba yote iliyonunuliwa na uwasilishaji wa mbegu za pamba na marobota ya pamba. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha upaikanaji wa takwimu na taarifa sahihi za miamala mbalimbali katika tasnia ya pamba. Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha na kupanua wigo wa majukumu ya afisa kilimo. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha usimamizi madhubuti wa shughuli zilizoainishwa katika Sheria ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya pamba.

Kifungu kipya cha 38A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayoainisha utaratibu wa usafirishaji na uhifadhi wa mabalo ya pamba na kuainisha adhabu ya ukiukwaji wa masharti

yaliyowekwa. Aidha, kifungu kipya cha 38B kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka kwa mchakataji wa pamba wajibu wa kuwasilisha kwa Bodi sampuli ya pamba kwa ajili ya upangaji wa madaraja kwa kuzingatia ubora wa pamba. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwajibikaji na kupunguza migogoro inayojitokeza kuhusiana na madaraja ya pamba.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386. Sheria hii ilitungwa mwaka 2005 kwa lengo la kuanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa ajili ya kukuza na kuwezesha umiliki wa shughuli za kuzalisha mapato na mali kwa Watanzania, kuweka mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa Baraza, kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Kiuchumi na kuweka utaratibu wa udhibiti wa masuala ya fedha ya Halmashauri na Mfuko. Tangu ilipotungwa, Sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho hivyo, haya ni marekebisho yake ya kwanza ambayo pamoja na masuala mengine, yanalenga kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha tafsiri za misamiti mbalimbali iliyotumika na kuongeza tafsiri ya msamiati ambao haujatafsiriwa katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo ili kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria yanaeleweka kama ilivyokusudiwa. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza miongoni mwa majukumu ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, jukumu la kusimamia, kuratibu, kuwezesha na kufanya ufuatiliaji wa taasisi na mashirika yanayofanya shughuli za uwezeshaji kiuchumi na hatua za ushirikishwaji wa wazawa zinazochukuliwa katika sekta mbalimbali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha usimamizi na uratibu wa pamoja wa shughuli za uwekezaji kiuchumi nchini na kuimarisha nafasi ya Baraza katika kusimamia shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Katibu Mtendaji mamlaka ya kukataa maombi ya usajili endapo mwombaji hajakidhi matakwa ya usajili.

Vilevile, kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuwezesha Waziri kurekebisha Majedwali ya Sheria. Marekebisho haya yanalenga kuboresha masharti kuhusu maombi ya usajili na utoaji wa cheti cha usajili na kurahisisha utaratibu wa marekebisho ya Majedwali. Vifungu vya 38 na 39 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka adhabu kwa makosa ambayo kwayo adhabu haijaainishwa kwenye Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha makosa yanayotendwa yanaadhibiwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435. Sheria hii ilitungwa mwaka 2013 ili kuweka masharti ya uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kuweka utaratibu wa kuendeleza, uendeshaji na matengenezo ya mifumo ya umwagiliaji na mifereji ya maji ili kutoa utekelezaji mzuri wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Mkakati wa Maendeleo ya Taifa wa Umwagiliaji. Tangu ilipotungwa, Sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho hivyo, haya ni marekebisho yake ya kwanza ambayo pamoja na masuala mengine, yanalenga kuboresha masharti ya Sheria kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wake bora.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali. Lengo la marekebisho haya ni kuweka tafsiri ya misamiati ambayo ilikuwa imetumika katika Sheria lakini haikuwa imetafsiriwa ili kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo. Vifungu vya 3 na 4 pamoja na Jedwali vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa matumizi ya neno ''Commission" na badala yake kutumia neno "Board". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurekebisha makosa ya kiuandishi yaliyojitokeza wakati wa utungaji wa Sheria na kuhakikisha masharti husika yanatumika kwa Bodi kama ilivyokusudiwa. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayoelekeza Tume kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa umwagiliaji. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko kwa kuwa ushirikiano kati ya Tume na mashirika ya ndani au nje ya nchi ni katika uendelezaji wa umwagiliaji na sio katika usimamizi wa umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 29 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza masharti yanayovipa vyama vya umwagiliaji vilivyoanzishwa chini ya Sheria ya Umwagiliaji utu wa kisheria. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza tija kwa vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa kwa kuvipa nguvu kisheria kufanya masuala mbalimbali kama vile kuingia mikataba, kumiliki mali na kuviwezesha kupata huduma mbalimbali kama vile kukopa katika taasisi za fedha. Aidha, kifungu hicho pia kinarekebishwa ili kuweka masharti yatakayowezesha maelekezo kutoka kwa mamlaka za serikali za mitaa kutolewa kwa vyama vya umwagiliaji baada ya mashauriano na Tume. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa hakuna mgongano wa maelekezo yanayotolewa kwa vyama kutoka kwa Tume na mamlaka za serikali za mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuviongezea vyama vya umwagiliaji jukumu la kuandaa hesabu, bajeti na kumbukumbu nyingine za vyama kila mwaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za vyama vya umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Sheria hii ilitungwa mwaka 2008 ili kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uwezo wa kufanya ukaguzi wa hesabu za umma kwa madhumuni ya kukuza uwajibikaji katika taasisi za kidemokrasia kwa kuzuia ubadhirifu wa fedha, rushwa na utoaji wa taarifa kwa walipakodi kuhusu utekelezaji wa sera na programu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 4A ili kuweka masharti kuhusu namna ambavyo malipo na stahili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitaamuliwa au kufanyiwa mabadiliko. Madhumuni ya marekebisho haya ni kubainisha mamlaka ya Rais kuhusu maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Sheria ili kukidhi upangaji wa maslahi hayo kwa kuzingatia uhalisia wa Ofisi hiyo na zuio la Mdhibiti na

Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kutoshika nafasi yoyote ya madaraka baada ya kustaafu utumishi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 03) wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 03) Bill, 2024) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA.

Hamza Said Johari (Mb.),
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
29 Januari, 2025

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake anakuja Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo. *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, maelezo ya awali na hadidu za rejea. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 96(1) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza katika Mkutano wa 16, Kikao cha Tisa kwenye Bunge la Kumi na Mbili tarehe 6 Septemba, 2024. Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Muswada, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 16 Oktoba, 2024 ili kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, kuhusu maudhuhi ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibala mbalimbali za Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* tarehe 17 Oktoba, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa Chama cha Wanasheria Tanganyika ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao. Kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mnamo tarehe 20 Oktoba, 2024 Kamati ilikutana na Mheshimiwa Hussein Bashe, Mbunge na Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao kwa pamoja walijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi ya Muswada huu ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2024 ukiwa umegawanyika katika sehemu saba na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita kwa madhumuni ya kuondoa upungufu na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hiyo. Sheria zilizopendekezwa kufanyia marekebisho ni kama zifuatavyo: -

(a) Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 *(The Anti Money Laundering Act, Cap. 423);*

(b) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211 *(The Cooperative Societies Act, Cap. 211);*

(c) Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201 *(The Cotton Industry Act, Cap. 201);*

(d) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386 *(The National Economic Empowerment Act, Cap. 386);*

(e) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435 *(The National Irrigation Act, Cap. 435);* na

(f) Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 *(The Public Audit Act, Cap. 418)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi inayojumuisha Ibara ya Kwanza inayohusu jina fupi na Ibara ya Pili inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake. Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au upungufu katika sheria nne kati ya sheria sita zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211, marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya Tano hadi Ibara ya 17 ya Muswada. Ibara ya 10 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 31 kinachohusu kushughulikia maombi ya usajili kwa kufuta neno "*sixty*" lililopo katika kifungu kidogo cha kwanza na badala yake kuweka neno "*twenty*".

Mheshimiwa Spika, vilevile ibara inapendekeza kuongeza maneno "*within ten days from the date of the refusal*" mara baada ya neno "*lighting*" lililopo katika kifungu kidogo cha (2)(c). Lengo ni kupunguza muda wa Msajili kushughulikia maombi ya usajili kutoka siku 60 hadi 20 na kumbana Msajili kutoa taarifa ya maandishi ndani ya siku 10 kwa maombi yaliyokataliwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha (4) na kuongeza kifungu kidogo cha (14) katika kifungu cha 55 kinachohusu hesabu na ukaguzi wa hesabu za vyama vya ushirika vilivyosajiliwa. Katika kifungu kidogo kipya cha (4), mkaguzi atakayekagua hesabu za Benki ya Ushirika atatakiwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu kutoka kwenye orodha ya wakaguzi waliyoidhinishwa na Benki Kuu na Msajili kutaarifiwa juu ya uteuzi huo. Lengo ni kuhakikisha wanateuliwa wakaguzi walioidhinishwa na Benki Kuu na benki

itakuwa na wajibu wa kumtaarifu Msajili na siyo kupata idhini yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu kidogo cha (14) kinachoongezwa, kinampa Msajili mamlaka ya kuchukua hatua za awali za kurekebisha hesabu za Chama cha Ushirika kutokana na matokeo ya ukaguzi uliyofanyika. Lengo ni kutoa fursa ya kutatua hoja za ukaguzi kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 95 au 55(13) juu ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 18 hadi Ibara ya 24 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 inapendekeza kufanya marekebisho ya jumla katika sheria kwa kufuta maneno "*cotton inspector*" na badala yake kuweka maneno "*agricultural officer*". Lengo la marekebisho ilikuwa ni kufuta cheo cha *cotton inspector* na kutumia cheo cha *agricultural officer* ili kuyaainisha na masharti ya sheria na muundo wa utumishi wa bodi ulioidhinishwa ambao unatambua cheo cha *agricultural officer*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386. Marekebisho haya yanafafanuliwa katika Ibara ya 25 hadi Ibara ya 31 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 27 kama ifuatavyo: kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3), (4) na (5) mara baada ya Kifungu kidogo cha (2), maudhui ya vifungu vidogo vinavyoongezewa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kuwa Katibu Mtendaji anaweza kukataa maombi ya usajili yaliyofanyika chini ya kifungu kidogo cha (1) kama maombi hayatazingatia matakwa yaliyoidhinishwa katika jedwali la kwanza la sheria.

(ii) Kifungu kidogo cha (4) kinaeleza kuwa pale ambapo maombi yatakataliwa chini ya Kifungu kidogo cha (3) Katibu Mtendaji atampatia mwombaji sababu za maombi husika kukataliwa ndani ya muda wa siku 14.

(iii) Kifungu kidogo cha (5) kinaeleza kuwa maombi yaliyokataliwa katika kifungu hiki yanaweza kuwasilishwa tena baada ya kurekebisha upungufu.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho ni kuboresha utendaji kazi wa Katibu Mtendaji wa Baraza. Vilevile ibara inafuta Kifungu cha 27(3) na kukiandika upya. Kifungu kipya kinaeleza kuwa Waziri anaweza kwa amri itakayotangazwa katika Gazeti la Serikali kurekebisha, kuongeza, kutofautisha au kubadili jedwali la kwanza la sheria hii. Lengo ni kumpatia Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kurekebisha jedwali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 29 inapendekeza kufuta na kuandika upya Kifungu cha 28(4) ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri kwa amri itakayotangazwa katika Gazeti la Serikali kurekebisha, kuongeza, kutofautisha au kubadili jedwali la pili la sheria hii. Lengo ni kumpatia Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kurekebisha jedwali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418. Marekebisho haya yanafafanuliwa katika Ibara ya 40 hadi Ibara ya 41 ya Muswada. Ibara ya 41 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 4(A) baada ya Kifungu cha Nne kinachohusu stahili na marupurupu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kifungu hicho kinampa mamlaka Mheshimiwa Rais, kuweza kufanya mabadiliko ya stahili na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa katika utumishi ama baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho kinaweka sharti kwa Mheshimiwa Rais kuzingatia Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sura ya pili na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kufanya

mabadiliko. Marekebisho hayo yamezingatia zuio la Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kutoshika nafasi yoyote ya madaraka baada ya kustaafu utumishi.

Mheshimiwa Spika, katika maoni na ushauri wa Kamati, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura 211, kwenye Ibara ya 10 ya Muswada Kamati ilishauri Serikali kufanya maboresho kwa kupunguza muda wa Msajili kushughulikia maombi ya usajili kutoka siku 20 hadi 14 na kumbana Msajili kutoa taarifa ya maandishi ndani ya siku saba kwa maombi yaliyokataliwa. Msingi wa pendekezo la Kamati umezingatia kuwa maombi ya usajili yanafanyika kwa njia ya mtandao. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 11 Kamati ilishauri kufuta maneno *Bank of Tanzania* lililotumika katika Kifungu (4) kinachopendekezwa na kutumika kwa neno '*bank*' pekee. Msingi wa pendekezo hili ni neno '*bank*' lililo katika kifungu cha Tafsiri ya Sheria za Vyama vya Ushirika limetafsiriwa kuwa *Bank of Tanzania*. Tunaipongeza Serikali kwa kubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 3.3 marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura 201, Ibara ya 19 inapendekeza kufuta matumizi ya Cheo cha *Cotton Inspector* (Afisa Pamba) na badala yake kutumia Cheo cha *Agricultural Officer* (Afisa Kilimo). Kamati ilishauri Serikali kuwa upo umuhimu wa kubaki na kada ya Afisa Pamba kwani Maafisa hao wana utaalamu mahususi kwenye zao la pamba. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 3.4 ni marekebisho ya Sheria ya Uwezeshaji wa Kiuchumi Sura 386, Ibara ya 28 inapendekeza kufanya maboresho kwenye kifungu cha 27 kwa kuongeza Vifungu vidogo vya (3), (4) na (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (2). Katika Kifungu kidogo cha (4) pale ambapo maombi ya usajili yatakaliwa, Katibu Mtendaji wa Baraza atampatia mtu aliyeomba usajili sababu za maombi husika kukataliwa ndani ya muda wa siku 14.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza muda wa Katibu Mtendaji kumfahamisha mleta maombi ya usajili sababu za kukataliwa maombi kupungua kutoka siku 14 na kuwa siku saba. Lengo la mapendekezo haya lilizingatia kuwa maombi yanafanyika kwa njia ya mtandao. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 29 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 28 na kumruhusu Waziri kufanya marekebisho ya majedwali ya sheria. Pamoja na kuwa sheria nyingi zimempa Waziri uwezo wa kufanya mabadiliko kwenye majedwali ya sheria, Kamati ilishauri Serikali kufuta maneno ambayo yanasomeka '*or replace*' yanayoonekana kwenye Ibara 28 na Ibara ya 29 kwa kuwa lengo ni kufanya mabadiliko madogo na siyo kuyabadili kwa kuyaondoa na kuyaandika upya. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418: Ibara ya 41 inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 4(A) baada ya Kifungu cha Nne kinachohusu stahili na marupurupu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kifungu hicho kinampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuweza kufanya mabadiliko ya stahili na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa katika utumishi ama baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho kinaweka sharti kwa Mheshimiwa Rais kuzingatia Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania sura ya pili na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kufanya rejea sahihi ya Ibara ya 142(3) na Ibara ya 144(6) ambazo zinaweka masharti ya mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya Ibara ya 142(3), maslahi yake hayatabadilishwa kwa maana ya kupunguzwa na hatateuliwa katika kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mtawalia. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla: Kamati ilishauri Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Sura 435, kwa kushusha mamlaka ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji hadi ngazi ya wilaya ili kuendana na mfumo wa dhana ya uhuru wa Tume kama unavyoonekana katika sehemu ya tatu ya sheria hiyo, badala ya Tume kuwakilishwa na Afisa ambao wapo chini ya Halmashauri. Tunaipongeza Serikali kwa kubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ina maoni kwamba pindi Bunge lako litakaporidhia kupitisha Muswada huu Serikali, ihakikishe inasimamia ipasavyo maboresho haya ili yaweze kuleta tija kwa wakulima na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilishauri Serikali kwa ujumla wake kufanya maboresho ya vifungu vya adhabu kwenye Ibara ya 20, 22, 24, 30 na 31 kwa kuweka ukomo wa juu, ukomo wa chini na uwiano wa adhabu ya faini na vifungo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mwongozo wa upangaji wa uwiano wa adhabu ya faini na kifungo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni shukurani. Naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako

na maelekezo yako vimekuwa ni chachu na nyenzo kubwa na muhimu katika ufanisi wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee, ninapenda kuchukua fursa hii pia kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ndugu Samweli Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndugu Onorius Njole; pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee pia tumpongeza Mheshimiwa Jaji Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Jaji wa Mahakama Kuu na tunamshukuru kwa ushirikiano wake wakati huo akiwepo wakati tunaendelea na Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Ndugu Baraka I. Leonard kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge na Kamati inamwahidi ushirikiano uliotukuka. Pia nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge na kwa kipekee Sekretarieti ya Kamati chini ya uongozi wa aliyekuwa Katibu wa Kamati hii, Ndugu Frank Nkya kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja. Baada ya kusema hayo Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ninaomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na.3) WA MWAKA 2024 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)* (No.3) *BILL, 2024]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2024)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na sita, kikao cha tisa kwenye Bunge la 12, tarehe 06 Septemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 16 Oktoba, 2024 ili kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza Johari (Mb) kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya mkutano wa kusikiliza maoni ya Wadau *(Public Hearing)* tarehe 17 Oktoba, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa Chama cha Wanasheria Tanganyika ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Kipekee Niwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mnamo tarehe 20 Oktoba, 2024 Kamati ilikutana na Mhe. Hussein Bashe (Mb) Waziri wa Kilimo na Mhe. Hamza Johari (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao kwa pamoja walijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2024 *[The*

*Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu saba (7) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita (6) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

a) Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 (*The Anti-Money Laundering Act, (Cap 423));*

b) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211 *(The Cooperative Societies Act, (Cap 211))*;

c) Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201 *(The Cotton Industry Act, (Cap 201))*;

d) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura ya 386 *(The National Economic Empowerment Act, (Cap 54))*;

e) Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435 *(The National Irrigation Act, (Cap 435))*; na

f) Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 *(The Public Audit Act, (Cap 418))*;

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

**2.2 Sheria zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake**

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria nne kati ya sheria sita zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211.** Marekebisho hayo yanayofafanuliwa katika Ibara ya 5 hadi Ibara ya 17 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 10 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 31 kinachohusu kushughulikia maombi ya usajili kwa kufuta neno "*sixty*" yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka neno "*twenty*". Vilevile ibara inapendekeza kuongeza maneno "*within ten days from the date of the refusal*" mara baada ya neno "*writing*" lililopo katika kifungu kidogo cha (2)(c). Lengo ni kupunguza muda wa Msajili kushughulikia maombi ya usajili kutoka siku sitini hadi ishirini na kumbana Msajili kutoa taarifa ya maandishi ndani ya siku kumi kwa maombi yaliyokataliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 11 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha (4) na kuongeza kifungu kidogo cha (14) katika kifungu cha 55 kinachohusu hesabu na ukaguzi wa hesabu za vyama vya ushirika vilivyosajiliwa. Katika kifungu kidogo cha (4) kipya mkaguzi atakayekagua hesabu za benki ya ushirika atatakiwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu kutoka kwenye orodha ya Wakaguzi walioidhinishwa na Benki Kuu na Msajili kutaarifiwa juu ya uteuzi huo. Lengo ni kuhakikisha wanateuliwa wakaguzi waliodhinishwa na Benki kuu na benki itakuwa na wajibu wa kumtaarifu Msajili na si kupata idhini yake.

Aidha, kifungu kidogo cha (14) kinachoongezwa kinampa Msajili mamlaka ya kuchukua hatua za awali za kurekebisha hesabu za chama cha ushirika kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanyika. Lengo ni kutoa fursa ya kutatua hoja za ukaguzi kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 95 au 55(13) vya Sheria hii.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura ya 201.** Marekebisho hayo yanayofafanuliwa katika Ibara ya 18 hadi Ibara ya 24 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 19 inapendekeza kufanya marekebisho ya jumla katika Sheria kwa kufuta maneno "*cotton inspector*" na badala yake kuweka maneno "*agricultural officer*". Lengo la marekebisho ni kufuta cheo cha "*cotton inspector*" na kutumia cheo cha "*agricultural officer*" ili kuwianisha masharti ya Sheria na muundo wa utumishi wa Bodi ulioidhinishwa ambao unatambua cheo cha "*agricultural officer*".

**2.2.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura 386**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 25 hadi Ibara ya 31 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 28 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 27 kama ifuatavyo: -

Kwa kuongeza vifungu vidogo (3), (4) na (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (2). Maudhui ya vifungu vidogo vinavyoongezwa ni: -

(i) Kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kuwa, Katibu Mtendaji anaweza kukataa maombi ya usajili yaliyofanyika chini ya kifungu kidogo cha (1) kama maombi hayatazingatia matakwa yaliyoainishwa katika jedwali la kwanza la sheria;

(ii) Kifungu kidogo cha (4) kinaeleza kuwa, pale ambapo maombi yatakataliwa chini ya kifungu kidogo cha (3), Katibu Mtendaji atampatia mwombaji sababu za maombi husika kukataliwa ndani ya muda wa siku kumi na nne; na

(iii) Kifungu kidogo cha (5) kinaeleza kuwa, maombi yaliyokataliwa katika kifungu hiki yanaweza kuwasilishwa tena baada ya kurekebisha mapungufu. Lengo la marekebisho ni kuboresha utendaji kazi wa Katibu Mtendaji wa Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Ibara inafuta kifungu cha 27(3) na kukiandika upya. Kifungu kipya kinaeleza kuwa Waziri anaweza, kwa amri itakayotangazwa katika gazeti la serikali, kurekebisha,

kuongeza, kutofautisha au kubadili jedwali la kwanza la sheria hii. Lengo ni kumpatia Waziri mamlaka ya kurekebisha jedwali.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 29 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 28 (4) ili kumwezesha Waziri, kwa amri itakayotangazwa katika gazeti la serikali, kurekebisha, kuongeza, kutofautisha au kubadili jedwali la pili la sheria hii. Lengo ni kumpatia Waziri mamlaka ya kurekebisha jedwali.

**2.2.4 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 40 hadi Ibara ya 41 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 41 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 4A baada ya kifungu cha 4 kinachohusu stahili na marupurupu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kifungu hicho kinampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuweza kufanya mabadiliko ya stahili na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa katika utumishi ama baada ya kustaafu.

Kifungu hicho kinaweka sharti kwa Mheshimiwa Rais kuzingatia Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2 na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kufanya mabadiliko. Marekebisho hayo yamezingatia zuio la Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kutokushika nafasi yoyote ya madaraka baada ya kustaafu utumishi.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya

marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata: -

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211 (*The Cooperative Societies Act, (Cap 211)*).

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 10 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho kwa kupunguza muda wa Msajili kushughulikia maombi ya usajili kutoka siku ishirini hadi kumi na nne na kumbana Msajili kutoa taarifa ya maandishi ndani ya siku saba kwa maombi yaliyokataliwa, msingi wa pendekezo la Kamati umezingatia kuwa maombi ya usajili yanafanyika kwa njia ya mtandao. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kwenye Ibara ya 11 Kamati ilishauri kufuta maneno "*Bank of Tanzania*" lililotumika katika kifungu kidogo cha (4) kinachopendekezwa na kutumika kwa neno "*Bank*" pekee, msingi wa pendekezo hili ni neno *"Bank*" lililopo katika kifungu cha tafsiri ya sheria ya Vyama vya Ushirika limetafsiriwa kuwa ni "*Bank of Tanzania*". Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura 201 (*The Cotton Industry Act, (Cap 201)*).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 19 inapendekeza kufuta matumizi ya cheo cha "*cotton inspector*" yani Afisa Pamba na badala yake kutumia cheo cha "*agricultural officer*" Afisa Kilimo. Kamati iliishauri Serikali kuwa upo umuhimu wa kubaki na kada ya Afisa Pamba kwani maafisa hao wana utaalaam mahususi kwenye zao la Pamba. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.4 Marekebisho ya Sheria ya Uwezeshaji wa Kiuchumi, Sura 386 *(The National Economic Empowerment Act, (Cap386))*.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 28 inapendekeza kufanya maboresho kwenye kifungu cha 27 kwa kuongeza vifungu vidogo

(3), (4) na (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (2). Katika kifungu kidogo cha (4), pale ambapo maombi ya usajili yatakataliwa, Katibu Mtendaji wa Baraza atampatia mtu aliyeomba usajili sababu za maombi husika kukataliwa ndani ya muda wa siku kumi na nne.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipendekeza muda wa Katibu Mtendaji kumfahamisha mleta maombi ya usajili sababu za kukataliwa maombi kupungua kutoka siku kumi na nne (14) na kuwa siku saba (7). Lengo la Mapendekezo haya uliziingatia kuwa maombi yanafanyika kwa njia ya mtandao. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 29 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 28 kwa kumruhusu Waziri kufanya marekebisho ya Majedwali ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa Sheria nyingi zimempa Waziri kufanya mabadiliko kwenye majedwali ya Sheria, Kamati iliishauri Serikali kufuta maneno "*or replace*" yanayoonekana kwenye Ibara ya 28 na 29 kwa kuwa lego ni kufanya mabadiliko madogo na si kuyabadili kwa kuyaondoa na kuyaandika upya. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.5 Marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 (*The Public Audit Act, (Cap 418)*).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 41 inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu cha kipya cha 4A baada ya kifungu cha 4 kinachohusu stahili na marupurupu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kifungu hicho kinampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuweza kufanya mabadiliko ya stahili na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa katika utumishi ama baada ya kustaafu.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu hicho kinaweka sharti kwa Mheshimiwa Rais kuzingatia Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2 na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa kufanya mabadiliko.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kufanya rejea sahihi ya Ibara ya 142(3) na Ibara ya 144(6); ambazo zinaweka masharti ya mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya ibara ya 142(3) maslahi yake hayatabadilishwa kwa maana ya kupunguzwa na hatateuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mtawalia. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.6 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, Sura ya 435 kwa kushusha mamlaka ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji hadi ngazi za wilaya ili kuendana na mfumo na dhana ya uhuru wa Tume kama unavyoonekana katika Sehemu ya Tatu ya Sheria hiyo, badala ya Tume kuwakilishwa na afisa ambao wapo chini ya Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.Vilevile Kamati ina maoni kwamba pindi Bunge lako litakaporidhia kuupitisha Muswada huu Serikali ihakikishe inasimamia ipasavyo maboresho haya ili yaweze kuleta tija kwa wakulima na wananchi kwa ujumla.

Aidha, Kamati iliishauri Serikali kwa ujumla wake kufanya maboresho ya vifungu vya adhabu kwenye Ibara ya 20, 22, 24, 30 na 31 kwa kuweka ukomo wa juu, ukomo wa chini na uwiano wa adhabu ya faini na vifungo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mwongozo wa upangaji wa uwiano wa adhabu ya faini na kifungo.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb | -**Makamu Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | - Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb | - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo,Mb | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Hamza Johari (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndg. Samwel Maneno Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Mhe. Jaji Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, tunamshukuru kwa ushirikiano wake kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge, Kamati inamuahidi ushirikiano uliotukuka. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati chini ya uongozi wa aliyekuwa Katibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la
Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

29 Januari, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa wasilisho hilo la maoni ya Kamati ili Bunge liweze kuyafahamu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu ili alete huu Muswada mwingine, nitoe maelezo kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, Muswada wetu wa *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2024)* una sehemu tisa, lakini katika hizi sehemu tisa sehemu ya tano inayohusu

*Amendment of The Immigration Act Cap 54* na *Part Seven* ambayo inahusu *Amendment of The Land Act Cap 113*.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utakapokuja kuwasilisha hapa, hizi sehemu mbili bado Bunge linazifanyia kazi, lakini sehemu nyingine zote zipo tayari. Kwa hiyo, hata wewe wakati unawasilisha ufahamu hizi sehemu mbili Bunge bado linazifanyia kazi.

Kwa hiyo, utawasilisha hoja yako kuhusu sehemu nyingine zote isipokuwa hizi mbili. Vivyo hivyo, Kamati itakapokuja hapa itawasilisha maoni yake kuhusu sehemu nyingine zote isipokuwa hizo mbili kwa sababu bado Bunge linafanyia kazi hoja zilizoko katika hizi sehemu mbili na tutakapokuwa tayari, basi kazi hiyo itafanyika kwa utaratibu ambao tumejiwekea kama Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa tuendelee.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite tena Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johari Hamza, aje awasilishe hoja yake kuhusu Muswada huu akiwa ameondoa hizo sehemu mbili kama nilivyotoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha wote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, pia, ni dua yangu kwa Mwenyezi Mungu ni kuwa atujalie wote afya njema na nguvu za kuendelea kutekeleza majukumu yetu na kuendesha shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii tena kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa umahiri na mafanikio makubwa katika nyanja zote ikiwemo kuboresha sekta ya sheria nchini. Mengi yamefanyika chini ya uongozi wake na sisi sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza nchi kimataifa kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sababu haya maelezo ya hapa awali umetoka kuyasema kwenye ile taarifa nyingine, na hii itaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, ninadhani unaweza kuanzia moja kwa moja pale kwenye Muswada.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2024 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024)* ambao uko mbele

ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria sita zifuatazo: -

(i) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341;

(ii) Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3;

(iii) Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291;

(iv) Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura ya 132;

(v) Sheria ya Madini, Sura ya 123; na

(vi) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zimetungwa na Bunge katika nyakati tofauti zikiwa na malengo mbalimbali katika kuimarisha mifumo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hata hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wake, zimebainika changamoto na upungufu katika maeneo kadhaa ya sheria hizo ambayo imeonekana ni muhimu kuboreshwa. Hivyo, lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya sheria husika pamoja na kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa sheria hizo. Muswada huu umegawanyika katika sehemu saba.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheria hizo zinapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mawakili, Sura ya 341, ambapo Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumwongeza Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria kama Mjumbe wa Kamati ya Maadili ya Mawakili. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi katika mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, marekebisho haya ni

utekelezaji wa uamuzi uliofikiwa na Mahakama Kuu katika kesi ya madai Na. 7817 ya mwaka 2024 ya Peter Madeleka dhidi ya Kamati ya Maadili ya Mawakili na wengine watatu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka 1994 kwa lengo la kuainisha utaratibu wa utekelezaji wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba. Tangu kutungwa kwake, sheria hii imerekebishwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, Kifungu cha Tisa cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa uhiari wa wadaawa kuamua iwapo shauri lililobainika kuwa na suala la uvunjifu wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba wakati wa usikilizwaji wake katika Mahakama za chini lipelekwe Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuipa Mahakama husika mamlaka ya kuamua utaratibu sahihi unaopaswa kuzingatiwa endapo shauri litahusisha masuala ya uvunjifu wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 na 14 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayohusiana na shauri kuanza kusikilizwa na Jaji mmoja ili kubaini kama shauri hilo lina madai ya msingi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha msingi wa utoaji haki kwa kuwezesha mashauri hayo kusikilizwa moja kwa moja na kuamuliwa na jopo la majaji watatu pasipo kuhitaji uamuzi iwapo suala hilo linafaa kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka 2002 kwa ajili ya kuweka masharti ya kuanzisha na kusimamia adhabu ya kutumikia jamii. Kifungu cha Pili, Saba na 10 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa cheo cha Mratibu wa Kitaifa wa Huduma za Jamii na badala yake kuweka cheo cha Mkurugenzi wa Huduma za Uangalizi.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha masharti ya sheria kuendana na muundo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambao kwa sasa unatambua cheo cha Mkurugenzi wa Huduma za Uangalizi na sio Mratibu wa Kitaifa wa Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa wakosaji wanaoweza kupata fursa ya kutumikia adhabu kwa kufanya kazi za jamii kwa wafungwa waliohukumiwa kwenda jela kutoka muda usiozidi miaka mitatu na kuwa miaka minne. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza mlundikano wa wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hicho pia kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa sharti la mashauriano kati ya Mahakama na Kamati ya Huduma za Kijamii na badala yake kuweka sharti la mashauriano kati ya Mahakama na Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa kuamua kazi ya jamii ambayo itafanywa na mkosaji aliyepewa adhabu ya kufanya kazi za jamii.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Mahakama kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii mwenye ufahamu mzuri wa masuala ya kazi za kijamii zitakazotekelezwa na mkosaji.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kufutwa na Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa Kamati za Huduma za Jamii katika ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji kwa kuwa Wajumbe wa Kamati hizo pia ni Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Mchakato wa Kesi na Mabaraza ya Haki za Jinai ambazo zinafanya kazi zinazofanywa na Kamati za Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuondoa uwepo wa vyombo vinavyotekeleza majukumu yanayofanana na kupunguza gharama za uendeshaji wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo,

Sura ya 132. Sheria hii ilitungwa mwaka 1974 kwa lengo la kuanzisha Shirika la Soko la Kariakoo na kuweka majukumu, mamlaka, usimamizi na udhibiti wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, tangu kutungwa kwake, sheria hii imerekebishwa mara tatu. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto zilizojitokeza katika usimamizi wa shirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "*specified market*" ambao kwa sasa tafsiri yake inatolewa chini ya Kifungu cha 10. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia Kanuni za Uandishi wa Sheria zinazoelekeza tafsiri za maneno yote yaliyotumika zaidi ya mara moja katika sheria kuwekwa katika kifungu mahususi cha tafsiri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa ili kulipa shirika mamlaka ya kuingia mikataba. Lengo la marekebisho haya ni kuliimarisha shirika katika utendaji wake na kuliwezesha kuingia mikataba mbalimbali kama taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa majukumu ya shirika kwa kujumuisha jukumu la kuanzisha na kudumisha mfumo madhubuti wa masoko kwa kuweka mipango kwa ajili ya ununuzi, utunzaji, ufungaji, uuzaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa majukumu ya shirika ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha muundo wa bodi kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa na kubainisha taasisi watakazotoka. Vilevile, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utendaji wa bodi na shirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kufutwa ili kuendana na mapendekezo katika Kifungu cha Pili kuhusu tafsiri ya msamiati "*specified market*".

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa makosa yanayotendwa chini ya kifungu hicho, pamoja na kuweka ukomo wa juu na chini wa adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha masharti ya kifungu hicho ili kuvipa fursa vyombo vya utoaji haki kutoa adhabu inayoendana na kosa lililotendeka.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa. Masharti yanayopendekezwa yatamwezesha Meneja Mkuu wa Shirika au afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Meneja Mkuu kufifilisha makosa yanayotendeka chini ya sheria badala ya mamlaka hayo kutekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi kama inavyoelekezwa sasa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha mapato yanayotokana na ufifilishaji wa makosa kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kumwezesha Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutengeneza kanuni, kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa utaratibu wa ufifilishaji wa makosa katika sheria na kuwezesha usimamizi bora wa mapato yanayotokana na ufifilishaji wa makosa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza fedha zitakazotengwa na Bunge kuwa miongongi mwa vyanzo vya mapato ya shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha shirika kuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika, toshelevu na endelevu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu kipya cha 18(A) kinapendekezwa kuongezwa ili kuliwezesha shirika, kwa ridhaa ya

bodi, kufungua na kuendesha akaunti ya benki. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha ya shirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kulipwa posho na malipo mengine kama itakavyoamuliwa na mamlaka husika. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu unaotumika wa upangaji wa posho na stahiki za Wajumbe wa Bodi katika mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza Mapendekezo ya Marekebisho katika Sheria ya Madini Sura ya 123. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 kwa lengo la kuainisha masharti yanayohusiana na utafutaji, uchimbaji, uchakataji na uuzaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, sheria hii sasa inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza Kifungu Kipya cha 88A ili kuzipa Taasisi za Umma wajibu wa kuzuia *(withholding)* malipo ya mrabaha na ada ya ukaguzi kutoka katika fedha zinazolipwa na kampuni za ujenzi na kuwasilisha malipo hayo kwa Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa mrabaha na ada za ukaguzi katika madini ya ujenzi. Mapendekezo haya yataziba mianya inayotumika sasa katika kukwepa ulipaji wa mirabaha na ada za ukaguzi hivyo kuongeza mapato yanayotokana na madini ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, ambapo Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa na Jedwali la Tatu linapendekezwa kuongezwa ili kuboresha mafao yanayotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu kama Mkuu wa Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kudumisha hadhi ya Makatibu Wakuu Viongozi Wastaafu na kutambua mchango wao wakati wa utumishi wao kwa Serikali hata baada ya kwisha kwa muda wao wa utumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024)* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA S. JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 4) WA MWAKA 2024 *(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 4) BILL, 2024)* KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha wote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024). Naomba pia niwatakie nyote Heri ya Mwaka Mpya 2025. Ni dua yangu kwa Mwenyezi Mungu kuwa atujalie wote afya njema na nguvu za kuendelea kutekeleza majukumu yetu na kuendesha shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa

umahiri na mafanikio makubwa katika nyanja zote, ikiwemo kuboresha Sekta ya Sheria nchini. Mengi yamefanyika chini ya uongozi wake na sisi sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza Nchi kimataifa kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mhe. *Dkt.* Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mhe. *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. *Dkt.* Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, kumpongeza Mhe. Naibu Spika na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kipekee niishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Makamu wake Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mb.) pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Madini na wadau wengine wote kwa ushirikiano waliotupatia katika mchakato mzima wa kushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ninamhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ufanisi mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria nane (8) zifuatazo: -

1. Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act, Cap. 341);

2. Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3 (The Basic Rights and Duties Enforcement Act, Cap. 3);

3. Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 (The Immigration Act, Cap. 54);

4. Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291 (The Community Service Act, Cap. 291);

5. Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura ya 132 (The Kariakoo Market Corporation Act, Cap. 132);

6. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (The Land Act, Cap. 113);

7. Sheria ya Madini, Sura ya 123 (The Mining Act, Cap. 123); na

8. Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (The Public Service Act, Cap. 298).

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zimetungwa na Bunge katika nyakati tofauti zikiwa na malengo mbalimbali katika kuimarisha mifumo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa nk. Hata hivyo katika kipindi cha utekelezaji wake, zimebainika changamoto na upungufu katika maeneo kadhaa ya sheria hizo ambayo imeonekana ni muhimu kuboreshwa. Hivyo, lengo la marekebisho haya ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya Sheria husika pamoja na kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheria hizo zinapendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mawakili, Sura ya 341, ambapo kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuongeza Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria kama mjumbe wa Kamati ya Maadili ya Mawakili. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi katika mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, marekebisho haya ni utekelezaji wa uamuzi uliofikiwa na Mahakama Kuu katika kesi ya madai Na. 7817 ya mwaka 2024 ya Peter Madeleka dhidi ya Kamati ya Maadili ya Mawakili na wengine watatu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka 1994 kwa lengo la kuainisha utaratibu wa utekelezaji wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara moja. Katika Muswada huu, kifungu cha 9 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa uhiari wa wadaawa kuamua iwapo shauri lililobainika kuwa na suala la uvunjifu wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba wakati wa

usikilizwaji wake katika mahakama za chini lipelekwe Mahakama Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuipa mahakama husika mamlaka ya kuamua utaratibu sahihi unaopaswa kuzingatiwa endapo shauri litahusisha masuala ya uvunjifu wa haki za msingi na wajibu wa kikatiba. Vifungu vya 10 na 14 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayohusiana na shauri kuanza kusikilizwa na Jaji mmoja ili kubaini kama shauri hilo lina madai ya msingi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha msingi wa utoaji haki kwa kuwezesha mashauri hayo kusikilizwa moja kwa moja na kuamuliwa na jopo la majaji watatu pasipo kuhitaji uamuzi iwapo suala hilo linafaa kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291. Sheria hii ilitungwa na Bunge mwaka 2002 kwa ajili ya kuweka masharti ya kuanzisha na kusimamia adhabu ya kutumikia jamii. Kifungu cha 2, 7 na 10 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa cheo cha Mratibu wa Kitaifa wa Huduma za Jamii na badala yake kuweka cheo cha Mkurugenzi wa Huduma za Uangalizi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha masharti ya Sheria kuendana na muundo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambao kwa sasa unatambua cheo cha Mkurugenzi wa Huduma za Uangalizi na siyo Mratibu wa Kitaifa wa Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa wakosaji wanaoweza kupata fursa ya kutumikia adhabu kwa kufanya kazi za jamii kwa wafungwa waliohukumiwa kwenda jela kutoka muda usiozidi miaka mitatu na kuwa miaka minne. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza mlundikano wa wafungwa magerezani. Aidha, kifungu hicho pia kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa sharti la mashauriano kati ya mahakama na Kamati ya Huduma za Kijamii na badala yake kuweka sharti la mashauriano kati ya mahakama na afisa ustawi wa jamii wakati wa kuamua kazi ya jamii ambayo itafanywa na mkosaji aliyepewa adhabu ya kufanya kazi za jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha mahakama kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa afisa ustawi wa jamii mwenye ufahamu mzuri wa masuala ya kazi za kijamii zitakazotekelezwa na mkosaji.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kufutwa na kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa Kamati za Huduma za Jamii katika ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji kwa kuwa wajumbe wa Kamati hizo pia ni wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Mchakato wa Kesi na Mabaraza ya Haki za Jinai ambazo zinafanya kazi zinazofanywa na kamati za huduma za jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa uwepo wa vyombo vinavyotekeleza majukumu yanayofanana na kupunguza gharama za uendeshaji wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Marekebisho haya yanakusudia kutoa hadhi maalumu kwa raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania. Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati “Diaspora Tanzanite Card”, “special status” na “Tanzania non-citizen diaspora”. Lengo la marekebisho haya ni kuyafanya masharti yanayopendekezwa kuongezwa yaeleweke kwa urahisi zaidi. Aidha, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, tafsiri hizo zimeboreshwa zaidi baada ya ushauri mzuri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza masharti mapya ya ruhusa ya kuingia nchini kwa kutumia Kadi ya “Tanzanite Diaspora” na taarifa ya idhini ya kupewa Kadi hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha mmiliki wa Kadi ya Tanzanite Diaspora na mgeni ambaye ana taarifa ya kuidhinishwa kuingia ndani ya Jamhuri ya Muungano kutumia nyaraka hiyo bila kuathiri takwa la kuwa na pasipoti halali.

Mheshimiwa Spika, Sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza vifungu vya 36A, 36B, 36C, 36D na 36E kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine ambaye aliwahi kuwa raia wa Tanzania au mwenye asili ya Tanzania. Kwa mujibu wa mapendekezo katika Muswada, hadhi maalumu haitahusisha uraia wa kuasili bali inakusudiwa kutumika kwa mtu ambaye alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano au mzazi wake, babu, bibi au mzazi wa babu au

bibi yake alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano. Kwa mujibu wa vifungu vipya vinavyopendekezwa, pale ambapo mtu anapewa hadhi maalum, hadhi hiyo itamwezesha kuingia katika Jamhuri ya Muungano na kushiriki katika masuala mbalimbali ikiwemo shughuli za kijamii na kiuchumi. Aidha, hadhi maalum itaenda sambamba na kupata Kadi ya Tanzanite Diaspora ambayo itakuwa ni uthibitisho rasmi kwamba mmiliki wa kadi hiyo ana hadhi maalum. Vilevile, masharti mapya yanayopendekezwa yanaainisha masuala kuhusiana na muda wa uhalali wa Kadi ya Tanzanite Diaspora, wategemezi na masharti kuhusu utaratibu wa kufutwa kwa hadhi maalumu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza neno "Kadi". Lengo la marekebisho haya ni kuainisha adhabu kwa makosa yatakayotendwa na wamiliki wa Kadi ya Tanzanite Diaspora kama ilivyo kwa wamiliki wa visa, vibali, vyeti na hati za kusafiria vinavyotolewa chini ya Sheria. Kifungu cha 48 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Waziri kutengenezea kanuni zitakazoweka masharti mbalimbali kuhusu utaratibu wa uombaji na utoaji wa hadhi maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Aidha, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, baadhi ya masharti katika Sehemu hii yameboreshwa zaidi ili kuhakikisha utekelezaji bora wa dhana ya hadhi maalumu inayokusudiwa kuanzishwa katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura ya 132. Sheria hii ilitungwa mwaka 1974 kwa lengo la kuanzisha Shirika la Soko la Kariakoo na kuweka majukumu, mamlaka, usimamizi na udhibiti wa Shirika.Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara tatu. Kwa ujumla marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii yanalenga katika kutatua changamoto zilizojitokeza katika usimamizi wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "specified market" ambao kwa sasa tafsiri yake inatolewa chini ya kifungu cha 10. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia kanuni za uandishi wa sheria

zinazoelekeza tafsiri za maneno yote yaliyotumika zaidi ya mara moja katika Sheria kuwekwa katika kifungu mahususi cha tafsiri.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kulipa Shirika mamlaka ya kuingia mikataba. Lengo la marekebisho haya ni kuliimarisha Shirika katika utendaji wake na kuliwezesha kuingia mikataba mbalimbali kama taasisi. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa majukumu ya Shirika kwa kujumuisha jukumu la kuanzisha na kudumisha mfumo madhubuti wa masoko kwa kuweka mipango kwa ajili ya ununuzi, utunzaji, ufungaji, uuzaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa majukumu ya Shirika ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha muundo wa Bodi kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi na kubainisha taasisi watakazotoka. Vilevile, kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utendaji wa Bodi na Shirika. Kifungu cha 10 kinapendekezwa kufutwa ili kuendana na mapendekezo katika kifungu cha 2 kuhusu tafsiri ya msamiati "specified market". Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa makosa yanayotendwa chini ya kifungu hicho pamoja na kuweka ukomo wa juu na chini wa adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha masharti ya kifungu hicho ili kuvipa fursa vyombo vya utoaji haki kutoa adhabu inayoendana na kosa lillilotendeka.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuboresha masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa. Masharti yanayopendekezwa yatamwezesha Meneja Mkuu wa Shirika au afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Meneja Mkuu kufifilisha makosa yanayotendeka chini ya Sheria badala ya mamlaka hayo kutekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi kama inavyoelekezwa sasa katika Sheria. Vilevile, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha mapato yanayotokana na ufifilishaji wa makosa kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kumwezesha Waziri mwenye dhamana na tawala za mikoa na serikali za mitaa kutengeneza kanuni kwa

ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa utaratibu wa ufifilishaji wa makosa katika Sheria na kuwezesha usimamizi bora wa mapato yanayotokana na ufifilishaji wa makosa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza fedha zitakazotengwa na Bunge kuwa miongongi mwa vyanzo vya mapato ya Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuliwezesha Shirika kuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika, toshelevu na endelevu. Aidha, kifungu kipya cha 18A kinapendekezwa kuongezwa ili kuliwezesha Shirika, kwa ridhaa ya Bodi kufungua na kuendesha akaunti ya benki. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha ya Shirika. Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi kulipwa posho na malipo mengine kama itakavyoamuliwa na mamlaka husika. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu unaotumika wa upangaji wa posho na stahiki za wajumbe wa bodi katika mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ambapo kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu chini ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, mtu aliyepewa hadhi maalumu atakuwa na haki ya kumiliki ardhi kupitia utaratibu wa hati miliki maalumu isiyo ya asili itakayotolewa na Kamishna wa Ardhi. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha raia wa kigeni mwenye asili ya Tanzania kumiliki ardhi kupitia utaratibu wa kupewa hati miliki maalumu isiyo ya asili. Ardhi hiyo inaweza kupatikana kwa njia mbalimbali ikiwemo urithi au kununua. Kwa mujibu wa mapendekezo hayo, hati miliki maalumu isiyo ya asili inayopendekezwa itatolewa kwa vigezo na masharti maalumu. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, kifungu cha 20 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha masharti ya kifungu hicho na mapendekezo kuhusu raia wa kigeni mwenye hadhi maalumu kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa hati miliki maalum isiyo ya asili itakayotolewa kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu. Kwa mujibu wa marekebisho haya, hati miliki maalumu itakayotolewa kwa mtu aliyepewa hadhi maalum itakuwa ya muda usiozidi miaka thelathini na tatu. Kifungu cha 20A kinapendekezwa kuongezwa na vifungu vya 48 na 49 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kutoa na kusitisha hati miliki maalumu isiyo ya asili iliyotolewa kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 kwa lengo la kuainisha masharti yanayohusiana na utafutaji, uchimbaji, uchakataji na uuzaji wa madini. Sheria hii sasa inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 88A ili kuzipa taasisi za umma wajibu wa kuzuia (withholding) malipo ya mrabaha na ada ya ukaguzi kutoka katika fedha zinazolipwa kwa kampuni za ujenzi na kuwasilisha malipo hayo kwa Tume ya Madini. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa mrabaha na ada za ukaguzi katika madini ya ujenzi. Mapendekezo haya yataziba mianya inayotumika sasa katika kukwepa ulipaji wa mirabaha na ada za ukaguzi hivyo kuongeza mapato yanayotokana na madini ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ambapo kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa na Jedwali la Tatu linapendekezwa kuongezwa ili kuboresha mafao yanayotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu kama mkuu wa utumishi wa umma. Lengo la marekebisho haya ni kudumisha hadhi ya Makatibu Wakuu Viongozi wastaafu na kutambua mchango wao wakati wa utumishi wao kwa Serikali hata baada ya kuisha kwa muda wao wa utumishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill,

2024) na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wasilisho hilo. Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, aje awasilishe Maoni ya Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99, Kanuni ndogo ya (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No.4) Act,2024)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa 17, tarehe 8/11/2024 kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 96 (1). Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza uchambuzi wa Muswada kwa kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyoainishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Hamza Johari (Mbunge) siku ya Jumanne tarehe 14 Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 Kanuni ndogo ya pili ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni yao kwa maana ya *public hearing* kuhusu Muswada huu kwa njia ya *electronic* au kufika kwenye Kikao cha Kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 15 Januari, 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa upekee Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu; na kwa upekee ninaomba kuwashukuru wadau wafuatao: Haki Ardhi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Mtandao wa Utetezi wa Haki za Binadamu Tanzania na *TALA*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumatatu Tarehe 20, Januari, 2025 Kamati ilikutana na Serikali ili kufanya majumuisho kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada huu. Majumuisho hayo yalihusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Katiba na Sheria na Watendaji mbalimbali wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) umegawanyika katika sehemu kuu saba na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au kuondoa changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi wakati sehemu ya pili hadi sehemu ya sita…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge kule nyuma punguzeni sauti kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi wakati sehemu ya pili hadi sehemu ya saba inaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika sheria kuu zinazofanyiwa marekebisho ambazo ni Sheria ya Mawakili Sura ya 341 *(The Advocate Act Cap. 341),* Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu Sura ya 3 *(The Basic Rights and Duties Enforcement Act Cap. 3),* Sheria ya Huduma za Jamii Sura ya 291 *(The Community Service Act Cap. 291),* Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo Sura ya 132 *(The Kariakoo Market Cooperation Act Cap. 132),* Sheria ya Madini Sura ya 123 *(The Mining Act Cap. 123*) na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 *(The Public Service Act Cap. 298),* Marekebisho ya Sheria ya Wakili Sura ya 341 *(The Advocate Act Cap. 341)*

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya pili ya Muswada kuanzia Ibara ya Tatu hadi Ibara ya Nne. Ibara ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha Nne cha Sheria ya Mawakili ili kumwongeza Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria kuwa Mjumbe wa Kamati ya Taifa ya Mawakili. Sheria hiyo ilivyo sasa, Kamati ya Taifa ya Mawakili inaundwa na Wajumbe ambao ni Jaji wa Mahakama Kuu aliyechaguliwa na Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu wake au Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili aliyehuisha leseni yake kwa mujibu wa Sehemu ya Sita ya Sheria hii na aliyeteuliwa na Chama cha Mawakili Tanganyika *(TLS)* kushiriki katika Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwa kuwa yakikidhiwa na Bunge yataondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi kati ya mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo Sura ya 132 *(The Kariakoo Market Cooperation Act Cap. 132)*. Sehemu hii inahusu Ibara ya 22 hadi 32. Ibara ya 22

inalenga kuboresha usimamizi, uendeshaji na ukuaji wa Shirika la Soko la Kariakoo ili kukabiliana na changamoto za kisasa katika masoko ya kifaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, maelezo yanayofuata kuhusu sehemu hii ya Muswada ni kama yalivyowakilishwa na mtoa hoja kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 inalenga kuboresha masharti yanayohusu mafao na marupurupu kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu. Marekebisho hayo yanahakikisha kuwa, viongozi hawa wanapewa heshima na uangalizi stahiki baada ya kustaafu. Lengo ni kuhakikisha kuwa, marekebisho haya yanaunganishwa rasmi na Sheria ya Utumishi wa Umma kwa utekelezaji bora.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 43 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 24 ili kuongeza mafao, marupurupu na huduma zinazotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu. Masharti hayo mapya ni: -

a) Pasipoti ya Kidiplomasia;

b) Huduma za matibabu kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu na Familia yake;

c) Huduma za usalama nyumbani na anaposafiri;

d) Posho za kujikimu wanapokuwa safarini kwa shughuli za Umma.

Mheshimiwa Spika, marupurupu haya yatadumu kwa maisha yake yote isipokuwa sheria itakavyoelekeza vinginevyo. Aidha, kifungu kinaweka masharti kuwa, Serikali itawajibika kugharamia huduma hizo kupitia Wizara ya Fedha au taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho ni kuheshimu nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuwapa viongozi hawa waandamizi wa Serikali hadhi na marupurupu yanayolingana na nyadhifa walizozitumikia. Vilevile kuimarisha ustawi wa viongozi wastaafu na

kuweka motisha kwa viongozi wa sasa kufanya kazi kwa bidii wakijua kwamba, Serikali itathamini hata baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 44 inarekebishwa kwa kuongezwa jedwali la tatu mara baada ya jedwali la pili ili kuboresha mafao yanayotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu kama Mkuu wa Utumishi wa Umma na hudumisha hadhi ya Makatibu Wakuu viongozi Wastaafu na kutambua mchango wao wakati wa utumishi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; Maoni ya jumla. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Muswada kama yalivyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha, kama ulivyofafanuliwa katika aya zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja, Marekebisho ya Sheria ya Wakili Sura 341. Kwenye Ibara ya Nne ya Muswada, Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ili Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria asiwe Mjumbe wa Kamati ya Taifa ya Mawakili, badala yake aongezwe wakili mwingine kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika *(TLS)* kwa kuwa Chama cha Mawakili Tanganyika ni sekta binafsi, hivyo ni muhimu kuongeza uwakilishi kutoka Chama cha Mawakili badala ya Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati imeridhia maboresho yabaki kama yalivyo ili kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi katika mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwenye sehemu ya marekebisho ya Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura 132. Kwenye Ibara ya 26, Kamati ilipendekeza Wajumbe wanaounda Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Soko la Kariakoo wanaowakilisha Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam na Wafanyabiashara wa Jumuiya ya Soko la Kariakoo, wasiwekewe vigezo maalum vya

wao kuwa Wajumbe. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 29, Kamati ilikuwa na maoni kuwa Ibara ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno "*not exceeding two thirds*" na badala yake ibaki "*two thirds*" ili kuepusha matumizi mabaya ya madaraka. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu inahusu Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 *(The Mining Act [Cap. 123])*. Kwenye Ibara ya 41, Kamati ilikuwa na maoni ya jumla kwamba, marekebisho haya yanayolenga kuiwezesha Serikali kupata mapato kupitia madini ya ujenzi yasibakie katika taasisi za umma pekee. Hivyo, Serikali na taasisi zake iendelee kufanya utafiti wa namna bora ambayo itawezesha Serikali kupata mapato zaidi kupitia sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kujadili na kuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika shughuli hii, naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Bunge kama yalivyowasilishwa kwenye meza yako.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa kwa karibu na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo mmeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati yetu ya kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini kwa

ushirikiano mkubwa waliotupatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali - *CPD*, Ndugu Honorius Njole kwa kuandaa Muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika sheria wakati wa zoezi la urekebu linaloendelea. Aidha, Kamati inawashukuru pia kwa ushirikiano waliyoipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru pia Watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wote kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa sheria zilizopendekezwa kurekebishwa, kwa ushirikiano waliotupatia Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa upekee, naishukuru Sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada huu na kukamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendments] (No. 4), Act, 2024)* pamoja na marekebisho yake kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NAMBA 4 WA MWAKA 2024 (*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 4) ACT, 2024*) - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Muswada Wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 Wa Mwaka 2024 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2024*).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Kumi na Saba, tarehe 8 Novemba, 2024 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 96 (1)**. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 136 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Mhe. Hamza Johari (Mb.), siku ya Jumanne tarehe 14 Januari, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni *(Public Hearing)* kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielekroniki au kufika kwenye kikao cha kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 15 Januari, 2025. Kwa upekee Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu, na kwa upekee ninaomba kuwashukuru wadau wafuatao: -

1. Haki Ardhi;
2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
3. Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (**THRDC**); na
4. TALA.

Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Siku ya Jumatatu tarehe 20 Januari, 2025 Kamati ilikutana na Serikali ilikufanya majumuisho kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada huu. Majumuisho hayo yalifanyika kwa kumuhusisha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria na watendaji mbalimbali wa taasisi za Serikali zinazohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati alimjulisha Mheshimiwa Spika.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada Wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2024*) ukiwa umegawanyika katika sehemu Kuu Tisa (9) na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Nane (8) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kuondoa changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Nane zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika Sheria kuu zinazofanyiwa marekebisho ambazo ni kama zifuatazo:-

a) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act, (Cap. 341)).
b) Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura ya 3 (The Basic Rights and Duties Enforcement Act, (Cap. 3) ).
c) Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291 (The Community Service Act, (Cap. 291)).
d) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 (The Immigration Act, (Cap. 54)).
e) Sheria ya Shirika la soko la Kariakoo, Sura ya 132 (The Kariakoo Market Corporation Act, (Cap. 132))
f) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (The Land Act, (Cap. 113))
g) Sheria ya Madini, Sura ya 123 (The Mining Act, (Cap. 123)); na
h) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (The Public Service Act, (Cap. 298)).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2024*) unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria nilizozitaja kwa lengo la kuondoa mapungufu mbalimbali yaliyobainika wakati wa zoezi la utekelezaji wa Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya uchambuzi na upembuzi yakinifu kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya uchambuzi huo pamoja na majumuisho yaliyofanyika baina ya Kamati na Serikali, Kamati hii kama ilivyokuwa kwa wadau mbalimbali, inakubaliana kwa

sehemu kubwa na mapendekezo ya Muswada huu. Aidha, uchambuzi kuhusu maudhui ya Sheria zinazorekebishwa ni kama ifuatavyo: -

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

### 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria tano kati ya sheria Nane zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hizo ambazo kamati ilizibaini kuwa na mapungufu ni pamoja na Sheria ya Mawakili, Sura ya 341, Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54, Sheria ya Shirika la soko la Kariakoo, Sura ya 132, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113a n Sheria ya Madini, Sura ya 123.

### 2.3 Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act (Cap. 341))

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Pili ya Muswada kuanzia **Ibara ya 3** hadi **Ibara ya 4**. Ibara ya 3 inaweka sharti kuwa sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 wakati Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha **Kifungu cha 4** cha Sheria ya Mawakili ili kumuongeza Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria kuwa Mjumbe wa Kamati ya Taifa ya Mawakili.

Sheria ilivyo sasa, Kamati ya Taifa ya Mawakili inaundwa na wajumbe ambao ni Jaji wa Mahakama Kuu aliyechaguliwa na Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu wake au Mkurugenzi wa Mashitaka, Wakili aliyehuisha Leseni yake kwa

mujibu wa sehemu ya Sita (VI) ya Sheria hii na aliyeteuliwa na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kushiriki katika Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho kwa kuwa yakiridhiwa na Bunge yataondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi katika mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 2.4 Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 *(The Immigration Act, (Cap. 54)*

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Tano** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 16** hadi **Ibara ya 21**. Ibara ya 17 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 kwa kuongeza tafsiri za maneno "*Diaspora Tanzanite Card"* ambayo ni kadi maalum inayotolewa kwa Raia wasiokuwa wa Tanzania wenye asili ya Tanzania waishio ughaibuni.

Vilevile, tafsiri ya maneno "*Special Status*" *kumaanisha* hadhi maalum inayotolewa kwa watu wenye asili ya Tanzania wasio raia wa Tanzania ili kuwawezesha kuingia, kukaa au kutoka nchini kwa masharti yoyote yatakayowekwa na Sheria zinginezo na tafsiri ya maneno "*Tanzania non-citizen Diaspora*" kuwa ni mtu aliyekuwa raia wa Tanzania au mwenye mzazi, babu, au bibi aliyekuwa raia wa Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kuweka wazi na kuwezesha utekelezaji wa masharti mapya yanayowahusu watu wenye asili ya Tanzania wanaoishi nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 28 kwa kuongeza masharti mapya ya kuingia Nchini kwa kutumia "*Diaspora Tanzanite Card*" au taarifa ya kusajiliwa kwenye rejesta kwa ajili ya kupatiwa kadi ya Tanzanite. Lengo ni kutoa fursa kwa watu wenye asili ya Tanzania waishio ughaibuni kuingia nchini kwa urahisi bila kuathiri mahitaji ya kuwa na pasipoti ya nchi zao.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 19 inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 36A hadi 36E, vinavyolenga kuanzisha *Diaspora Tanzanite Card* na masharti ya hadhi maalum kwa watu wenye

asili ya Tanzania waishio ughaibuni. Aidha, vifungu hivi vinatoa taratibu za kisheria kuhusu namna ya kupata hadhi hii, haki na wajibu wa aliyepewa, pamoja na masharti ya kufutwa kwa hadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Marekebisho yanaweka sharti la Kufutwa kwa hadhi maalumu kwa mtu atakayekiuka misingi iliyowekwa kwenye sheria na mtu aliyekuwa na kadi hiyo atatakiwa kuirudisha kwa mamlaka iliyotoa kadi hiyo. Vilevile, mtu aliyefutiwa hadhi hiyo, anaweza tena kuomba kwa mamlaka baada ya kipindi cha mwezi mmoja kupita na maombi hayo yatashughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Uhamiaji. Lengo ni kuzuia matumizi mabaya ya hadhi maalum na kulinda maslahi ya taifa kwa kuhakikisha watu wenye hadhi maaalum hawashiriki vitendo vya kuhatarisha usalama wa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 20 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 45(1) ili kuongeza masharti ya *Diaspora Tanzanite Card* kwenye masharti yaliyokuwepo hapo awali yanayohusu masharti ya kisheria kwa wamiliki wa Visa, vibali, au vyeti vilivyotolewa chini ya Sheria ya Uhamiaji. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa masharti ya kifungu cha 45 kwa kuongeza *card* za diáspora kwenye orodha ya hati zinazosimamiwa na kudhibitiwa na Sheria ya Uhamiaji. Vilevile kadi hii itahusika na masharti yanayohusu maombi, uhalali, na hatua za kinidhamu kwa wamiliki wake. Lakini pia, marekebisho haya yatawezesha mamlaka kufuatilia matumizi na uhalali wa kadi hii kwa mujibu wa sheria sawa na vyeti na Visa zingine ili kupunguza uwezekano wa ukiukwaji wa sheria kwa maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 21 inapendekeza kuongeza masharti katika kifungu cha 48 (1) hususan aya mpya ya (q) kuhusu Waziri kutengeneza kanuni za kueleza taratibu za maombi na utoaji wa hadhi maalum. Lengo la marekebisho haya ni kufafanua mchakato wa maombi, utoaji na ufuatiliaji wa hadhi maalum kupitia kanuni, aidha, kuwezesha mamlaka husika (waziri) kutunga kanuni zinazowiana na masharti ya sheria na kupunguza tafsiri potofu na migogoro ya utekelezaji wa masharti yanayohusu hadhi maalumu

### 2.5 Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura ya 132 *(The Kariakoo Market Corporation Act, Cap 132)*

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu ibara za 22 hadi 32. Ibara ya 22 inaeleza kuwa sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Kariakoo, Sura ya 132. Sehemu hii inalenga kuboresha usimamizi, uendeshaji, na ukuaji wa Shirika la Soko la Kariakoo ili kukabiliana na changamoto za kisasa katika masoko ya kitaifa na kimataifa. Marekebisho yanahusisha vifungu mbalimbali vinavyoboresha mamlaka, majukumu, na utendaji wa Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 23 inapendekeza Marekebisho ya Kifungu cha 2 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "*specified market*" ili kumaanisha Soko la Kariakoo pamoja na masoko mengine yanayosimamiwa na Shirika. Lengo ni Kuongeza mamlaka ya Shirika kushughulikia masoko mengine zaidi ya Kariakoo pekee na kuboresha uwezo wa Shirika katika usimamizi wa masoko mengine yanayohitaji uangalizi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 24 inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 3 kwa kuongeza aya (e) ambayo inayoliongezea Shirika uwezo wa kuingia kwenye mikataba au shughuli nyingine za kibiashara kama Taasisi huru. Lengo ni Kulipa Shirika mamlaka ya kisheria ya kujitegemea katika kufanya maamuzi ya kibiashara yanayoweza kulisaidia kiuchumi na kuliwezesha Shirika kushirikiana na wadau wa biashara kitaifa na kimataifa. Aidha, aya zilizokuwa (b), na (c) zinapangwa upya na kuwa (c), na (d) mtawalia.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 25 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4(1) kwa kuongeza kazi za Shirika na kujumuisha-

(a) Kuanzisha na kudumisha mfumo bora wa masoko.
(b) Kutoa huduma za ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi na usindikaji wa bidhaa.

Aidha, Ibara inakusudia kuongeza aya mpya ili kuboresha ufanisi wa Shirika katika shughuli za soko. Lengo ni kuimarisha jukumu la Shirika katika kudhibiti masoko na kuwezesha biashara ndani na

nje ya Tanzania. Pia, kuboresha huduma kwa wafanyabiashara na wateja wa masoko yanayosimamiwa na Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 26 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 5 kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi, na uteuzi wao sasa utazingatia uwakilishi wa sekta muhimu, ikiwemo Wizara za Serikali, Baraza la Biashara, na jamii ya wafanyabiashara. Aidha, Ibara inaweka masharti kuwa Meneja Mkuu wa Shirika atakuwa Katibu wa Bodi, na Bodi inaweza kualika washauri wa kitaalamu kuhudhuria vikao lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Lengo ni kupunguza gharama za uendeshaji wa Bodi, kuimarisha uwakilishi wa kitaalamu katika maamuzi ya Bodi na kuwezesha Bodi kufanya maamuzi bora kwa ushauri wa wataalamu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 27 inapendekeza kufuta Kifungu cha 10 kwa kuwa maudhui yake yamewekwa katika Ibara ya 23 inayohusu tafsiri ya *specified markets*. Lengo ni kupunguza urudiaji wa masharti na kuboresha uwazi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 28 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 15 kwa kuongeza faini/adhabu kwa makosa yanayohusiana na Sheria ya Kariakoo kutoka faini ya shilingi elfu tano hadi kati ya shilingi laki mbili na milioni moja, au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na usichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja. Lengo ni kuimarisha uzingatiaji wa sheria kwa kutoa adhabu kali zinazolingana na uzito wa makosa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 29 inapendekeza kufuta na kuandika upya Kifungu cha 16 ili kumpatia Meneja Mkuu wa Shirika mamlaka ya kufifilisha makosa chini ya Sheria hii. Utaratibu wa utoaji fomu na namna ya kufififlisha utawekwa kwa mujibu wa Kanuni. Aidha, fedha zilizokusanywa kutoka kwenye adhabu hizi zitaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa uamuzi wa Waziri husika.

Aidha, Ibara inaweka sharti la kutoa taarifa ya ufifilishaji wa makosa hayo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Lengo ni kuwezesha

utekelezaji wa haraka wa masharti ya sheria na kudhibiti mapato yanayopatikana kutokana na makosa

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 30 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 17 kwa kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato vya Shirika kwa kujumuisha misaada, michango, na mapato kutoka uwekezaji wa Shirika. Lengo ni Kuhakikisha Shirika lina mapato endelevu na ya kutosha kugharamia shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 31 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 18A ili kulipatia Shirika uwezo wa kufungua na kusimamia akaunti ya benki kwa ridhaa ya Bodi. Lengo ni kuleta uwazi na uwajibikaji wa kifedha katika Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 32 inapendekeza kufuta kifungu cha 24 na kukiandika upya ili kuainisha masharti mapya kuhusu posho na malipo kwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika. Masharti hayo yanahusu wajumbe wa Bodi kulipwa posho na malipo kutoka kwenye fedha za Shirika kwa kiwango kitakachoamuliwa na mamlaka inayohusika na masuala ya fedha au malipo katika taasisi za umma. Lengo la marekebisho ni kuimarisha uwajibikaji wa kifedha kwa kuweka mfumo rasmi wa malipo kwa wajumbe wa Bodi ili kuzuia matumizi holela ya rasilimali za Shirika. Vilevile, kuhakikisha posho na malipo yanaendana na viwango vya kawaida vinavyotumika katika Mashirika ya Umma.

## 2.6 Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (*The Land Act, Act, Cap. 113)*

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusu Ibara ya 33 na Ibara ya 39. Ibara ya 33 inaeleza kuwa, Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Aidha, kwa ujumla, Sehemu hii inalenga kuboresha Sheria ya Ardhi kwa kushughulikia masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi kwa watu wasio raia wa Tanzania ila wana asili ya Tanzania waishio ughaibuni waliopata hadhi maalum *(special status)*. Pia, inatoa mfumo wa umiliki wa ardhi kwa njia maalum kwa watu na mashirika yanayohusiana na *Diaspora Tanzanite Card*.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 34 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 kwa kuongeza tafsiri ya neno jipya "*special derivative right*" ambalo litamaanisha haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa mujibu wa masharti maalum yaliyotolewa na Kamishna wa Ardhi, ikiwemo:

(a) Kupangisha ardhi *(lease);*
(b) Kupangisha ardhi ndogo *(sub-lease)*;
(c) Kupata leseni ya matumizi ya ardhi *(licence)*;
(d) Haki ya matumizi *(usufructuary right)*; na
(e) Haki nyingine zinazofanana na hizo.

Lengo ni kuweka msingi wa kisheria kwa haki hiyo ya umiliki (*special derivative right)*, ambayo ni aina mpya ya umiliki wa ardhi kwa Watanzania waishio ughaibuni waliopata hadhi maalumu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 35 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 19 kwa kuongeza kifungu kipya cha 19(1A) ambacho kinaweka masharti kwamba mtu mwenye kadi ya *Diaspora* au shirika linalomilikiwa na watu wenye kadi hii linaweza kupewa *special derivative right*. Hata hivyo, mashirika haya lazima yawe na wanahisa wachache *(minority shareholders)* ambao ni raia wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara hii pia inaongezea aya (d) katika Kifungu cha 19(2) ili kutoa haki ya kumiliki ardhi kwa mtu mwenye *Diaspora Tanzanite Card* kupitia *special derivative right*. Aidha, utaratibu wa maombi utaelezwa kwenye kanuni. Lengo ni kuwapa watu wenye asili ya Tanzania wasio raia waishio ughaibuni nafasi ya kumiliki ardhi kwa masharti maalum, huku wakizingatia usalama na maslahi ya taifa kwa kuhakikisha kwamba raia wa kawaida wa Tanzania wanashiriki katika umiliki wa mashirika yenye ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 36 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 20A Kinachoweka masharti ya umiliki wa *special derivative right* kwa mtu mwenye hadhi maalum. Aidha, haki hii inatumika tu kwenye ardhi ya kawaida *(general land)*. Vilevile, masharti na taratibu zinazotumika kwenye leseni za kawaida za

ardhi zitatumika pia kwenye haki hii kwa mabadiliko madogo. Aidha, haki hii itaisha ikiwa hadhi maalum ya mmiliki itafutwa chini ya Sheria ya Uhamiaji. Lengo ni Kuweka mfumo wa wazi wa kisheria kwa umiliki wa ardhi kwa masharti maalum ili kuimarisha uwajibikaji na urahisi wa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 37 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 32 kwa kuongeza aya mpya(d) inayohusu muda wa umiliki wa *special derivative right* kuwa ni muda wa hadi miaka 33. Lengo ni kuweka kikomo cha muda wa umiliki wa ardhi kwa masharti maalum ili kuhakikisha kwamba matumizi ya ardhi yanaendelea kufuatiliwa mara kwa mara na mamlaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 38 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 48 kwa kumtaka Kamishna wa Ardhi kutoa mapendekezo kwa Waziri pale anapotaka kufuta *special derivative right* badala ya Rais. Lengo ni Kupunguza mzigo wa maamuzi kwenye ngazi ya juu ya Serikali na kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 39 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 49 kwa kuongeza maneno "au Waziri" ili kutoa mamlaka kwa Waziri kufanya uamuzi wa kufuta *special derivative right*. Lengo ni kuharakisha mchakato wa uamuzi kuhusu haki za umiliki wa ardhi kwa wale waliopoteza hadhi maalum au waliokiuka masharti ya umiliki.

## 2.7 Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 *(The Mining Act, Cap 123)*

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusu Ibara ya 42 na Ibara ya 44. Ibara ya 42 inaeleza kuwa, sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Sehemu hii inalenga kuboresha masharti yanayohusu mafao, marupurupu, kwa Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu.

Marekebisho haya yanahakikisha kuwa viongozi hawa wanapewa heshima na uangalizi stahiki baada ya kustaafu.

Lengo ni kuhakikisha kuwa marekebisho haya yanaunganishwa rasmi na Sheria ya Utumishi wa Umma kwa utekelezaji bora.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 43 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 26 ili kuongeza mafao, marupurupu, na huduma zinazotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu. Masharti haya mapya ni-

(a) Pasipoti ya Kidiplomasia;
(b) Huduma za matibabu kwa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu na familia yake;
(c) Huduma za usalama nyumbani na anaposafiri; na
(d) Posho za kujikimu anapokuwa safarini kwa shughuli za Umma.

Marupurupu haya yatadumu kwa maisha yake yote isipokuwa sheria itakavyoelekeza vinginevyo. Aidha, kifungu kinaweka Masharti kuwa, Serikali itawajibika kugharamia huduma hizi kupitia Wizara ya Fedha au taasisi husika. Lengo la Marekebisho ni kuheshimu nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuwapa viongozi hawa waandamizi wa serikali hadhi na marupurupu yanayolingana na nyadhifa walizozitumikia. Vilevile, kuimarisha Ustawi wa Viongozi Wastaafu na Kuweka motisha kwa viongozi wa sasa kufanya kazi kwa bidii, wakijua kuwa serikali itawathamini hata baada ya kustaafu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 44 inarekebishwa kwa kuongezwa jedwali la tatu mara baada ya jedwali la pili ili kuboresha mafao yanayotolewa kwa Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu kama mkuu wa utumishi wa umma na kudumisha hadhi ya Makatibu Wakuu Viongozi wastaafu na kutambua mchango wao wakati wa utumishi wao kwa Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata:

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 *(The Advocates Act (Cap. 341))*

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 4 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ili Katibu Mtendaji wa Tume ya kurekebisha Sheria asiwe Mjumbe wa Kamati ya Taifa ya Mawakili badala yake aongezwe wakili mwingine kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika *(TLS)* kwa kuwa Chama cha Mawakili Tanganyika ni Sekta binafsi hivyo ni muhimu kuongeza uwakilishi kutoka Chama cha Mawakili (TLS) badala ya Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na majadiliano yaliyofanyika kati ya Kamati na Serikali, Kamati imeridhia maboresho yabaki kama yalivyo ili kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa maslahi katika mazingira ambayo mlalamikaji ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 *(The Immigration Act, (Cap. 54)*

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 17 ya Muswada Kamati iliomba kupata ufafanuzi wa mantiki wa aya "b" kwa kuwa maneno yaliyotumika ni ya jumla, mfano maneno *"other purposes"* hivyo kuleta mkanganyiko katika kutafsiri maudhui yake. Pia, Kamati ilishauri Marekebisho yaongeze maneno *"by birth pursuance to section 4 of the Tanzanian citizenship Act"* mwishoni mwa tafsiri ya "Tanzania Non-Citizen" ili Kuondoa dhana

ya kuhusisha raia ambao wamepata uraia kwa njia ya *Registration* (maombi) kwa watu wanaohusiana na Tanzania *non-citizen Diaspora* na kuweka wigo wa uraia wao na Kufuta maneno" *or such other descendant or*" ili Kuweka wigo wa uhusiano kwa kigezo cha kupewa Hadhi Maalum.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 19 Kamati ilishauri Kifungu kipya cha 36A(2) Kiweke kigezo cha uchumi katika kutoa Hadhi maalum Ili kuhakikisha kuwa *Diaspora* wanachangia Uchumi wa nchi kupitia Uwekezaji na Kifungu kipya cha 36A(3) kirekebishwe kwa kuongeza maneno "in collaboration with the ministry of Foreign Affairs" ili Kuweka masharti ya ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Mambo ya Nje kwa masuala yanayohusu mambo ya nje. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kifungu kipya cha 36B Kamati ilishauri Uhuishaji wa Kadi ya Tanzanite uendane na kigezo cha Uthibitisho wa Uwekezaji uliofanywa na mtu aliyepewa kadi ya Tanzanite ili Kuhakikisha kuwa Diaspora wanachangia Uchumi wa nchi kupitia Uwekezaji.

Aidha, kifungu cha 36D(c) Serikali itoe ufafanuzi kuhusu suala la "morals of United Republic", kama ni muhimu kuorodheshwa katika kifungu hiki

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na maoni kuwa, kuorodhesha masuala ya good moral standing inaweza kupelekea kuacha baadhi ya masharti/vigezo vingine muhimu hivyo kuminya wigo wa udhibiti na kwa kuwa maadui hawajulikani ni vyema maadui hao wakatajwa wazi kama ambavyo ilibainishwa wazi katika Sheria au kipengele hicho kifutwe ili kuondoa utata kuhusu tafsiri wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo Na katika Kifungu cha 36E (2) Kamati iliomba ufafanuzi kuhusu ulazima wa diaspora aliyefutiwa

hadhi maalumu kurejesha kadi hiyo kwenye mamlaka kwa kuwa mfumo hauitambui.

Aidha, Serikali itoe ufafanuzi kuhusu masharti ya kifungu cha 36E (3)- yanayotoa nafuu kwa mtu aliyefutiwa Hadhi Maalum (*special status*) kwa kuomba hadhi ya aina nyingine; pia Kamati ilihoji kuhusu uhalali wa mali za mtu aliyefutiwa hadhi maalum au kufariki kwa kuwa hakuna kifungu katika Muswada au Sheria inayorekebishwa kinachoelezea haki hizo.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa, Sheria iweke Kifungu cha Sheria ambacho kitaongelea uhalali wa mali za mtu ambaye atafutiwa hadhi maalum au kufariki akiwa na hadhi maalum

**Maoni ya Jumla kuhusu Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54**

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itafute namna ambayo itaanzisha chombo maalum kitakachoanzishwa na kupewa mamlaka na Sheria ya kusimamia na kuratibu masuala ya Diaspora badala ya masuala hayo kusimamiwa na idara au taasisi tofauti za serikali kama ilivyo kwa nchi nyingi ambazo zina mfumo wa Kuwatambua Diaspora wa Nchi zao.

**3.4 Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo, Sura ya 132 *(The Kariakoo Market Corporation Act, Cap 132)***

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 26 Kamati ilipendekeza wajumbe wanaounda Bodi ya wakurugenzi wa Shirika la Soko la Kariakoo, wanaowakilisha manispaa ya jiji la DSM na wafanyabiashara wa jumuiya ya soko la Kariakoo wasiwekewe vigezo maalumu vya wao kuwa wajumbe.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.
**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 29 Kamati ilikuwa na maoni kuwa, Ibara ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno "*Not exceeding two thirds*" na badala yake ibaki "*two thirds*" ili kuepusha matumizi mabaya ya Madaraka. Tunaipongeza Serikali

kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.5 Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (*The Land Act, Act, Cap. 113)*

**Mheshimiwa Spika**, Kwenye Ibara ya 35 Kamati ilikuwa na maoni kuwa kama Marekebisho ni kwa ajili ya *Diaspora, Derivative right* isiguse Mashirika ambayo Sheria haijayazungumzia, lengo ni Kusaidia sheria kueleweka na kurahisisha utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Ardhi kinaweka masharti kuhusu aina ya umiliki wa Ardhi kwa raia (Citizens), ambao ni wa namna mbili (rejea kifungu husika). Kifungu cha 19 (2) kinatoa masharti ya Mtu ambaye siyo raia, au kampuni ya kigeni kuwa atamiliki ardhi kupitia sheria ya "The Tanzania Investment Act Cap 38".

**Aidha,** Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ardhi kinaweka Masharti ya mtu asiye raia (non-citizen) kumiliki ardhi. Hivyo; Kutambulisha "*Special status*" katika kifungu cha 19 cha Sheria ya ardhi kunaleta mkanganyiko, kwani *Special Status* inatolewa kwa mtu ambaye siyo raia *(Non-Citizen)*.

**Mheshimiwa Spika;** Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali na Taasisi zinazohusika kusimamia Sheria hii zihakikishe kwamba zinasimamia ipasavyo na kujali maslahi mapana na ustawi wa watanzania kama ilivyobainishwa kwenye Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### 3.6 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kwa ujumla wake kufanya maboresho ya vifungu kwenye Ibara ya 34, 37, 38, na 39 kwa kuweka ukomo wa juu wa vizazi wa kuwatambua Tanzania Non-Citizen Diaspora, ili kulinda maslahi ya Watanzania na Diaspora wasio raia wa Tanzania. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka usimamizi Madhubuti wa Diaspora wasio raia wa Tanzania

kwa kumpatia Kamishina wa Ardhi mamlaka ya kutoa hati maalum hafifu badala ya mamlaka hayo kupewa Waziri.

### 3.7 Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 *(The Mining Act, Cap 123)*

**Mheshimiwa Spika**, kwenye Ibara ya 41 Kamati ilikuwa maoni ya jumla kwamba Marekebisho haya yanayolenga kuiwezesha Serikali kupata mapato kupitia Madini ya ujenzi yasibakie katika Taasisi za Umma,na Hivyo Serikali na Taasisi zake iendelee kufanya utafiti na namna bora ambayo itawezesha Serikali kupata mapato zaidi kupitia sekta ya Madini.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo,Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe

14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe
20. Suma Ikenda Fyandomo - Mjumbe
21. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (Mb.), na Naibu Waziri wake Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.) kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Mhe. Hamza Johari (Mb.), akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali ***(CPD)*** Ndg. Onorius Njole kwa kuandaa Muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika Sheria wakati wa zoezi la urekebu lialoendelea. Aidha, Kamati inawashukuru pia kwa ushirikiano walioipatia kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati inawashukuru pia watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wote kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii; na kwa upekee niishukuru

sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Act, 2024*)** Pamoja na Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.

**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria**

29Januari, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa wasilisho hilo la maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina ya Wabunge hapa ambao wameomba kuchangia hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi. Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia katika Sehemu ya Nne ya Muswada huu inayopelekea marekebisho ya Sheria ya Huduma za Jamii, Sura Na. 291 iliyoweka masharti ya kuanzisha na kusimamia kifungo cha jamii.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kuwatambua Maafisa Ustawi wa Jamii kupitia marekebisho haya

ya sheria, ambapo sasa Kifungu cha Tatu kinapendekeza yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba, wafungwa waliohukumiwa kwenda jela kwa muda usiozidi miaka minne, wapate fursa ya kutumikia kifungo kwa kufanya kazi za kijamii. Mabadiliko haya ni ya msingi sana kwa sababu yatapelekea kupunguza msongamano na mlundikano wa wafungwa kwenye Magereza yetu, jambo ambalo litachangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha afya miongoni mwa wafungwa hawa. Pia, kubwa zaidi itapunguzia Serikali mzigo mkubwa ilionao katika kuwahudumia wafungwa hawa ikiwemo eneo la bili kubwa ya Serikali kila mwezi ya chakula kwa ajili ya wafungwa na mahabusu kwenye Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kwamba, kifungu hiki cha Tatu, sasa kinaweka sharti la mashauriano kati ya Mahakama na Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa kuamua kazi ya jamii ambayo itafanywa na mfungwa aliyehukumiwa kutumikia kifungo cha kufanya kazi za kijamii.

Mheshimiwa Spika, utambuzi huu kwa Maafisa Ustawi wa Jamii wetu ni jambo la msingi sana na ni jambo la kuipongeza Serikali. Hivyo, kwa dhati kabisa naendelea kuipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Maafisa Ustawi wa Jamii, kwa sababu ni ukweli usiopingika, kwa muda mrefu sana tumekuwa tukichanganya kati ya Afisa Ustawi wa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii, wakati hawa wana taaluma mbili tofauti na taaluma ya Afisa Ustawi wa Jamii ni taaluma muhimu sana hususani katika mazingira tuliyonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Serikali imewatambua Maafisa Ustawi wa Jamii hadi kuweka sharti kwamba wao ndiyo ambao watakaa kujadiliana na Mahakama ili kuamua kazi za kijamii zitakazofanywa na wafungwa ambao wamepewa kifungo hiki cha kufanya kazi za kijamii, hivyo ninatumia fursa hiyo, kutokana na utambuzi huo wa Serikali, basi ninaishauri Serikali mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ili Maafisa Ustawi hawa waweze kutekeleza majukumu yao ya sasa pamoja na jukumu hili jipya, basi ni dhahiri na ni muhimu sana Serikali iweze kuwatengea bajeti Maafisa Ustawi wa Jamii pia Serikali iweze kuwapa vitendea kazi hawa Maafisa Ustawi wa Jamii, maana kinyume na hapo hawataweza kutekeleza jukumu hili kubwa na muhimu ambalo wamepewa pamoja na kuimarisha ufanisi wa majukumu yao ya sasa. Kwa hiyo, ninasisitiza sana Serikali iwape bajeti pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kwamba, pale ambapo Jeshi la Polisi linakwenda kukamata wahalifu, ninatambua kwamba kama katika kaya ile pengine kuna watoto, huwa anakwenda na askari mwanamke, lakini kutokana na utambuzi huo wa Maafisa Ustawi wa Jamii, ndani ya marekebisho haya ya sheria, basi napendekeza kwa Serikali pale ambapo Jeshi la Polisi linakwenda kukamata wahalifu awepo pia Afisa Ustawi wa Jamii kwa sababu yeye ndiye analo jukumu la kuhakikisha ustawi na usalama wa watoto.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, ninatambua kwamba ipo ramani ambayo inaelekeza katika vituo vyetu vya Polisi, dawati la jinsia na watoto linapaswa liwe ni jengo ambalo lina vyumba vinne ili Maafisa Ustawi wa Jamii kwenye vituo vyetu vya Polisi waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa faragha inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapendekeza pia kwa Serikali, kwa kutambua hawa Maafisa Ustawi wa Jamii, basi Serikali ione namna ambavyo itaweza kutenga bajeti na namna ambavyo katika vituo vipya vyote vya Polisi ambavyo Serikali inajenga ihakikishe kwamba kunakuwa kuna jengo mahsusi kwa ajili ya dawati la jinsia na watoto ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba pia niishauri Serikali kuangalia namna ambavyo wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia, ubakaji na ulawiti, wanavyoweza wakapewa msamaha wa gharama za matibabu. Jambo hili ni la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, pia, kwa kuwa katika eneo hili tumetambua nafasi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika kuelekeza namna ambavyo wale wafungwa ambao watakwenda kufanya kazi za kijamii, lakini kwa upande mwingine tunatambua pia wafungwa ambao wako kwenye Magereza zipo gharama zao za matibabu ambazo zinagharamiwa na Serikali. Basi kwa msingi huo huo, Serikali ione pia namna ya kutoa msamaha wa gharama za matibabu kwa wahanga wa matukio ya ubakaji na ulawiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Maafisa Ustawi wa Jamii wanalo jukumu kubwa la kujenga na kuimarisha maadili hususan maadili ya watoto, basi Serikali ije na mpango madhubuti wa kujenga shule za maadilisho kwa ajili ya watoto ambao wanakuwa wamefanya makosa ya kijinai. Kwa kufanya hivyo tutaweza kujenga watoto wetu na kuwapa ile nafasi ya pili katika maisha yao ili waweze kuwa wananchi bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kutambua Maafisa Ustawi wa Jamii na ninatumia fursa hii kipekee kumpongeza sana Afisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wetu, Mkoa wa Kagera, anaitwa Rebeca pamoja na Askari wa Jeshi la Polisi anayesimamia Dawati la Jinsia pale Bukoba kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ninaamini endapo Serikali itaamua kuendeleza utambuzi huu kwa kutenga bajeti iliyo madhubuti na kuwapa vitendea kazi, basi Maafisa Ustawi wa Jamii wataweza kutekeleza majukumu yao na tutaweza kuwa na jamii yenye ustawi bora na tutaweza kulinda wananchi wote kwa ujumla hususan ustawi na usalama wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninashukuru kwa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, na Mheshimiwa Seif Gulamali, ujiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu wa Marekebisho Mbalimbali ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia Mabadiliko ya Sheria yaliyofanyika kwenye Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji *(The National Irrigation Act)*. Kimuundo ilivyo sasa hivi, Maafisa wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wanaishia ngazi ya Mkoa, wanaishia Mkoani kisheria, wakati miradi ya umwagiliaji mingi iko huku chini Halmashauri, ngazi za Wilaya, Vijiji na kwenye Kata.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria, majukumu yao sasa hivi, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inajenga skimu mpya za umwagiliaji halafu ikimaliza kujenga inaishia hapo, wanawakabidhi vyama vya wale wakulima wanaotumia eneo lile, ambavyo vinaitwa vyama vya umwagiliaji pamoja na Halmashauri ili kuendesha skimu hizo. Kwa hiyo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wao wanaishia kwenye kujenga tu, lakini katika kuendesha, wanawaachia vyama vya umwagiliaji ambao ni wakulima pamoja na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa *practice* hii imeonesha kwamba uwezo wa wale wakulima, vyama vya umwagiliaji na Halmashauri kuhudumia hizi skimu za umwagiliaji umekuwa ni shida na uko katika kiwango ambacho hakiridhishi. Ndiyo maana utakuta kuna skimu nyingi za umwagiliaji ambazo zimejengwa, zimefanya kazi kwa muda mchache, ikatokea tu labda mvua kubwa, maji yakakata tuta au nini, hivi vyama vya umwagiliaji pamoja na Halmashauri, uwezo wa kuzihudumia skimu za umwagiliaji umekuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, skimu nyingi unakuta zimejengwa, lakini baada ya hapo mwaka mmoja au miwili, hazifanyi kazi tena. Kwa hiyo, tunayo mifano ya skimu nyingi tu za umwagiliaji ambazo zimejengwa, zimekamilika, lakini zimeshindwa kuendelea kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mabadiliko yaliyoletwa kwenye hii Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, yanashusha sasa hawa

Maafisa Umwagiliaji, wasiishie tu ngazi ya Mkoa, bali washuke mpaka ngazi ya Wilaya ili waweze kuzisimamia hizo skimu kule chini Wilayani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mabadiko haya, yanatoa sasa uwezo wa hawa Maafisa Umwagiliaji ambao wameshushwa mpaka Wilayani kuzisimamia skimu za umwagiliaji *on a daily basis* na kutoishia kwenye kuzijenga tu, bali na kuhakikisha zinaendelea kufanya kazi na zinaendelea kutoa huduma kwa wananchi hasa wananchi ambao wanaunda hivyo vyama vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano mingi, kwa mfano mimi kwenye Jimbo langu, nina skimu kadhaa za umwagiliaji ikiwemo Skimu ya Umwagiliaji ya Kahama ya Nhalanga na Skimu ya Umwagiliaji ya Ikindwa na Skimu ya Umwagiliaji ya Mwagogulu. Skimu hizi zilijengwa na Serikali kwa gharama kubwa na baada ya kujengwa, Tume ya Umwagiliaji wakakabidhi kwa vyama vya umwagiliaji chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, skimu hizi karibu zote sasa hivi hazifanyi kazi kwa asilimia ile iliyokusudiwa, kwa sababu zimeharibika na zinahitaji matengenezo ambayo kwa uwezo wa hivi vyama vya umwagiliaji vya wakulima wenyewe na Halmashauri hawawezi kuzi-*maintain*. Kwa hiyo, inahitaji *intervention* ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa sababu wanao utaalamu na bajeti ili ku-*maintain* hizi skimu ziweze kufanya kazi muda wote.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya pia yatafanya hata Maafisa Ugani kule chini waweze kuwa *busy* na kutumika ipasavyo. Kwa sababu sasa hivi Serikali imefanya juhudi kubwa sana kuwawezesha Maafisa Ugani kwa kuwapatia vyombo vya usafiri, mashine za kupimia udongo, na mambo mengine. Kwa hiyo sasa, haya mabadiliko katika sheria hii yatafanya sasa watumike ipasavyo na waongeze tija kwenye kilimo chetu ambacho tunakitegemea sana hasa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nadhani wote tunafahamu na haipingiki kwamba ili tuweze kuongeza tija kwenye kilimo na kuleta mabadiliko ya maana kwenye kilimo, hakuna namna. Ni lazima

tujikite sana katika ku-*leverage* kilimo cha umwagiliaji. Sasa hivi kuna mabadiliko ya tabiachi. Kwenye baadhi ya maeneo mvua zimekuwa za shida, siyo kama ilivyokuwa katika siku za nyuma. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunatumia skimu za umwagiliaji kuongeza tija katika kilimo kwa maana ya kupata mazao mengi na kwa mavuno mengi kwa hekari moja.

Mheshimiwa Spika, nalishawishi Bunge liunge mkono mabadiliko haya katika Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ili Maafisa wa Tume ya Umwagiliaji wasiishie mkoani, washuke chini mpaka ngazi za Wilaya na huko chini ambako ndiko skimu za umwagiliaji zilipo. Pia, wafanye kazi ya ku-*maintain* hizi skimu ili ziendelee kuwepo badala ya kuishia kujenga tu na kukabidhi kwa vyama vya wakulima na Halmashauri ambao kimsingi *practice* imeonesha uwezo wao wa kuhakikisha skimu zinaendelea kuwepo ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono mabadiliko haya na ninalishauri Bunge likubaliane na liunge mkono ombi hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Hussein Amar ajiandae.

Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Boniphace Butondo ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwa sehemu ya wachangiaji katika hii Miswada miwili ambayo imeletwa.

Mheshimiwa Spika, binafsi nipende kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, jana tumeshuhudia upokeaji wa Waheshimiwa Marais zaidi ya 27 kutoka ndani ya Afrika na tumeshuhudia Waheshimiwa Makamu wa Marais, Mawaziri Wakuu na viongozi mbalimbali lakini

pia ikiwepo Rais wa Benki ya Afrika na Benki ya Dunia wakija hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hii iinaonesha jinsi gani ambavyo ana ushawishi ndani ya Afrika na nje ya Afrika. Hongera sana Mheshimiwa Rais, hakika umeitangaza Tanzania ndani na nje ya Bara letu la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupata uteuzi wa Chama chake cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Urais wa CCM mwaka huu 2025. Hongera nyingi kwake. Ama kwa hakika, anapata utulivu wa kuendelea kuliongoza Taifa hili kwa miaka mingine mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudi katika hii Miswada ambayo ipo mbele yetu, tunayo Miswada miwili ambayo ni Miswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3)* na *(No. 4) Bill, 2024)*. Miswada hii yote tumeijadili ndani ya Kamati kwa muda wa zaidi ya wiki mbili. Tunaishukuru sana Serikali kupitia Wizara zote pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tumekuwa tukibishana katika maeneo mbalimbali na katika maboresho katika maeneo ambayo tulikuwa tukiwaelekeza kufanya maboresho, wameendelea kuiboresha na leo tunaiona Miswada hii imekuja, na kwa hakika imekaa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kusema, mfano huu Muswada wa Sheria wa Marekebisho wa Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2024, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2024*) na Muswada wa Marekebisho wa Sheria (Na. 4) wa mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 4) Bill, 2024)*. Zipo sheria toka zimetungwa hazikuwa na maboresho na zile ambazo zimefanyiwa maboresho nyingine zimefanyiwa mara moja, lakini lengo kuu ya Miswada hii kuileta hapa Bungeni ni kuhakikisha kwamba tunaongeza usimamizi, tunaongeza udhibiti, tunaongeza kukuza mitaji na kuwawezesha wananchi wetu kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana unaweza ukaona tuna Sheria ya Kudhibiti na Utakatishaji Fedha Haramu, Sura ya 423 *(The Anti-Money Laundering Act, (Cap. 423)* lakini ipo Sheria ya Vyama vya Ushirika hii tumeweza kuichambua hii Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura ya 211 *(The Cooperative Societies Act, (Cap 211),* na Sheria ya Tasnia ya Pamba.

Mheshimiwa Spika, ninajua wakulima wa pamba ni wadau wakubwa sana wa hii sheria, lakini lengo letu lilikuwa ni kuhakikisha kwamba vile vyama vya ushirika, yule Afisa Msimamizi wa Kilimo, anaweza kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa kuhakikisha kwamba kilimo cha pamba kinakuwa na tija, na pia vyama vya ushirika vinaweza kusimamiwa kwa ukaribu zaidi kuhakikisha kwamba na vyenyewe vinaleta tija hasa idadi ya wajumbe katika vyama vyetu vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kupitia Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, Sura ya 386 *(The National Economic Empowerment Act, (Cap. 386)* na yenyewe hii, ni kuwawezesha wananchi wetu katika masuala mazima ya kuhakikisha uchumi wa mtu mmoja mmoja, na uchumi wa nchi unakua.

Mheshimiwa Spika, tumepitia pia Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati katika kuboresha wakaguzi na wasimamizi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuwa na mahusiano ya karibu katika usimamizi. Hizi *scheme* zetu zinaharibika huko chini wakati mwingine zinakosa nani wa kuzisimamia.

Mheshimiwa Spika, *scheme* ikiharibika katika eneo mfano pale Igunga, ukienda kuomba fedha labda kwenye halmashauri ili waweze kurekebisha ile *scheme,* baada ya kuwa imeshatengenezwa unaambiwa hii ipo kwenye Wizara ya Umwagiliaji. Wizara ya Umwagiliaji wanakwambia hili jambo lipo kwenye halmashauri. Kwa hiyo, tumerekebisha hii sheria kuhakikisha kwamba tunaongeza ufanisi na usimamizi wa karibu katika kuboresha *scheme* zetu na ziwe na usimamizi ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Spika, pia Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 *(The Public Audit Act, [Cap. 418])* na hii yenyewe yote ni katika kuhakikisha kwamba udhibiti wa fedha za umma katika maeneo mbalimbali ambapo zinatolewa na yenyewe tumeipitia. Kwa hiyo, sheria zote hizi tumezipitia kwa lengo la kuhakikisha tunaongeza usimamizi, udhibiti, ukaguzi, kukuza uchumi, kuongeza uzalishaji na pia kuboresha vyama vyetu vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu Bunge letu hili liweze kuzikubali na kuzipitisha hizi sheria kuonyesha kwamba zinaweza kwenda kutekelezeka na tutunge hizi sheria ambao zinaweza kwenda kutusaidia sisi wananchi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja ambazo nilikuwa nikizichangie hapa pia, lakini kwa sababu umeziondoa baadhi, zile mbili, kwa hiyo nami mchango wangu katika hayo maeneo pia na-*reserve* kuhakikisha kwamba tutakapoileta nitakuwa sehemu ya wachangiaji kuhakikisha kwamba kile ambacho nimejiandaa nacho naweze kukiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Butondo, na Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze nami kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM ambao na mimi ni mjumbe na kumpitisha kuwa mgombea Urais kwa mwaka 2025 kwenye Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe tuliamua hivyo kwa sababu nyingi, lakini naweza nikazitaja sababu chache. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kufanya kazi kubwa na kuchangia miradi yetu mingi kwa nchi nzima ikiwemo elimu, afya,

miundombinu, lakini pia na mambo mengine mengi ikiwemo pamoja na usafirishaji wa anga na reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mwanasheria Mkuu kwa kuleta marekebisho ya sheria namba tatu na namba nne, zile sheria sita kwenye Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria, mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati hiyo tumeweza kuzichakata na kuangalia upungufu uliokuwepo, na pia kurekebisha na kuona baadhi ya sheria ambazo zimekwenda kama vile kupitwa na wakati, zilikuwa za muda mrefu, za miaka mingi, lakini ukizingatia na uhalisia wa sasa hivi, tuliona kuna umuhimu sana wa kuzibadilisha kutokana na uhitaji wa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, sheria hizo sita tumeweza kuzichambua na tumeweza kuzipitia vizuri. Mimi kama Mjumbe wa Kamati nalishauri Bunge liungane na maoni na ushauri wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria ili tuweze kuzipitisha hizo sheria ili ziendane na wakati na kuleta matumaini katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sina mengi sana, nimesimama tu hapa kulishawishi Bunge liweze kuungana na Kamati kwa ushauri wote ambao tumeuleta mbele yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na maoni ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, na Mheshimiwa Deogratius Mwanyika ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika marekebisho haya ya sheria mbalimbali ambazo zimewasilishwa na nina uhakika Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na wataunga mkono, nami nawashawishi na kuwashauri waunge mkono ilimradi kazi iweze kuendelea katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba niunge mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo nchi yetu inapendeza kwa kuletewa maendeleo mengi, lakini nampongeza pia kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Urais katika uchaguzi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wana-Kishapu tuna imani kubwa kwamba Mheshimiwa Rais wetu ataendelea kuliendesha gurudumu la maendeleo vizuri kama alivyokuwa anafanya katika kipindi hiki na tunajivunia mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imeyapiga katika kipindi hiki cha miaka minne tangu uongozi wake ulipoanza wa Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nikupongeze wewe kwa namna ambavyo tunakwenda vizuri, unavyotuendesha kama Bunge. Pia, ninampongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna ambavyo amewasilisha Miswada hii katika Kamati na kwa namna alivyotoa ushirikiano na tulivyoichakata kwa pamoja kama Kamati ya Katiba na Sheria chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Dkt. Mhagama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianzie na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sura ya 211 na hasa juu ya jambo zima la kupunguza muda ule wa usajili wa vyama vya ushirika na hasa vile vya vyama vya msingi ambavyo vilikuwa vinachukua siku 20 mpaka siku 14 na kabla ya pale ilikuwa inachukua muda mrefu zaidi na mapendekezo ya Serikali yakaja ipunguzwe kutoka siku 20 na kuendelea na ibaki siku 14, lakini Kamati imetumia busara kubwa na kushauri kwamba ingefaa iwe siku saba peke yake.

Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zipo. Kitu cha kwanza sasa hivi nchi yetu tumekuwa na Mkongo wa Taifa na hivyo tumeboresha pa kubwa sana suala zima la mfumo wa kisasa wa kidigitali na kwamba mifumo kwa ujumla wa kimtandao imekuwa ikifanya kazi vizuri maofisini na hasa maeneo yote tu ambayo Serikali inatekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, jambo hili yatupasa tubaki katika siku chache zaidi kwa sababu haipo sababu ya kuchukua siku nyingi hizo. Nami ninaendelea kuunga mkono kwamba siku saba zinatosha kufanya usajili wa vyama vyetu vya ushirika na ilimradi vyama hivi viweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati, lakini na kupunguza urasimu usiokuwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashawishi na kuomba kwamba jambo hili lifanyike katika siku hizo saba, lakini pia zipo sababu nyingi, kwa kuwa michakato hii inaanzia ngazi za chini, kuanzia chini huko kwa Maafisa wanaohusiana na kilimo ngazi ya kata, ngazi ya vijiji na kwenda wilayani, kwa hiyo, taratibu za usajili zinaweza zikafanyika kwa muda mfupi ili kupunguza urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na marekebisho ya tasnia ya pamba ambayo kuna suala lililokuwa linamhusu afisa aliyekuwa anaitwa *cotton inspector* na sasa hivi anabadilika kuwa *agricultural officer* kwa maana ya kwamba mabadiliko haya nayaunga mkono kwa sababu kimsingi yanaendana na muundo wenyewe wa tasnia ya pamba kuhusu suala zima la watumishi. Kwa hiyo, kimsingi ni kwa sababu limekuja katika muda muafaka ili kuendana na muundo wa kiutumishi katika tasnia ya pamba, nakubaliana kwamba *cotton inspector* anaweza akaondoka katika tafsiri ya kwamba yeye ndio atakuwa kama Mkuu wa Idara ya Kilimo alikuwa anasimama kama Mkuu wa Idara ya Kilimo na Viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa kumbadilisha kuwa *agricultural officer,* maana yake atasimamia masuala yote yale ya kilimo bila kujali kilimo cha pamba, kilimo cha korosho na kilimo cha mazao mengine yote. Kwa hiyo, huyo atashughulika na mazao yote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko hayo, Kamati tulishauri kwamba pamoja na kumwondoa huyu *cotton inspector* kushughulika na masuala yote ya kilimo, ukaguzi wa kilimo kwenye masuala ya viwanda, ashughulike kwa ujumla na masuala ya kilimo. Tunashauri *cotton inspector* angebaki kama mkaguzi peke

yake wa pamba, kwa sababu tunajua pamba ina sheria zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu yapo mazao makubwa ya kimkakati ya kibiashara ambayo yana sheria zake. Mazao kama kahawa, zao kama korosho, zao kama pamba na katani, tunafahamu sote kwamba haya ni mazao ya kimkatati tangu enzi za Mwalimu Nyerere na ndiyo maana yalitungiwa sheria maalumu za mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunashauri na kama Kamati tulivyoshauri kwamba *cotton inspector* abaki kama afisa atakayekuwa yupo chini ya *agricultural officer,* ambaye atasaidia kwa ujumla katika suala zima la kusimamia suala la pamba, hii ni pamoja na kusimamia kanuni za kilimo bora za pamba, hii ni kusimamia usafi wa zao la pamba, pamoja na kusimamia masoko, zile *societies* ambazo zinanunua pamba kwa maana ya *buying posts* zote zilizopo chini, na pia kukagua pamba katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kutokuondoa hili neno la *cotton inspector,* lakini awe chini ya *agricultural officer.* Kwa hiyo, hili tulikuwa tunashauri sana kwamba lisimamiwe kwa ajili ya kulinda ubora wa pamba, na huyo atakuwa anakagua mashamba, kuangalia kama kanuni za kilimo bora za pamba zinakwenda, usafi wa pamba masokoni na maeneo mengine. Kwa hiyo, kwa msingi huo, ndiyo maana tunasema kwamba hii ni vizuri *cotton inspector* akabaki lakini akawepo akawa chini ya *agricultural officer. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, naomba nami nitumie nafasi hii kuwashawishi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukubaliana na marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Mwanyika, na Mheshimiwa Florent Kyombo, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao kwa nafasi ya kwanza wamempongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na Chama chake Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba naye, ninampongeza sana Dkt. Emmanuel John Nchimbi ambaye ameteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea mwenza kwa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia asubuhi hii kwenye marekebisho ya sheria hizi mbili ambazo zimekuja mbele yako leo. Maeneo mengi yamepata uchangiaji kutoka kwa Wabunge waliyotangulia, lakini nami nilitamani niweke mkazo kwenye maeneo kama matatu.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako nilitamani nianze na Marekebisho ya Sheria ya Mawakili Sura ya 341 *(The Advocates Act, (Cap 341)*. Muundo wa Kamati hii ya Taifa ya Mawakili iliacha ombwe pale ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuwa na maslahi kwenye mashauri yanayoweza kuletwa dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, Waheshimiwa Wabunge mkirejea Kamati hii, Wajumbe wanaounda Kamati hii utabaini kwamba yupo Jaji wa Mahakama Kuu, lakini yupo Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, sasa pale ambapo inatokea Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameletewa mashtaka ambayo yanatakiwa yafanyiwe maamuzi, utajikuta kwamba Mwanasheria Mkuu haingii, kwa hiyo, hawezi kuwa na kura ya maamuzi, lakini

pia Naibu wake kwa sababu anatoka ofisi hiyo hiyo, hawezi kuingia, kwa hiyo, hawezi kuchangia kwenye kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mazingira kama hayo yameonekana kwamba yanaweza kukwamisha maamuzi katika Kamati ya Taifa ya Mawakili.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati mwanzo yalikuwa kwamba, ili huyu mjumbe anayeongezwa kupata akidi, atokane na Chama cha Mawakili Tanganyika. Hata hivyo, baadaye baada ya mjadala na ufafanuzi mzuri wa Serikali, tulibaini kwamba mapendekezo ya Serikali yabaki hivyo yalivyo kwa sababu yanatuwezesha kupiga hatua wakati tutakapotakiwa kufanya maamuzi juu ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pia, nami nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono sehemu hiyo ya Muswada kwa sababu inatusaidia kufanya maamuzi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitamani nichangie na kwa sababu halijapata wachangiaji wengi, ni marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 *(The Mining Act Cap. 123)*.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya wakati yameletwa kwenye Kamati, kulikuwa na mvutano kidogo na Serikali. Sababu kubwa ilikuwa ni kwamba, waliolengwa au marekebisho haya yanalenga kuifanya taasisi ya umma ambayo inaweza kuwa halmashauri ya wilaya au taasisi yoyote ya Serikali ambayo inatoa ukandarasi *(contract)* kwa *contractors* wanaojihusisha na masuala ya madini (Mchanga, kokoto na madini mengine) kuwa mawakala wa Tume ya Madini, kwa maana ya kwamba, wakusanye mrabaha kwa niaba ya Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona Serikali ina mawazo mazuri na mapendekezo yaliyotoka kwenye Kamati ni mazuri. Hata hivyo, imejinyima fursa, kwa sababu katika mapendekezo haya haya, Serikali ilikuwa na fursa ya kupanua wigo kwa sababu anayetoa kandarasi siyo taasisi ya umma peke yake, zipo

kampuni binafsi kubwa ambazo pia zinaajiri na zinatoa kandarasi mbalimbali ambazo zinahitaji matumizi ya maliasili za madini. Kwa hiyo, hao pia wangetumika kama mawakala wa kukusanya mirabaha ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho haya ambayo Kamati imeridhia na ambayo ninaliomba Bunge liridhie, Serikali ikafanye kazi ya ziada kuona uwezekano wa Sekta Binafsi kuingia kuwa wakala wa ukusanyaji wa mirabaha ya Serikali ili kupanua wigo wa mapato ya Serikali na hivyo kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ambayo nilidhani nichangie pia ni Sheria hii ya Utumishi wa Umma Sura ya 298. Sheria hii inamhusu Katibu Mkuu Kiongozi. Wengi hapa tunajua hali halisi ya viongozi wetu wakubwa. Kwa namna ambavyo Makatibu wakuu wetu viongozi wanavyotoa muda wao kuwatumikia Watanzania kupitia kutumikia Sekta ya Utumishi wa Umma, haiwapi fursa ya kufanya shughuli nyingine kwa *nature* tu ya kazi yao. Sasa katika mazingira kama hayo, wanakuwa *fully dedicated* kwenye kazi moja tu ya kusimamia shughuli za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, huyu ni mmoja katika viongozi muhimu katika Taifa letu. Ninajua na sisi kama Kamati tulijiridhisha tunayo mihimili hiyo mitatu, lakini ndani ya mhimili wa Serikali bado kuna baadhi ya maeneo ambayo watumishi wake wanahitaji motisha ya hali ya juu ili waweze kufanya kazi kwa uadilifu na uzalendo mkubwa. Sasa tuliona, Serikali kwanza iliona, lakini Kamati pia ikajiridhisha na kuna hoja ambazo zimeletwa na Serikali zina msingi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, moja, itampa motisha huyu Katibu Mkuu Kiongozi kufanya kazi kwa uadilifu zaidi, akiona kama Taifa tumekwishamwekea ulinzi wa maisha yake yote. Hata hivyo, ipo *tendency* ya baadhi ya viongozi ambao tunawapa fursa za kuitumikia nchi yetu katika ngazi mbalimbali, zinatumika vibaya kwa sababu wanaomzunguka na wanaomtegemea wanakosa

*security*. Katika sheria hii, tumeongeza *security* kwa mke wake na familia.

Mheshimiwa Spika, ninaposema *security,* simaanishi ulinzi wa mitutu ya bunduki. Tunamaanisha *financial security* ili waweze kukidhi mahitaji yao ya wakati wote. Sasa kwa sababu uongozi haumhusu mtu mmoja na unahusu pia familia, tuliona ni vizuri tukalitazama katika mapana hayo. Tumekubaliana na mapendekezo ya Serikali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, tumetoa pia tahadhari. Yapo mazingira ambapo Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kumaliza kazi ya ukatibu Mkuu Kiongozi, huwa anateuliwa kwa jukumu lingine. Tumeona wengine wamepata nafasi za Ubalozi na wakapelekwa kwenye vituo vya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya, tumeiomba Serikali ifikirie upya utaratibu huu. Kwa sababu huyu kiongozi ambaye anastaafu, ameshawekewa utaratibu mzuri wa kustaafu, ni vizuri baada ya kumaliza majukumu haya astaafu ili nafasi hizo nyingine wapewe Watanzania wengine ambao wana sifa zinazotosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratius Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nifanye marekebisho kidogo kusudi *Hansard Record* zikae vizuri. Ninajua hata wewe umeshangaa! Jina langu naitwa Deodatus na siyo Deogratius. Ni maneno ya Kilatini yenye maana tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kuwa mgombea pekee wa chama chetu. Pia, Mheshimiwa Dkt.

Nchimbi naye vilevile kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mimi nina nyongeza. Napata fahari kubwa sana ya kuwa kiongozi katika Bunge lako na kuwa Mtanzania ambaye nchi yetu jana na juzi imetambuliwa na ulimwengu mzima kwa sababu ya suala la nishati salama. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake kubwa za kuifanya nchi yetu iwe ni moja katika nchi muhimu sana Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nichangie kwa kifupi tu Muswada ulio mbele yetu, Sheria (Na. 5) ya 2024/2025, kwa maana moja kwamba, ukiangalia Sheria nyingi ambazo wenzangu wameshaziongea, Sheria ya Umwagiliaji, Sheria ya Pamba na Sheria ya Ushirika, ni sheria ambazo kwa kiasi kikubwa zinaleta suala kubwa la uwazi na uwajibikaji katika sekta za kilimo. Kwa hiyo, kwa nafasi yangu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, niliona ni vizuri nami nikachangia kwenye Muswada huu na *nika-focus* zaidi kwenye Sheria ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, katika Sheria hii Sura ya 211, wachangiaji wengine wamesema hapa kwamba, inaongeza uwazi kwenye kuomba uundaji wa chama cha ushirika. Hapo mwanzo Mrajisi aliweza kupokea *application* akakaa nayo na hata kama akitoa majibu ya kutokukubali, asitoe sababu na asilazimike kukupa sababu au asilazimike kukujibu. Sasa tunaona kwamba ndani ya siku 10 atatakiwa kutoa majibu kwamba kwa nini pengine hajaruhusu chama hicho kipate usajili? Ni jambo linaloongeza uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, jambo lingine ambalo ni la muhimu na ningependa niliongelee, ni Ibara ya 11 ambayo inakwenda kufanya mabadiliko kwenye kifungu Na. 55. Ibara hii au kifungu hiki kinazungumzia masuala ya mahesabu na ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa na ninadhani ni jambo linalofahamika kwamba, vyama vyetu vya ushirika vimerudi. Kwa miaka ya huko nyuma vilikuwa katika hali nzuri sana na ilikuwa

unasikia sifa kuwa mwanaushirika. Pia, vilikuwa ni *icon* ya uzalishaji. Hata hivyo, kwa miaka ya hivi karibuni, vyama vile vilivyo vingi vimekuwa katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa ambayo imefanyika miaka 10 iliyopita, tunaona kabisa kwamba vimeanza kufufuka na vinarudi na kuanza kupata ule ung'ao wake. Hata hivyo, bado vinapitia changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninatoa ushawishi kwa Wabunge kuunga mkono mabadiliko haya kwa sababu Sheria hii ya Ushirika iliyo mbele yako kwa kiasi kikubwa sana pamoja na kuondoa urasimu niliouongelea, lakini inaongeza uwazi, udhibiti na vilevile inaongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kwamba, kwanza katika kuongeza uwazi na udhibiti, unapoongelea mahesabu, mtu wa kwanza kwenye hesabu ni *internal auditor* wa chama cha ushirika. Hata hivyo, *internal auditor* au chama kinakuwa *audited* na *external auditor*.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa zamani ilikuwa Mkutano Mkuu wa Chama, unachagua nani awe mkaguzi. Pia, kwa kweli *Bank of Tanzania* ilikuwa bado ina *role* ndogo kwenye hilo. Hata hivyo, kwenye kudhibiti jambo hili sasa, tunaona wazi kwamba sasa kwenda mbele, Mkaguzi wa chama cha ushirika atakuwa ni lazima aridhiwe na Benki ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna uhakika kwamba, Benki yetu ya Tanzania sasa yenyewe ina utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kujua ni nani wanaweza wakawa wadhibiti wazuri kwenye maeneo ya vyama vya ushirika. Kwa hiyo basi, *Bank of Tanzania* itaandaa orodha ambayo vyama vya ushirika vitatakiwa kuchagua wakaguzi kutoka kwenye orodha hiyo. Hilo ni jambo zuri la udhibiti au *control*. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu wote kwamba, moja ya changamoto kubwa ya vyama vya ushirika ilitokana na ubadhirifu na wizi wa mali na fedha za vyama vya ushirika. Sasa siyo

kwamba kulikuwa hakuna udhibiti, kulikuwa na udhibiti ambao ulifuata matakwa ya sheria iliyopo.

Mheshimiwa Spika, katika kufuata matakwa ya sheria iliyopo, bado kulikuwa na urasimu mkubwa ndani ya sheria ambao ulitoa mwanya zaidi kwa wale wanaotuhumiwa kuwa na nafasi ya kufanya mambo mengine ambayo yatawaweka mbali na mkono wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pia, sheria iliyopo mbele yetu sasa inaziba huo mwanya kwa kumpa mamlaka mahususi mrajisi wa vyama vya ushirika kwamba, itakapotoka tuhuma baada ya hesabu ambayo imepitia kwenye *process* ya kuhakikiwa au kuwa *audited*, itakapotoka kwamba kuna tuhuma zozote, kwa mujibu wa kifungu kipya ambacho kimeletwa na Ibara ya 11 kifungu Na. 55 (14), Mrajisi wa vyama vya ushirika sasa atakuwa na mamlaka kwa maslahi ya kulinda afya ya chama cha ushirika na kwa maslahi ya ustawi wa chama cha ushirika, kuchukua hatua zozote ambazo ataona zinafaa wakati jambo hili likiwa bado linaendelea kwenye upelelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ni kwamba, mrajisi huyu sasa ingawa hakuweza kufanya huko nyuma, sasa atakuwa na mamlaka ya kisheria ya kudai maelezo kutoka kwa watuhumiwa kwa haraka kuhusiana na hasara au wizi unaosemekana. Vilevile, atakuwa na mamlaka ya kuisimamisha Bodi ya Chama cha Ushirika mara moja. Pia, siyo hilo tu, atakuwa na uwezo wa kumsimamisha Mtendaji Mkuu kwa tuhuma zinazoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo ilikuwa ni lazima aingie kwenye utaratibu wa kawaida. Alikuwa na mamlaka ya kutoa *surcharge* kutaka maelezo, lakini mtu ambaye anatuhumiwa na akapewa *surcharge*, alikuwa na uwezo wa kutoa maelezo. Pia, kama akiona kwamba mrajisi anataka kumchukulia hatua, alikuwa anaweza kwenda kwa Waziri ndani ya siku 30 akaomba na kufanya *appeal* kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, pia, Waziri alikuwa halazimiki kisheria kutoa mwelekeo ndani ya siku kadhaa. Alichoweza kufanya ni

kwamba, toka ambapo Waziri atatoa maelekezo, ndani ya siku 15 mtu huyo alitakiwa afanye utaratibu, kama ni wa kulipa au kutokulipa, ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kwamba, Waziri hana tena nafasi hiyo, au hata kama anayo, tayari mrajisi atakuwa ameweza kuchukua hatua ambazo zinaweza zikasaidia kuzuia ubadhirifu zaidi au kupoteza ushahidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni la muhimu na ningependa baadaye kutoa ushauri, linahusiana na Ibara ya 14 ambayo inakwenda kubadilisha kifungu Na. 74 kwa kuongeza *sub para number four*. Ni wazi kwamba baadhi ya maeneo ya ubadhirifu yalitokana na watu kutafuta upenyo ndani ya Sheria. Vilevile, watu walitengeneza kampuni na waliweza kuhamisha *assets* kwenda kampuni hizo. Pia, kwa kufanya hivyo, ubadhirifu uliweza kufanyika kirahisi zaidi kwa sababu *a company is the separate legal personality*. Mrajisi hana mamlaka ya kushughulika na kampuni.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa maana ya kampuni, kampuni inaripoti kwa wanahisa. Kwa hiyo, sheria ya zamani ilikuwa imetengeneza hiyo *loophole* na hapakuwa na miongozo thabiti ya kuweza kushughulika na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa kifungu Na. 74 ambacho kinazungumzia uwekezaji wa fedha za ushirika ambalo ndilo jambo muhimu kubwa katika vyama vya ushirika, katika kifungu hiki kilichoongezwa sasa, tunaona kwamba sasa mrajisi atatakiwa; moja, kuhakikisha kwamba anaweka utaratibu na miongozo ambayo ita-*guide* uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kampuni zilizoundwa, utakuta Mwenyekiti wa kampuni iliyoundwa ambayo inachukua hizo mali za vyama, kampuni hiyo Mwenyekiti wake ni yule yule ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika. Utakuta Mtendaji wa Chama cha Ushirika naye ni Katibu wa Kampuni. Kwa maana hiyo *there is a clear conflict of interest* ambayo mrajisi peke yake asingeweza kuishughulikia kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, pia, hawa watu kwa mujibu wa sheria hii iliyopo, walikuwa wanaingia kwenye utaratibu wa kawaida wa kimahakama ambao wote tunaufahamu. Pamoja na jitihada kubwa za kupunguza mlundikano wa kesi ndani ya Mahakama zetu, lakini bado *challenge* hiyo ipo. Kwa hiyo, zingechukua muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa sasa wa *sub-clause (4)* ambayo inaletwa na Ibara ya 14, Waziri sasa atatumia kifungu 141 *sub-clause (2)* ambayo nayo imekuwa *amended* kwa kubadilisha *sub-clause (p)* kwa kumpa mamlaka ya kutoa miongozo na *guidance* ya namna ya vyama vya ushirika kufanya uwekezaji. Pamoja na kwamba vilikuwa vinaruhusiwa, vinaweza vikaingia kwenye *bonds*, vinaweza vikanunua *shares*, vinaweza vikanunua dhamana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sheria sasa inamtaka Waziri aweze kutoa miongozo mahususi kuhusiana na masuala ya uwekezaji ambayo ndiyo ilikuwa *conduit* kubwa ya ubadhirifu na wizi kwenye vyama vingi vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa wazo na angalizo kwamba sheria hizi, *(rules)* hizi, ni vizuri zikatengenezwa mapema na zikafanya ushirikishwaji kama ambavyo utaratibu unataka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia katika marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Sheria (Na. 03) na Sheria (Na. 04).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nami niungane na wenzangu kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono na utayari wake wa kuweza kuleta hizi sheria kubadilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kimahususi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kuaminiwa na chama chetu na kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais katika uchaguzi ujao kwa kiti cha Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika sambamba na hilo, nimpongeze pia naye kwa kumwamini na kumwona kaka yetu Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi anafaa kuwa mgombea mwenza, na pia nimpongeze Mheshimiwa Stephen Wasira kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana wewe kwa kuamini Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria tukiongozwa na kaka yetu ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, nami nikiwa Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote tulioletewa mabadiliko ya sheria mbalimbali hizi mbili; Sheria ya Marekebisho ya Sheria (Na. 3) na (Na. 4) ndani yake yakiwa na jumla ya sheria 14.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuliambia Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kwa weledi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na wasaidizi wake, kwa weledi wa Wizara zote ambazo mabadiliko ya hizi sheria ndogo ndogo 14 zimegusa katika sekta mbalimbali Mawaziri na wasaidizi wao, lakini kwa weledi wa Kamati yetu, tumeweza kupitia vizuri na kijiridhisha pasipo shaka na kuleta kwenu. Kwa hiyo, nawaomba kwa heshima kubwa kwamba turidhie kuunga mkono sheria hizi ziweze kupita na sheria ziweze kutungwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mbalimbali yameguswa na wachangiaji mbalimbali, lakini nami sina budi kuweza kugusa katika maeneo machache kwa ajili ya kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ambalo linagusa uchumi wa nchi yetu na Pato la Taifa ni katika eneo la kilimo. Katika eneo hili, tumeona tunarekebisha Sheria ya Tume ya Umwagiliaji ambayo kwa msingi mkubwa tunaona katika eneo la umwagiliaji kwa kweli limekuwa ni eneo ambalo tunaweza kuwa na kilimo

chenye tija na cha uhakika, na sasa tukiweka misingi mizuri na mnyororo wa mawasiliano katika tume hiyo, basi sasa lile lengo kubwa la Taifa letu la kuweza kupata pato kubwa kutokana na kilimo cha umwagiliaji linaweza kutimia.

Mheshimiwa Spika, hiyo inajibiwa kwa kuhakikisha kwamba tunapokuwa na Ofisi ya Taifa inayosimamia eneo la umwagiliaji tukawa na Ofisi ya Mkoa ambayo inasimamia eneo la umwagiliaji, basi siyo budi kuwa na Ofisi ngazi ya Wilaya ambapo kimsingi katika wilaya ndiyo maeneo ambapo tunawekeza uwekezaji mkubwa katika maeneo yetu mbalimbali katika majimbo na wilaya. Kwa hiyo, sheria hii imekuja kuziba lile *gap* ambalo lilikuwepo la kuhakikisha kwamba ngazi ya wilaya sasa tunakuwa na ofisi ambayo itasimamia kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaamini ule upungufu wote ambao Wabunge wote katika majimbo mbalimbali na wilaya zetu tunashuhudia tumekuwa na skimu za umwagiliaji viporo ambazo zilijengwa nusu, zikabaki nusu, ikawa kwa kweli kilimo cha umwagiliaji badala ya kuwa tija, kikawa ni kilimo ambacho kiliweza kutumia fedha za Serikali pasipo kufikia mwisho na thamani ya fedha hizo ambazo ziliwekezwa kutoweza kufikiwa. Kwa hiyo, kwa mabadiliko ya sheria hii, tunaona sasa tunakuja kujibu hiyo changamoto ambayo ilikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli nilipongeze Bunge lako kwa kupokea miswada hii, na pia naipongeza Serikali kwa kuliona hili. Ninaamini litakuwa la tija zaidi, na tunapopitisha sheria hii, naomba basi Serikali iendelee kuweka miundombinu mizuri kuhakikisha kwamba sasa hizi ofisi ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili kwa kweli ni kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais. Tumeona katika maeneo mengi bado anaendelea kujitahidi kuwajali watumishi wake katika ngazi mbalimbali. Katika Miswada hii miwili tumeona pamoja kwamba hawa ni viongozi ambao utumishi wao ndani ya Serikali unahitaji weledi na umakini, lakini pia unahitaji uzalendo na kijitoa kwa moyo ili kuweza kusimamia majukumu katika yale maeneo

waliyopangiwa. Sasa Mheshimiwa Rais amekuja kwa kuboresha kidogo stahili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona katika kazi inayofanyika, kwa mfano tuanze na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni kazi ambayo Bunge letu kwa kweli linaungana na ofisi yake kuona kazi kubwa wanayoifanya, na sasa akiwa anafanya kazi kwa weledi na uzalendo mkubwa, baada ya kustaafu inapokuwa inaonekana kuna wasiwasi mbele. Hiyo inaweza ikaingiliana na msimamo wake wa kuweza kufanya kazi kwa weledi na uzalendo namba moja katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, sasa atakuwa anaona kwamba Serikali imemjali, imemwekea utaratibu mzuri ambao kwa kweli hata baada ya kazi yake, kwa kuwa kazi anayoifanya wakati mwingine kuna msigano huko ndani, maana yake ni sehemu ambayo unagundua makosa mbalimbali, kwa hiyo, wakati mwingine mtu akishastaafu anaweza akakosa hata huduma mbalimbali kutoka kwa watu wanaomzunguka kwa sababu inawezekana katika utendaji kazi wake alishamgusa mtu mmoja au mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali sasa inakuja kumwezesha na kumpa *confidence* kwamba wewe fanya kazi kwa weledi wako na baada ya majukumu yako utaishi vizuri na kuweza kumalizia maisha yako hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuliona hili na hii inaenda sambamba na kiongozi mkubwa wa Serikali ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi kwa kazi wanayoifanya. Sasa baada ya majukumu yao kwisha, basi waendelee kuishi katika *standard* angalau ile ile kama ambavyo walikuwa kwenye majukumu na wasiwe na wasiwasi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninayo kila sababu ya kuipongeza Serikali, na hili tunaona linaendelea katika maeneo mbalimbali hatua kwa hatua. Kwa hiyo, naomba tuendelee kulipokea kwa sababu tumeona hapo nyuma maboresho katika

maeneo mengine katika stahiki za watumishi na hapa wamekuja, na ninaamini Serikali itaenda kuleta maeneo mengine ili kila sehemu angalau iweze kuboreshewa na kuhakikisha kwamba kila mmoja anaishi kwa ustawi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni Shirika la Kariakoo, na tumebadilisha Sheria ya Shirika la Kariakoo ambayo ilikuwa ni Sura ya 132. Hapo awali katika Shirika hili la Kariakoo majukumu yake kwa kweli yalikuwa yako *confined* (yamefungwa) kwamba shirika hili liweze kufanya kazi katika Soko la Kariakoo, lakini ulikuwa ukiangalia ile *composition* hata Bodi ya Wakurugenzi ndani ya shirika hilo ambayo inajumuisha Wizara mbalimbali za Serikali, inajumuisha Mabaraza ya Biashara, lakini pia na uwakilishi wa jamii katika biashara mbalimbali, ilikuwa huoni tija kwamba hawa wote kweli wanakaa kwa ajili ya kusimamia hili soko.

Mheshimiwa Spika, leo tunakuja na sheria ambayo inatanua wigo, inaongeza majukumu, na inawapa nafasi ya kuongezea mamlaka shirika hilo na kuweza kusimamia na masoko mengine. Pia inaipa uhuru taasisi hiyo kuingia mikataba ambayo itasababisha hilo Soko la Shirika la Kariakoo kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili mimi ninaungana na Serikali na ninaunga mkono hoja. Ninaomba na Waheshimiwa Wajumbe wa Mkutano huu waendelee kuunga mkono hoja kwa kuwa ni mapenzi mema ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba sasa hili soko linatanua wigo na linafanya kazi vizuri na inaweza kuongezea katika pato la Taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunavyokwenda, kwa marekebisho haya kwa kweli ni jambo la kuipongeza sana Serikali. Nasi kama Kamati kwa kukuwakilisha wewe ambaye umetupa majukumu haya, tuliona kwa kweli lina tija kwa Taifa letu. Kwa hiyo, niendelee kuipongeza Serikali na kuomba Wajumbe wa kikao hiki chini yako tuweze kuunga mkono hoja, haya marekeisho ya sheria zote ndogo ndogo 14 ndani ya hizi sheria namba tatu na namba nne ili basi hatua ya kutunga sheria iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, ninakushukuru sana kwa nafasi nyingine tena, nami ninaunga mkono hoja *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nimwombe radhi Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika kwa kukoseakosea jina lake. Makatibu Mezani majina ya Waheshimiwa Wabunge yawe yanaandikwa matatu kwa wale wenye majina matatu ili kuondoa hii habari ya mtu kichwani kwake kuwa anawaza Deogratius wakati mtu anaitwa Deodatus. Kwa hiyo, majina yanapoletwa hapa mbele ya wachangiaji yaletwe majina yote matatu, itaondoa huu mkanganyiko ambao kila wakati unajitokeza, na Mbunge analazimika kila wakati kukumbusha jina lake jambo ambalo halipendezi.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuja na Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, viongozi na watendaji wote bila kumsahau kwa upekee Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Hamza Johari kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu kuwezesha Miswada mbalimbali kukamilika.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na wenzangu, tumeshirikiana kujadili Muswada huu kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu sehemu ya saba inapendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 41 ambapo inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu

kipya cha 4A ambacho kitahusu stahiki na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadiliana na Serikali, Kamati tuliishauri Serikali kurejea Ibara ya 143(3) na 144(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninanukuu:-

"Mshahara anaolipwa mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya ibara hii pamoja na masharti yake ya kazi havitabadilishwa, baada ya mtumishi huyo kuteuliwa, kwa jinsi ambayo itapunguza maslahi ya mtumishi huyo, lakini maelezo haya hayahusiki na posho anayolipwa mtumishi huyo." Ibara ya143 (3)

"Mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au aliyepata kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano." Ibara ya 144 (6)

Kutokana ibara hizi, kwa kweli Serikali ilikuwa sikivu na ilifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kifungu hicho kipya cha 4A kinakwenda kumpa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano kuweza kufanya mabadiliko ya stahiki na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa kwenye utumishi wa umma na akiwa amestaafu utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mwakilishi wa wafanyakazi, nimeona moyo wa Mheshimiwa Rais wa kuwajali wafanyakazi katika ngazi mbalimbali za utumishi, halina ubishi. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa na majukumu makubwa sana, lakini Katiba katika Ibara ya 144 (6) kama nilivyoinukuu tumeona ikisema kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba anaweza kustaafu akiwa bado ana umri wa kufanya kazi nyingine, lakini Katiba inamtaka hivyo, lakini Mheshimiwa Rais na Serikali yake wameona umuhimu wa kuja na kifungu hiki ambacho kitamwezesha Mheshimiwa Rais kuweza kufanya mabadiliko ya stahiki na maslahi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akiwa ameajiriwa na akiwa amestaafu.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi ambacho nimetumika kama mwakilishi wa watumishi, nimeendelea kuona moyo wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa watumishi wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi nchini na huo ndiyo uthibitisho wa moyo wa dhati wa Mheshimiwa Rais kwa watumishi nchini kwa kuongeza kifungu kipya katika sheria hiyo chenye maslahi kwa watumishi husika.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunakaribia kuhitimisha hoja yetu hii na kanuni zetu zinatutaka tumalize wachangiaji, wameshaisha. Kwa hiyo, ninamwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aje ahitimishe hoja yake kwa dakika chache. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo unaliongoza Bunge hili na namna ambavyo umeongoza kikao chetu cha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Makamu wake Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya wakati tunaandaa Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira tuliyokuwa nayo wakati tunafanya zoezi hili yalikuwa ni mazuri na tulikuwa na *spirit* ile ya kuelewana katika maeneo ambayo tulihitaji kuelewana, na kwa

kufanya hivyo, ingawa kazi yetu ilikuwa ni ndefu, ilikuwa rahisi, kutokana na *spirit* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda kuwashukuru kwa dhati kabisa, na kwa kufanya hivyo imetusaidia leo hata mazingira mliyokuwa mnayaona wakati wa uchangiaji vilevile yamekuwa mazingira ya kuunga mkono. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wa Kisekta kwa sababu Miswada hii inahusisha sekta tofauti tofauti, kwa hiyo, nawashukuru kwa michango yao mizuri na uwepo wao kipindi chote wakati tunafanya kazi hii. Vilevile, ninamshukuru *Chief Whip* Mheshimiwa William Lukuvi, kwa kazi nzuri ambayo alikuwa anaifanya ya kutu-*coordinate* na kuhakikisha kwamba wakati wote tunatekeleza jukumu hili na kuhakikisha kwamba tunalikamilisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu wa Bunge na timu yote ya Bunge kwa ushirikiano wao ambao walitupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza, madhumuni ya kufanya mabadiliko haya yalikuwa ni changamoto mbalimbali ambazo tumekuwa tukikutana nazo, lakini na baadhi ya sheria kuwa zimepitwa na wakati. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu kuzipitia upya na kufanya urekebu kidogo ili ziweze kunyumbulika na hali halisi ilivyo sasa na kuondoa baadhi ya changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosikia michango mingi iliyowasilishwa ikiwemo na ile ya maandishi, imejikita zaidi katika kuunga mkono hoja hii. Nasi tunawashukuru wachangiaji wote kwa michango hiyo mizuri ambayo ilianzia kule wakati wa Kamati na sasa leo tumeendelea kuipokea na tutaendelea kuiboresha kadiri iwekezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine nakushukuru tena na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, unatoa hoja, halafu wanaunga mkono. Badala ya kusema ninaunga mkono hoja, unatoa hoja ili waunge mkono.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niliyoyasema, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa sababu amehitimisha hoja zote mbili, zimeungwa mkono.

Baada ya kusema hayo sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 36A

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 37

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 37, Mwanasheria Mkuu wa Serikali halafu leo umekaa mbali. Ukiwa na hoja yako, kiti cha kukaa ni hapa ili uwe karibu na mimi hapa, kama sitaki kuongea kwa nguvu niweze kukufikia. Keti tu hapo usiwe na wasiwasi. Keti hapo, lakini hiki ndiyo kiti cha kupitishia hoja zako.

Sawa, hii ya 37 ni uandishi ambayo hatutaweza kubadili hapa, lakini Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na *CPD* huu uandishi umeandikwa hapa kwenye kifungu cha 37(a)(3) inasema; "*An irrigators' organization established and registered.*"

Sasa najua kwenye utungaji wa sheria ukiacha ile *magistrates'* huwa tunaendelea pale mbele. Hawa wengine nadhani huwa tunaandika kitu *complete* bila ya hii *possessive apostrophe*. Sasa hii ya *possessive apostrophe* kuna watu wamesoma Kiingereza humu ndani watasema hapa inaingiaje? Nadhani wewe utakuwa umenielewa, yaani matumizi ya lugha hii huwa inabidi yawe yamenyooka, ndiyo lugha ya kisheria.

Tukiishaanza kuingiza ile lugha nyingine, Mawakili watakosa kazi ya kufanya. Tukirahisisha lugha ya kisheria Mawakili watakosa kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 41

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 41, kina marekebisho ya Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali nimejaribu kupitia huku, kusudio lilikuwa ni nini? Nikaona kusudio linarejea kwenye Kifungu ambacho kwenye Katiba tayari ibara ipo. Hiki Kifungu kazi yake ni nini hapa? Hiki Kifungu cha 41 kina shughuli gani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndiyo kile Kifungu ambacho kina lengo la kuweka yale mafao ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**MWENYEKITI:** Sasa hakikuweka hayo mafao, jambo ambalo pia ukipitia ile sheria ni kweli, yaani hakuna mahali panaeleza huyu kama atalipwa chochote au halipwi. Hapa tumetoka kuongeza kifungu kwa ajili ya Katibu Mkuu Kiongozi, tukataja pale, lakini hapa ni sawa tu pia tukiamua kwamba tusitaje. Ila sasa namna kifungu chenyewe kilivyoandikwa, ukienda kusoma ile ibara ya Katiba inachosema, na Sheria yenyewe iliyopo sasa hivi inachosema, yaani unaona kwamba hiki kifungu ni kama hakina maana kuwekwa hapa.

Maadamu hatuna nia ya kutaja ni kitu gani atapewa, sasa hiki kifungu ni kwa ajili ya kazi gani? Kwa sababu hata hapa hatujasema atapewa nini? Tumesema Rais ndiye atakayesema, na hata hivi vingine vili-*envisage* hivyo hivyo, ndiyo maana

vikaacha kimya. Sasa tumeweka, lakini hatujasema. Sasa sijui tulikusudia nini?

Tena hiki cha pili ndiyo kabisa kinaleta vurugu, kwa sababu kinataka twende tena kwenye kifungu cha Katiba ambacho kipo tayari. Sasa kinamtuma tena Rais aende kule halafu kinaongezea na maneno mengine, "*as well as the nature of functions*", Yaani akaanze tena kujiuliza *nature* ya *function* za *CAG!* Mlikusudia nini hapo ili tujue hiki kifungu kiende, au vipi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusudio lilikuwa ni hilo, pengine labda nitashauriana kidogo na wataalamu namna ya kukiweka vizuri, lakini kusudio lilikuwa ni hilo.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kama kusudio ni hilo kwa kuanzia, kwa sababu hakuna mahali panaposema hata kumtaja kwamba Mheshimiwa Rais ndiye atakayeamua kwenye ile sheria, na kwenye Katiba hakipo, hiki kifungu kidogo cha kwanza kikiwepo hapa hakina madhara, japokuwa hatujasema atapewa nini? Hakina madhara, ila hiki cha pili kwa sababu kule tayari kipo na uandishi wenyewe uliojitokeza hapa, "*shall have regards*", mimi sijaelewa kabisa. Hii "*shall have regards*" ndiyo nini Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakiangalia hiki cha pili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiki cha kwanza nadhani kinaendana na malengo ya Serikali ambayo walikusudia. Sasa kwa sababu tunaitunga kwa Kiingereza, japokuwa hawaja-*enumerate* kwamba anapewa kitu gani kama walivyosema kwa *Chief Secretary,* lakini hapa hapana madhara kwa kusema kwamba atakuwa na mafao na yatakuwa yanaamuliwa na Rais. Kwa hiyo, ni jambo zuri tu kutaja. Ni hatua njema.

Hiki cha pili, ule uandishi wake kidogo umekaa katika mazingira tatanishi. Kwa hiyo, hiki mkakitazame, tunapitisha hicho cha kwanza peke yake. Kwa hiyo, haitakuwa 4(a)(1), itakuwa 4A kitabaki hicho cha kwanza.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijiridhishe kidogo. Nina wasiwasi kuki-*drop.*

**MWENYEKITI:** Ninakupa dakika chache jiridhishe.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya.

**MWENYEKITI:** Ninyi huku nyuma muwe mnajiridhisha, maana huku mmeandika *"as regard,"* sijui *"nature and functions of the Controller and Auditor General"* na ni kifungu kinachojitegemea peke yake.

Jamani, Mwenyekiti wa Kamati unaweza ukawa unakitazama pia, siyo Mwanasheria Mkuu peke yake, na wanasheria wengine mlioko humu. Sijui nianze kuwataja na nyie muwe mnaangalia.

Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama ulivyosema ni kweli ki-*drafting* haijakaa sawa kwa sababu *Article 1.4.4.6* imeweka hivyo, lakini mantiki yetu wakati tunajadiliana na Serikali, inatoa tu *guidance* kwamba pamoja na kwamba *president* ndiye mwenye *power ya* ku-*vary* lakini a-*vary* akifahamu kwamba *Article 1.4.4.6* huyu mtu hapewi kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa lugha tu ya Kiswahili ya mjini ni kwamba alijaribu kumwangalia *in a way* kwamba huyu mtu hapati kazi nyingine. Kwa hiyo, *its just a reminder* kwa sheria pamoja na kwamba ipo kwenye Katiba, ndiyo maana tuliona kwamba *it is not fatal.*

**MWENYEKITI:** Haya mwanasheria mwingine ambaye yuko na hicho kifungu hapo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikiacha kinaweka msisitizo na tukiki-*drop* pia hakina madhara. Kwa hiyo, ninashauri tukiache. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kama ikitokea kwamba mnataka kuangalia sasa haya mafao ya CAG kwa ujumla, hii sehemu ya Katiba kama mnataka itajwe huku, mnaweza kuitaja pale mwanzo. Hiki Kifungu kidogo cha pili kwenye ile *drafting* hakijakaa vizuri.

Sawa, kwa hiyo, tunarejea pale, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amejiridhisha 4A ndiyo itakuwepo hapo, hiyo *(1)* itakuwa inaondoka na ile (2) ndogo inaondoka.

Wanasheria mlioko humu ndani na wote mkishakuwa kwenye hii wote ni wanasheria, wote tunatunga sheria saa hizi. Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Bunge Zima Kifungu kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Serikali inapendekeza kupanga upya Kifungu cha 20 hadi 41 kuwa Kifungu cha 19 hadi 40.

**MWENYEKITI:** Mpangilio mpya wa vifungu unaafikiwa?

*(Mpanglio Mpya wa vifungu uliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024]* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024]* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imeungwa mkono. Unarejea? Utarajea tena baadaye.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sawa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mwanasheria Mkuu kusoma hivyo, sasa tunaendelea na utaratibu wetu. Samahani ninawahoji kwanza kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024]*. Wote mmeafiki. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali zipatazo sita kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to Keep the Laws Updated with some Challenges Observed in its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024] ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kusomwa mara ya tatu kwa utaratibu ambao tumejiwekea, maana yake Muswada huu umeshapita kwenye hatua zote za Bunge kwenye kutunga sheria.

Sasa nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024],* umetungwa rasmi na Bunge.

Kwa kusema hivyo, nampongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wote chini yake, Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, na wataalamu wetu wa Bunge kwa kuhakikisha jambo hili linaweza kufikia hatua hii ambapo sasa tumekamilisha na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa sheria hii. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ninamwita tena Katibu ili tuendelee na Muswada mwingine uliobaki.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano ya Muswada huu ambayo ni Kifungu cha 16 mpaka Kifungu cha 21, bado inafanyiwa kazi.

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada huu ambayo ni Kifungu cha 33 mpaka Kifungu cha 39 bado inafanyiwa kazi.

Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, Serikali inapendekeza kupanga upya vifungu vyake.

**MWENYEKITI:** Mpangilio mpya wa vifungu unaafikiwa?

*(Mpangilio Mpya wa vifungu uliafikiwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws*

*(Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024]* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024]* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024]*. Wote mmeafiki, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Sita kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria *hizo (A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to Keep the Laws Updated with some Challenges Observed in its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024] ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu, na kwa utaratibu wetu, tumemaliza kazi yetu ya kutunga sheria.

Baada ya kumaliza zoezi hilo, sasa nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2024],* umepitishwa rasmi na Bunge.

Sasa kwa utaratibu wetu, tutaipeleka Miswada hii miwili kwa Mheshimiwa Rais ili naye aweze kufanya kwa sehemu yake kwa kadiri anavyotakiwa na Katiba.

Kwa kusema haya, nampongeza tena Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna ambavyo hizi sheria ambazo amezileta mbele yetu kama alivyoeleza, sababu nyingine zimepitwa na wakati na nyingine zilihitaji maboresho ili utendaji uwe mzuri zaidi. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wenu. Wakati huo huo nawashukuru kwa ushirikiano mzuri mnaoutoa kwa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa mawazo wanayoyaleta kwenu na ninyi mnayachukua na kuyafanyia kazi. Tunawashukuru kwa ushirikiano.

Pia, Kamati yetu tunawapongeza kwa kazi nzuri ya kuendelea kusimamia mabadiliko haya ya sheria mbalimbali yanayojitokeza kwa sababu ni dhahiri sheria hizi zinakuwa za sekta mbalimbali, lakini mnaweza kuzifanyia kazi pamoja kwa ushirikiano na Wabunge wote wanaozisimamia sekta nyingine. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati yetu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali uendelee na ushirikiano huu ambao unautoa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi na shukrani hizo na ninyi mlioshiriki zoezi zima hili kuhakikisha Bunge linakamilisha

kazi yake ya Kikatiba, ninawashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na yale niliyoyasema wakati tukiwa tumekaa kama Kamati ya Bunge Zima, zoezi hili la utungaji wa sheria kama Waheshimiwa Wabunge mnavyofahamu ni zoezi zito kidogo, lakini huwa tunahitaji msaada wa wataalamu ili nasi tuweze kwenda vizuri.

Sasa katika haya marekebisho ambayo tusingeweza kuyafanya katika ngazi hii, lakini ni kujaribu kutazama huko baadaye, lugha ile ya kisheria ndiyo ambayo tunapaswa kutumia ndiyo maana tunawatumia ninyi kama wataalamu. Katika sehemu ya yale mabadiliko ambayo tumeyafanya leo na huko baadaye mtayatazama tena. Mmetumia lugha ya wingi hivi, sasa inaonekana kama huyu akiwa mmoja, hayo siyo masharti yake, yaani mpaka awe ameungana na mwingine.

Kwa mfano, Kifungu cha 11(2) kwenye ile sheria ya mambo ya umwagiliaji kinaongelea *regional irrigation engineers.* Sasa je, akiwa mmoja? Katika ule utungaji wa sheria inabidi wakiwa wengi wanafuata yale na akiwa mmoja pia afanye hayo hayo, na sasa imeanza na maneno "*a regional irrigation engineers.*"

Sasa leo tumebadilisha kifungu hiki kwa kumwongeza yule wa wilaya, lakini lugha iliyotumika ni hiyo hiyo na yenyewe inaongelea kama vile inazungumzia hawa lazima wawe wote. Inasema, "*a regional and district engineers*" sijui kitu gani? Sasa ukiweka maneno kama hayo, maana yake ni lazima wawe pamoja.

Kama unakusudia yale yawe ya *district* pia yawe ya *regional,* maana yake unatumia neno "*all*" badala ya "*and*". Ukitumia "*and*" tafsiri inaweza kumaanisha awepo huyu wa *regional* na *district* ndiyo hayo wayafanye, kwa sababu hizo sasa zitakuja, ni tafsiri na tutaanza sasa kubishana. Kwa hiyo, inabidi tuziweke lugha zetu katika ile lugha ya kisheria, lakini pia kuondoa ule mkanganyiko unaoweza kuja saa ya kutoa tafsiri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.46 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Januari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*